

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Tano – Tarehe 8 Februari, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa Mbunge afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu:-

Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi

SPIKA: Katibu shunguli inayofuata.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) na Mapendekezo

ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) na Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza linakwenda Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, kwa niaba yake Mheshimiwa Cecilia Pareso.

Na. 58

Ubovu wa Eneo la Katokoro

MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza eneo la Katokoro linalounganisha Kata za Katoro na Kyamulaile katika Jimbo la Bukoba Vijijini ili kuondoa adha ya usafiri inayowakabili wananchi wa maeneo hayo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Festo John Dugange, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo korofi la Katokoro ambalo limejaa maji lina urefu wa kilomita 5 ambayo ni sehemu ya barabara ya Katoro – Kyamulaile – Kashaba yenye jumla yakilomita 15.7 inayounganisha Kata za Katoro, Kyamulaile na Ruhunga. Aidha, barabara hiyo pia inaunganisha maeneo mbalimbali ya Halmashauriya Wilaya ya Bukoba na Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) imefanya usanifu kwa ajili ya kuboresha eneo hilo korofi ambapo kiasi cha fedha shilingi milioni 572 kinahitajika kunyanyua tuta la barabara na kujenga makalvati.

Mheshimiwa Spika, ili kupata ufumbuzi kwa sasa katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 87 kwa ajili ya kurekebisha eneo korofi katika barabara hiyo. Hata hivyo, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkandarasi aliyekuwa anafanya kazi hiyo alisimamishwa kutokana na eneo hilo kujaa maji.

Mheshimiwa Spika, wakati jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa kudumu wa barabara hiyo zikiendelea, mara maji yatakapopungua, mara moja Serikali itamrejsha kazini mkandarasi huyo ili kurejeshwa mawasiliano katika eneo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Paresso, nimekuona nimekuona.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana lakini kwenye *tablets* zetu hatuna *Order Paper*.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kumekuwa na utamaduni wa fedha nyingi zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji miradi mbalimbali ya barabara kucheleweshwa hivyo ufanisi wa kile kinachokusudiwa hakifikiwi. Je, Serikali sasa mko tayari kuhakikisha kama fedha zinatengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara yoyote zinatoka kwa wakati ili barabara hizo zitengenezwe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya Karatu inatoka Njia Panda – Mang’ola - Lalago ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. Barabara hii imekuwa ikiahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami hasa kipindi cha uchaguzi ahadi inakuwa ni tamu kweli masikioni mwa wananchi lakini baada ya hapo barabara hiyo haijengwi kiwango cha lami. Serikali mtuambie ni lini kwa hakika barabara hiyo itajengwa kwa sababu Sera ya Wizara ya Ujenzi inasema kuunganisha barabara za Mikoa na Mikoa kwa kiwango cha Lami na barabara ile inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za miradi mbalimbali ya barabara kuchelewa kupelekwa katika miradi hiyo, utaratibu wa fedha kupelekwa katika miradi mbalimbali unazingatia upatikanaji wa fedha ambazo zimetengwa kwenye bajeti husika. Hivyo, kutokana na kutegemea mapato

ya ndani kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, mara nyingi kumekuwa na ucheleweshwaji na miradi hiyo kwa sababu ya upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuongeza jitihada kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa kwa wakati na fedha za miradi hiyo zinawasilishwa kwenye miradi husika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha mpaka sasa takribani asilimia 48 ya fedha ya miradi ya barabara tayari imekwishawasilishwa katika mamlaka ya Serikali za Mitaa na kazi za utekelezaji wa miradi hiyo zinaendelea. Suala hili litaendelea kufanyiwa kazi kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na barabara ya Arusha Simiyu inayotokea Karatu, ni kweli hii ni barabara muhimu sana na inaunganisha mikoa hii miwili. Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba barabara hizi kuu ambazo zinaunganisha mikoa zinajengwa kwa kiwango cha lami ili kurahisisha shughuli za kiuchumi na za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kama alivyouliza kwamba Serikali imekuwa ikitoa ahadi, ni kweli na ahadi ya Serikali hakika itatekelezwa. Nimhakikishie tu kwamba mara fedha zikipatikana barabara hiyo itajengwa ili wananchi waweze kupata huduma zilizokusudiwa.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa za kuboresha miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Conchesta kwamba tayari kazi ya kuboresha barabara ile inaendelea ili iweze kupitika ambapo sasa hivi wanafanya kazi za kuchepua maji, kuweka mawe na changarawe. Vilevile napenda kumfahamisha Conchesta kwamba mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo

la Bukoba Vijijini tumeshawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na barabara hii itafanyiwa kazi kwa kuzingatia mpango kazi uliowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa umuhimu wa kipande hicho cha barabara unafanana na barabara ya Kanazi - Kyaka kupitia Katoro, ni lini barabara hiyo nayo itatengewa fedha na kujengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Kanyazi, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuboresha miundombinu ya barabara ikiwepo barabara hii ya Kanazi, Kyaka kupitia Katoro. Kimsingi tathmini na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kujenga barabara hizi unaendelea. Mpango umeandaliwa kwa ajili ya kufanya tathmini lakini kuhakikisha kwamba barabara hizi zinatafutiwa fedha ili ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutekeleza mipango yake hii ya kufanya tathmini lakini pia kutafuta fedha ili barabara hizi ziwezwe kujengwa na kusogeza huduma kwa wananchi.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Yahaya Omar Masare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, siku hizi sijui unakaa upande gani, uliza swali lako Mheshimiwa Masare.

Yaani CCM wote, haya tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali litaulizwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo.

Watu wa *IT*, hebu wekeni maswali haya haraka kwenye *tablets*.

Na. 60

Ongezeko la Wanyamapori katika Hifadhi ya Selous

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la wanyamapori katika Hifadhi ya Mbuga ya Selous na sasa tembo na nyati wanavamia mashamba pamoja na makazi ya wanavijiji na kuleta taharuki:-

Je, Serikali inaweza kuwarudisha wanyama hao porini mbali zaidi na wananchi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mary Francis Masanja, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mali asili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa na inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha utaratibu wa kuweka alama katika shoroba na mapito ya wanyamapori ili kuimarisha uhifadhi wake na kuendelea kufanya utafiti na kueneza matumizi ya mbinu mbadala za kujikinga na wanyamapori waharibifu hasa tembo. Baadhi ya mbinu hizo ni: Matumizi ya pilipili, mafuta machafu (*oil*) na mizinga ya nyuki; na kutoa mafunzo kwa askari wa wanyamapori wa vijiji. Katika Wilaya ya Namtumbo, jumla ya askari wa wanyamapori wa vijiji 198 wamepewa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikiendelea kufanya doria za msako kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu ambapo katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2020 zilifanyika doria za msako zenye jumla ya sikuwatu 133 katika vijiji vya Wilaya ya Namtumbo; kutoa elimu kwa wananchi juu ya mbinu za kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu ambapo jumla ya wananchi 2,303 walipata elimu katika vijiji 42 vya Wilaya za Namtumbo na Tunduru; kuimarisha vituo maalum vya doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika Kanda za Kalulu na Likuyu-Sekamaganga.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa jambo hili ni la dharura kwani kwa sasa wakulima wamelima, wamepanda, wamepalilia na kutia mbolea katika mashamba yao kwa thamani kubwa lakini makundi ya tembo yameingia na kuvuruga mashamba hayo na wakulima wamepata taharuki hasa baada ya mkulima mmoja kuuwawa na tembo hao. Je, Serikali inaweza sasa kupeleka kikosi maalum kufanya *operation* ya kuwaondoa na kuwafukuza tembo hao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa jambo hili linasababishwa pia na makundi ya ng'ombe waliondolewa katika maeneo ya Mkoa wa Morogoro na kuingia katika maeneo ya hifadhi ya tembo hawa na kuharibu *ecology* yake na kufanya tembo hawa kufika kwa wananchi. Je, Serikali kwa kutekeleza azma ya Mheshimiwa Rais aliyoitoe katika hotuba yake ukurasa wa kumi na sita hapa Bungeni kwamba itaongeza maeneo ya hekta kufika milioni sita...

SPIKA: Fupisha swali Mheshimiwa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, Serikali imejipangaje kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuongeza maeneo ya wafugaji ili kuondoa mgongano huu?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Vita. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Francis Masanja, leo utajibu maswali hapa, yapo manne hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tayari *tablets* zenu zote zina maswali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge la Jimbo la Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ambalo amesema kupeleka vikosi kazi kwa ajili ya kwenda kushughulikia uvamizi wa tembo; Serikali ipo tayari na hata leo anavyowasilisha tayari Serikali ilishafanya mchakato wa kuhamisha hao tembo na inaendelea kuwaondoa katika maeneo hayo ya mashamba na shughuli za kibinadamu. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Kawawa, kwenye hili suala la uvamizi wa tembo katika maeneo yanayozunguka au ya kandokando ya hifadhi kwamba, Serikali ina vikosi ambavyo viko katika Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kutumia Jeshiusu inaendelea kuwaondoa hawa tembo na wanyama wengine wakali ili kuwawezesha binadamu kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kundi la ng'ombe kwamba wanahamia kwenye maeneo ambayo yamepakana na hifadhi; naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba Kamati ya Mawaziri iliundwa na Serikali kuangalia maeneo yote yenye migogoro ikiwemo migogoro inayozunguka mipaka yote ya hifadhi. Sasa hivi Kamati hii ilishamaliza kazi yake na utekelezaji wake unaenda kuanza baada ya Bunge hili Tukufu kumalizika. Hivyo maeneo yote ambayo yana migogoro kama ya namna hii Serikali inakwenda kuyamaliza na niwaondoe wasiwasi

Waheshimiwa kwamba wote ambao wana changamoto hii inakwenda kumalizwa na maamuzi ya Kamati ya Mawaziri. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

Na. 61

Mgogoro wa Mipaka Kati ya TANAPA na Wananchi

MHE. FESTO R. SANGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarudia zoezi la kuweka alama za mipaka kwa kuwashirikisha wananchi ili kumaliza mgogoro uliopo wa mipaka kati ya Hifadhi ya Kitulo na wananchi wa Vijiji vya Misiwa, Makwalanga, Igofi na Nkondo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2016, Serikali ilishaweka alama za mipaka za kati kwenye maeneo ya Hifadhi ya Taifa Kitulo inayopakana na vijiji vya Misiwa, Mwakalanga, Igofi na mwaka 2018 katika Kijiji cha Nkondo.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la uwekaji wa alama lilishirikisha Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Makete, Waheshimiwa Madiwani, Serikali za Vijiji, wananchi kwa ngazi ya vijiji, pamoja na wataalam wa ardhi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Makete. Elimu ilitolewa kwa wananchi kuhusu zoezi la uwekaji alama za mipaka kwenye vijiji hivi kabla ya uwekaji wa alama za mipaka hiyo. Baada ya utoaji wa elimu, wananchi walichagua wawakilishi watano katika kila kijiji ili

kujiunga na timu ya watumishi kutoka Hifadhini na wataalam wa ardhi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Makete, ili kufanya utambuzi wa eneo la mipaka na kuweka mipaka hiyo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na.279 la Mwaka 2005 la uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa Kitulo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba maeneo hayo tajwa yalikuwawekewa alama za mipaka na zoezi hilo lililishirikisha wananchi kikamilifu. Lengo kuu la zoezi hilo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa mipaka inaonekana bayana na pia shughuli za kibinadamu hazifanyiki ndani ya eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kwamba mgogoro wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa Kitulo na vijiji vilivyotajwa ulishapatiwa suluhu kwa kuzingatia Tangazo la Serikali na tunachokiomba kutoka kwa wananchi ni ushirikiano wao ili kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi.

SPIKA: Mheshimiwa Festo, wanasema hakuna mgogoro.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Majibu ya Serikali hayajaniridhisha kwa sababu wananchi wetu kwenye zoezi hili la kuweka *beacon* walishirikishwa kuweka *beacon* tu, hawakushirikishwa kwenye mipaka itawekwa maeneo gani.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili tuongozane kwenda Makete tukawape majibu wananchi wetu na kurudia zoezi la kuweka *beacon*? Kwa sababu zoezi hili limesababisha wananchi wangu wengi saa hizi wako ndani lakini sehemu ya shule zimewekwa *beacon*...

SPIKA: Mheshimiwa Festo...

MHE. FESTO R. SANGA: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari twende wote?

SPIKA: Nisikilize kwanza; swali lako halijaeleweka kabisa, kwamba wananchi wako wlaishirikishwa kuweka *beacon* lakini hawakushirikishwa mahali pa kuweka, sasa...

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, kilichotokea wananchi wamefika wamekuta watu wa kutoka Serikalini wanaweka *beacon*, hawajaambiwa kwamba ni eneo hili la mpaka au wapi. Kilichotokea nyumba nyingi za wananchi ziko ndani ya hifadhi, kitu ambacho hakikuwepo, siku za nyuma mipaka ilikuwa mbali. Leo hii wananchi wangu wengi wako ndani ni kwa sababu ya hilo jambo. Sasa ninachomuomba Naibu Waziri tuongozane baada ya hili Bunge twende Makete akawape wajibu wananchi wetu turudie zoezi; hicho ndicho ninachomwomba. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Festo unapaswa kumwomba Spika ili uongozane na Waziri, sasa kama unamwomba Waziri ruhusa hiyo hakuna. Mheshimiwa Waziri majibu tafadhali. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara iko tayari kuhudumia wateja wa aina yoyote akiwemo Mheshimiwa Sanga, hivyo naahidi baada ya Bunge lako Tukufu nitaongozana naye nikiwa na wataalam kwenda kuonesha hiyo mipaka ili wananchi watambue mipaka ya hifadhi ni ipi na iendeleo kuheshimiwa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Namwelewa Mheshimiwa Festo anachokipigania. Watu wa Maliasili wana tabia, wanakubaliana na wananchi wanapoenda kuchora na kufanya nini, wanapokuja wanaongeza, yaani hii ndiyo tabia ambayo ni vizuri mkaielewa na ndiyo chanzo cha migogoro inavyokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, tafadhali.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza na linakwenda kabisa sambamba na tatizo alilionalo Mheshimiwa Sanga kule Kitulo. Zoezi la uwekaji mipaka ya Hifadhi za Taifa na maeneo ya jamii halikuwa shirikishi kabisa katika Jimbo langu la Longido katika eneo linalotutenga na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro. Kuna eneo la *buffer zone* la hekta 5,000 ambazo lilitengwa tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza kwamba liwe ni eneo la *buffer zone* lakini matumizi yaliyoruhusiwa ni kuchunga tu. Hivi leo baada ya *beacon* kuwekwa bila kuwashirikisha wananchi wanaanza kupelekeshwa kuchungia katika *buffer zone*. Naomba kuiuliza Wizara, je, wako tayari kutoa tamko kwamba eneo la *buffer zone* katika ukanda wa msitu wa Mlima Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa zina *access* ya wachunga mifugo wa Longido na Siha kuchungia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Masanja.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maeneo ya *buffer zone* yana miongozo yake na Wizara itaangalia kama inaruhusu kutumika kwa shughuli zingine. Hata hivyo, kwa sababu Kamati ya Mawaziri ilishafanya maamuzi ikapitia baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa na migogoro na maamuzi hayo tunatarajia kwamba yataanza kutekelezwa baada ya Bunge lako hili Tukufu, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba awe na subira tumalize Bunge, tuangalie sasa kama yale maeneo anayoyasema yeye yatakuwa ndani ya maamuzi ya Kamati ya Mawaziri ambavyo vijiji 920 tayari vitakuwa vimefaidika na maeneo hayo. Kama kitakuwa hakimo basi Wizara itaendelea kushirikiana naye kuangalia ni kitu gani ambacho tunaweza kufanya ili tusiweze kuathiri maeneo ya machunga (malisho) na kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Kwenye michakato hii kuna maneno mawili; kuna maneno kuhusishwa na kuna maneno kushirikishwa. Wanachofanya wanakuja kuwahusisha wananchi, halafu wanafanya wenyewe. Ukiwauliza wanakwambia tuliwashirikisha, kumbe haya maneno ni mawili tofauti. Wanawahusisha na siyo kuwashirikisha. Kwa sababu kama mlirikishana kwa nini pawe na *dispute*? Hakuna sababu.

Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, uliza swali lako.

Na. 62

Mpango wa Kumaliza Migogoro ya Mipaka katika Hifadhi ya Taifa Tarangire

MHE. SILLO D. BARAN aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi ya Tarangire na Vijiji vya Gijedabung, Ayamango, Gedamar na Mwada katika Jimbo la Babati Vijijini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, bado tupo kwako; Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilihakiki mpaka wa Hifadhi ya Taifa Tarangire mwaka 2004 kwa kutumia Tangazo la Serikali Na. 160 la tarehe 19 Juni, 1970 ambapo alama za mipaka ziliwekwa ardhini. Kazi hiyo ilifanywa na wataalam kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, uhakiki huo ulibainisha kuwa: (i) hifadhi ilikuwa imechukua baadhi ya maeneo ya Vijiji vya Mwikantsi (Hekta 1,014) na Sangaiwe, Kata ya Mwada (Hekta 536), hivyo maeneo haya yalirejeshwa kwa wananchi. (ii) wananchi pia, walichukua maeneo ya hifadhi katika Vijiji vya Ayamango (Hekta 2,986.3), Gedamar (Hekta 2,185.1), Gijedabung (Hekta 1,328.2), Quash (Hekta 1,587.9) na Orng'andida (Hekta 930.6) ambavyo vimerejeshwa.

Mheshimiwa Spika, katika Vijiji vya Quash na Orng'ndida maeneo yaliyoangukia ndani ya mpaka wa hifadhi hayakuwa na watu, hivyo ilikuwa rahisi kuyarejesha hifadhini. Upande wa maeneo ya Vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gijedabung uthamini wa mali za wananchi ambao walikuwa ndani ya mpaka wa hifadhi ulifanyika. Jumla ya kiasi cha shilingi za Kitanzania 175,050,924 zililipwa kwa wananchi hao kama fidia ya mali, posho ya usumbufu, posho ya makazi na posho ya usafiri kwa wote waliotakiwa kuhama. Malipo hayo ya fidia yalifanyika kama ilivyokuwa imepangwa na wananchi waliondoka ndani ya hifadhi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu marefu, wakati mwingine yawe mafupi kidogo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri,.

Mheshimiwa muuliza swali naamini ulishapata majibu ya mwanzo; swali la nyongeza.

MHE. SILLO D. BARAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa bado mgogoro huu unafurukuta katika vijiji nilivyovitaja, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufanya ziara ili wananchi wapate kutatua migogoro hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili...

SPIKA: Kwa nini Waheshimiwa mnamgombea Mheshimiwa Waziri kama mpira wa kona aje majimboni kwenu?

Endelea Mheshimiwa swali la pili.

MHE. SILLO D. BARAN: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka 2019 ulitokea uharibifu wa mazao ya wananchi katika vijiji nilivyovitaja ambao ulisababishwa na wanyama hasa tembo, je, ni lini Serikali itawalipa kifuta jasho wananchi hawa ambao mashamba yao yameathirika?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mary Francis Masanja tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Sillo juu ya kuongozana na mimi maana ni majukumu yangu ya kazi, hivyo hilo niko tayari baada ya Bunge lako hili Tukufu tutaenda naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza ambalo ameuliza juu ya uharibifu wa wanyama wakali; Serikali inawajali sana wananchi wake na inatambua kwamba kuna uharibifu wa wanyama wakali ambao wamekuwa wakiwasumbua wananchi hasa wale ambao wanakuwa wamepanda mazao yao na wanyama wakali hususan tembo huenda katika maeneo hayo na kuharibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua hilo ilianzisha Mfuko ambao huwa tunalipa kifuta jasho au kifuta machozi. Kifuta machozi au kifuta jasho ni kwa ajili ya kuwapoza wale ambao wanakuwa wameathirika na changamoto hii ya wanyama wakali. Hivyo, hadi Machi, 2020, Serikali ilikuwa imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 5.9 kwa ajili ya kifuta machozi au kifuta jasho kwa wananchi hawa ambao wamekuwa wakiathirika na changamoto ya wanyama wakali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kuhakiki madai yote ambayo wananchi wameathirika na changamoto hii ya wanyama wakali na itaendelea kulipa kadri inavyopata taarifa.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa leo ndiyo Waziri anajibu maswali kwa mara ya kwanza kabisa, hamumwonei hata huruma jamani? (*Kicheko*)

Swali la mwisho kwa Wizara hii ya Maliasili, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini.

Na. 63

Ongezeko la Viwango vya Tozo za Utalii Nchini

MHE. MRISHO M. GAMBO aliuliza: -

Serikali imeongeza viwango vya tozo za utalii kwa Hifadhi zilizo chini ya *TANAPA* kuanzia mwezi Julai, 2021.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusitisha tozo hizo ili kutoa fursa kwa Sekta ya Utalii nchini ambayo imeathirika sana na ugonjwa wa *Corona*?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Francis Masanja tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ongezeko la tozo limelenga Hifadhi za Taifa nne ambazo ni Ziwa Manyara, Serengeti, Tarangire na Arusha. Kiwango cha tozo kilichoongezeka kwa

hifadhi husika ikilinganishwa na viwango vya sasa ni kama ifuatavyo: -

HFADHI	ENTRY FEE		SEASONAL AND SPECIAL CAMPING FEE		CONCESSION FEE	
	Tozoya sasa	Tozokuanzia 1/7/2021	Tozoyasasa	Tozo kuanzia 1/7/2021	Tozoya sasa	Tozo kuanzia 1/7/2021
Serengeti	60 USD	70 USD	50 USD	60 USD	50 USD	60 USD
Manyara	45 USD	50 USD	50 USD	60 USD	40 USD	40 USD
Tarangire	45 USD	50 USD	50 USD	60 USD	40 USD	40 USD
Arusha	45 USD	50 USD	50 USD	60 USD	40 USD	40 USD

Mheshimiwa Spika, wakati wafanyabiashara ya utalii wakiishinikiza Serikali kuacha tozo zikiwa za chini sana, wenyewe wamekua wakiwatoza watalii tozo za juu ambazo hawataki kuziweka wazi kwa Serikali. Usiri wa tozo za makampuni binafsi unainyima Serikali taarifa za msingi za kuweza kuona uzito wa hoja yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwamba suala la COVID-19 lisitumike kuinyima Serikali mapato ambayo yanasaidia kukuza uchumi wa nchi. Pia, nisisitize kwamba pamoja na shinikizo la kupunguza tozo, sekta binafsi haijawasilisha takwimu zozote Serikalini za kuthibitisha ongezeko la idadi ya wageni waliofuta safari zao kuja nchini kutokana na ongezeko la tozo.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Mrisho Gambo.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, naomba niweke wazi tu kwanza kwamba sija ridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake sekta ya utalii kwa Mkoa wa Arusha na nchi nzima imeathirika sana. Wananchi wengi sana wamekosa ajira, madereva wamekosa ajira kwa sababu magari hayatembezi kutokana na uchache wa watalii, *guides* wamekosa ajira, wafanyakazi wa mahoteli wamepunguzwa kwenye maeneo yao, magari

ambayo yangetembea, yangeweka mafuta *shell* zingeweza kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwenye ukanda wa Afrika Mashariki, karibu nchi nyingi zimeweza kupunguza tozo kipindi hiki. Mfano, Kenya, *Nairobi National Park* wamepunguza tozo kutoka Dola 43,000 mpaka 35,000. Ukienda Rwanda kwenye masuala ya *gorilla* wamepunguza kutoka Dola 1,500 mpaka Dola 500. Ukienda Uganda kwenye masuala pia ya *gorilla* wamepunguza kutoka Dola 700 mpaka 500. Naomba Wizara ya Maliasili na Utalii iangalie athari za ugonjwa wa *Corona* kwenye masuala ya ajira na masuala mengine.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mpango gani wa kuipa ahueni sekta ya utalii ili kuweza kunusuru changamoto kubwa ya ajira ambayo imewaathiri wananchi wa Mkoa wa Arusha pamoja na Tanzania kwa ujumla?

SPIKA: Swali hili ni la msingi sana. Majibu ya swali hilo, Waziri mwenyewe wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro tafadhali. (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Gambo ametoa takwimu, wenzetu wamepunguza kutoka Dola 1,500 mpaka 1,000, kutoka Dola 700 mpaka 500; hizo ndiyo takwimu zake. Viwango vya kuingia katika hifadhi zetu bado viko chini sana ukilinganisha na ubora wa hifadhi tulizonazo. Ukisema Serengeti hulinganishi na hifadhi yoyote iliyoko katika Afrika Mashariki; kule Rwanda unaona *gorilla* tu. *Serengeti is a jewel*, bado ni Dola 60. Kwa hiyo, viwango bado viko chini sana. Nilitaka kwanza hilo niliweke sawa.

Mheshimiwa Spika, la pili, Serikali inatoa tahafifu gani hasa kwa kipindi hiki? Wizara imegawa suala la utalii katika misimu miwili; *high season* na *low season*. Ongezeko hilo ambalo tunalisema litagusa kwenye *high season* tu; *low season* bado *rates* zitabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa nini? Katika *high season*, sehemu kama Ngorongoro kwa siku moja yanaingia magari 400 ambayo yanaathari kubwa kiikolojia wakati kwenye *low season* yanaingia magari 70. Tunataka tu-*balance* sasa, hawa wafanyabiashara wetu ambao tutawapa tahafifu, waende sasa kwenye *low season* ili tutunze pia na ikolojia iliyopo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, AJIRA, KAZI, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono majibu mazuri yaliyotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini swali la msingi na maswali ya nyongeza yamegusa pia sekta ya ajira katika sekta hiyo ya maliasili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu, wakati wa *Covid*, hata sasa na hata baadaye, kama kunatokea tatizo lolote linalohusiana na suala la wafanyakazi, tunaomba wafanyakazi, waajiri watumie *platform* yao ambayo ni ya dhana ya utatu ambayo tumekuwa tukiitumia mara nyingi kuamsha mijadala na kutafuta *solution* katika mazingira ya mawanda hayo ya sekta ya kazi, ajira na Serikali. Kwa hiyo, nawashauri watumie *platform* hiyo.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Gambo bado una nafasi, tunaelekea kwenye Mipango, unaweza ukafafanua zaidi hoja yako; tunaelekea kwenye bajeti. Ni hoja nzito na ya msingi, kwa sababu pana upungufu huo mkubwa sana yaani haiwezekani *graph* ya watalii inapungua halafu wewe unaongeza bei, ijenge tu vizuri hoja yako. (*Makofi*)

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, tafadhali.

Na. 64

Utoaji wa OC kwa Wakuu wa Polisi Wilaya

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa Wakuu wa Polisi wa Wilaya kama inavyotoa kwa Wakuu wa vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama?

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Masanja, pole sana. *(Kicheko)*

Sasa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mahali hapa, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa ametujalia tumekutana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii niwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Uzini kwa uzalendo na mapenzi makubwa ya kunichagua kwa kura nyingi nikawa Mbunge. Maana wamenitoa kutoka kwenye mavumbi, wamenitoa kwenye majalala, wamenileta kwenye viti, nimekaa na wafalme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii nimshukuru na kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, maana baada ya Mungu kuweka baraka, naye ikampendeza akaniteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa jibu swali Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kama Taasisi ya Serikali hupokea fedha za matumizi (*OC*) toka Wizara ya Fedha na huzigawa fedha hizo kupitia Kamati Maalumu ya Fedha (*Tanzania Police Force Resources Committee*), ambayo huzigawa fedha hizo kwenda kwa Makamanda wa Polisi wa Kanda Maalum, Mikoa na Vikosi; na hao ndiyo wenye mamlaka ya kupata *OC* kisheria.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kugawa fedha kwenda kwa Wakuu wa Polisi wa Wilaya hufanywa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa husika kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kila Wilaya, kama vile ukubwa wa wilaya, Idadi ya vyombo vya usafiri ilivyonavyo, ikama ya Askari na takwimu za matukio ya kihalifu yaliyopo. Ahsante.

SPIKA: Wizara ya Mambo ya Ndani hamjajibu hili swali, wanauliza kwa nini hamgawi ninyi sasa?

Mheshimiwa Husna endelea na swali la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Wizara ya Mambo ya Ndani, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia katika maeneo mengi, Jeshi la Polisi limeshindwa kufika kwa wakati kwenye matukio kwa sababu za kukosa mafuta na matengenezo ya magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ustawi wa jamii yetu unategemea sana ulinzi na usalama unaofanywa na Jeshi letu la Polisi. Swali la kwanza, je, Wizara haioni sasa ni wakati muafaka wa kufanya marekebisho hayo ya kisheria?

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara haioni ni muda muafaka sasa kupeleka hizo fedha moja kwa moja kwa Wakuu wa Polisi wa Wilaya badala ya kupitisha kwa Wakuu wa Polisi wa Mikoa ambapo imetengeneza urasimu? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Husna. Sidhani kama kuna sheria inayoagiza hilo yaani *issue* ni kwamba...

Karibu ujibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamza Khamis Khamis. Yaani Jeshi lilivyo Kamanda wa Wilaya hawezi kumhoji boshi wake. Sasa fedha ikija hapo juu, hata akipiga huyo wa juu, huyu wa chini hawezi kuhoji. Kwa hiyo, mnachotakiwa ninyi muwagawie; huyu mkubwa umpe zake na huyo wa Wilayani naye umpe zake. Ndiyo swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza amesema kwamba hatuoni haja ya kufanya mabadiliko ya sheria hii? Mabadiliko ya sheria siku zote yanakwenda na mahitaji. Inawezekana ikawa kuna hitaji la kufanya hivyo, lakini sheria hii ikawa iko hivi hivi mpaka tufike wakati tuone namna ambavyo tunaweza kufanya mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, nataka kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ukiangalia Sheria ya Bajeti, kuna kitu kinaitwa *vote holder* na kuna kitu kinaitwa *sub-vote holder*. Sasa *vote holder* moja kwa moja anayo *IGP* na *sub-vote holder* anayo *RPC*. Kwa hiyo, fungu likitoka kwa *IGP* linakuja kwa *RPC*. Huo ndiyo utaratibu halafu sasa ndiyo zinagawiwa Wilaya husika kama ambavyo tumeeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama sasa inafika wakati tunahitaji mabadiliko ya sheria hii, basi acha tulichukue hilo tukakae na wadau halafu tuone namna ambavyo tunaweza

tukalifanyia mabadiliko. Kwa sababu, suala la kufanya mabadiliko ya sheria *is a matter of procedure...* (Makofi)

SPIKA: Unajua Waheshimiwa Wabunge huwa mnapiga makofi ambapo hamjui hata mnapiga makofi ya nini? (Kicheko)

Ahsante, malizia kujibu. Umemaliza eeh!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Ndiyo.

SPIKA: Ahsante sana. Maana Waziri akakae na wadau, akina nani? Halafu tunashangilia, tunakubali hiyo kanzu. (Kicheko)

Mheshimiwa Jackline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 65

Elimu ya Sheria za Usalama Barabarani kwa Madereva wa Bodaboda

MHE. JACKLINE K. ANDREA aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mpango gani wa elimu ya sheria ya usalama barabarani kwa madereva wa bodaboda ili waendeshe kwa kutii sheria na kuepusha ajali?

SPIKA: Bado tuko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani limekuwa likitoa elimu kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani kwa madereva, bodaboda na watumiaji wengine wa barabara na vyombo vya moto kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani (*The Road Traffic Act No.68/1973*).

Mheshimiwa Spika, elimu hiyo hutolewa kwa kupitia Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, televisheni, radio, magazeti, vipeperushi mbalimbali, Maadhimisho ya Saba Saba na Nane Nane, matamasha mashuleni na kwenye vijiwe na maskani ya bodaboda. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka Desemba, 2020 jumla ya vipindi 399 vya Elimu ya Usalama Barabarani vimerushwa hewani na kuoneshwa mubashara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na vituo 89 vya *radio* na televisheni. Pia elimu imetolewa kwa madereva wa bodaboda 638,275 na kwenye vijiwe vya bodaboda 7,760 nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Wizara inashukuru sana wadau mbalimbali katika kutoa elimu hiyo ambayo ni *TRA, PUMA, AAT, APEC, Future World Training College* na *Amend*. Lengo ni kujenga ufahamu wa sheria na kuepusha ajali kwa madereva wa bodaboda na watumiaji wengine wa barabara. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Jackline, swali la nyongeza.

MHE. JACKLINE K. ANDREA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii niweze kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kwamba tunajua Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inajitahidi kupunguza ajali za bodaboda, tukiangalia kwa mwaka 2019 tulikuwa na ajali 567 lakini mwaka 2020 tuna 240. Je, Jeshi la Polisi lina mpango gani wa kuhakikisha ajali hizi zinapungua zaidi? Tukiangalia wahanga wakubwa ni

vijana na wanawake ndiyo wanaopata shida ya kupoteza vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; utafiti unaonyesha askari wastaafu wanachelewa kupata mafao yao, je, Wizara husika ina mpango gani wa kuhakikisha askari hawa baada ya kustaafu wanapatiwa mafao yao kwa haraka ili kuepusha wanapokuwa kazini kuchukua rushwa ili kujilimbikizia akiba?

SPIKA: Ahsante. Swali la pili liko pembeni kidogo, lakini jitahidi kulijibu pia. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu ya maswali hayo, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi inaonekana Mheshimiwa tumempa sababu moja au njia moja ambayo tunaweza tukaitumia katika kuepuka hizi ajali. Zipo njia ambazo tumeshazichukua kama Serikali na nyingine tuko mbioni kuzichukua kwa kushirikiana na Wizara nyingine au kushirikiana na taasisi nyingine kuhakikisha kwamba hizi ajali za barabarani zinapungua. Cha kwanza tumefikiria kuendelea kuwafundisha zaidi hasa vijana wa bodaboda namna ya kutumia alama za barabarani ambazo zina uwezo mzuri wa kuwaeleza kwamba wanakoelekea wanaweza wakapata ajali.

Mheshimiwa Spika, lingine tuna mpango sasa wa kutengeneza mfumo wa kufunga au ku-*control* ajali kwa kutumia vidhibiti mwendo, ambapo tunahisi hivi vinaweza kupunguza ajali. Pia tuna mpango wa kufanya marekebisho ya sheria ambayo yanakwenda moja kwa moja kwenye masuala ya faini na adhabu katika mambo haya ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie pia

kuwaelimisha vijana kwa sababu naamini katika mkoa wake vijana wa bodaboda wapo, basi azidi kuwaelimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujibu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusu mafao ya Askari. Kwa kweli Wizara inajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunawalipa wastaafu posho zao mara tu baada ya wao kustaafu. Katika kipindi cha 2018/2019 tumejitahidi kati ya wastaafu 591; jumla ya wastaafu 479 tayari tulishawapatia mafao yao na sasa hivi wengi wanaishi maisha mazuri.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kinachokuwa kinatukabili kama sehemu ya changamoto, inafika wakati inakuwa OC nazo na bajeti nayo inakuwa mihani, kwa hiyo, ndiyo maana kuna wakati wanachelewa kidogo kulipwa. Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama itakuwa kuna mtu ambaye hajapata mafao yake na amestaafu, basi tukitoka hapa tuonane, tuone tunamsaidia vipi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Salome Makamba, nilikuona.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la msingi la ajali za barabarani kwa bodaboda na vyombo vingine vya usafiri. Tatizo hili ni Kitengo cha Usalama Barabarani kugeuza kitengo hiki kama chanzo cha mapato. Watu wanakwepa matrafiki, wanakimbia kwa sababu ukikamatwa hakuna onyo, ni faini. Bodaboda siku hizi wanakamatwa kwa kukimbizana na trafiki. Nadhani hii inasababishwa na uzee wa sheria hii ni ya mwaka 1973. Ni lini Serikali italeti mabadiliko ya Sheria ya Usalama Barabarani ili tufungue mjadala wa namna gani tutaiboresha ili kupunguza ajali za barabarani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ni swali fupi tu la lini mnaleta sheria? Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDAINI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Salome, Muswada huu uko njiani, muda wowote tutaleta tuje tujadili tuone namna ambavyo tunaweza tukafanya mabadiliko ya baadhi ya sheria hizi. Mheshimiwa asiwe na wasiwasi, tuko mbioni kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mnauliza lini, uko njiani, sasa mnataka nini? *(Kicheko)*

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali litaulizwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray. Aah, bado kuna swali la Wizara hiyo hiyo. Loh! Ni la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela. Samahani Mheshimiwa Deus.

Na. 66

Shamba Lililokuwa Limechukuliwa na Jeshi la Magereza Mollo

MHE. DEUS C. SANGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya kukabidhi kwa wananchi wa Vijiji vya Msanda, Muungano, Songambe na Sikaungu shamba lililokuwa limechukuliwa na Jeshi la Magereza Mollo Sumbawanga lenye ukubwa wa ekari 495?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko na wewe Mheshimiwa Naibu Waziri. Mwenzako Mheshimiwa Mary alikuwa na maswali manne, wewe una matatu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza na wananchi wa vijiji vilivyotajwa walikuwa na mgogoro siku za nyuma ambapo mgogoro huo ulimalizwa mwaka 2019 kwa Serikali kutoa eneo la ekari 1,800 kwa lengo la kumaliza mgogoro kama ilivyohitajika.

Mheshimiwa Spika, hitaji la ekari 495 ni dai jipya ambalo Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza na Ofisi ya Mkoa wa Rukwa, tunaendelea kulifanyia kazi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Deus nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba dai la ekari 495 ni jipya, bali ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani mbele ya Mheshimiwa Rais wakati huo alipofanya ziara Mkoa wa Rukwa kwamba watawakabidhi wananchi ekari 495. Liliokuwa linasubiriwa ni kukabidhi kwa maandishi kwa sababu Jeshi la Magereza limekuwa likisema kwamba hatuwezi kufanyia kazi matamko ya wanasiasa mpaka tupewe barua kutoka Wizarani. Ni lini Wizara itawapa barua Jeshi la Magereza ili kukabidhi hizo ekari 495 kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tamko hili limepelekea Askari Magereza sasa kuingia kwenye mgogoro mkubwa na wananchi na kuwanyanyasa kwa kuwapiga na mara ya mwisho juzi tu hapa nilikuwa huko Jimboni, mama mmoja (na nikipurushia *clip* utaona) amepigwa na kugaragazwa kwenye matope. Je, Wizara iko tayari kuunda

Tume itakayokuja kuchunguza unyanyasaji unaofanywa na hawa Askari Magereza na watakaobainika kunyanyasa wananchi hatua kali za kisheria zichukuliwe iwe fundisho kwa wengine? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tufike wakati tukiri kwamba kuna baadhi ya maeneo bado yana mivutano baina ya wananchi na Kambi za Magereza. Swali kwamba ni lini tutatoa hilo eneo, suala la utoaji wa eneo linahitaji taratibu, siyo suala la kusema tunakwenda na kutoa.

Mheshimiwa Spika, lingine amesema watu wananyanyaswa, wanapigwa, kitu ambacho tunakifanya kupitia Wizara, kwanza tutachunguza, tukiona kwamba kuna Maafisa wetu wa Magereza ambao wanahusika na unyanyasaji huo, hatua kali tutazichukua kupitia Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa kwa sababu ya muda, tuendelee na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray. Mheshimiwa karibu uulize swali lako.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

Na. 67

Bajeti ya Kuboresha Elimu ya Veta – Manyara

MHE. REGINA N. QWARAY aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza bajeti ya kuboresha elimu katika Vyuo vya Ufundi (*VETA*) Mkoani Manyara ili kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi?

SPIKA: Tuko Elimu sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Mbunge wa Mafia, majibu ya swali hilo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza wigo wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza mipango mbalimbali ya kuboresha utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi nchini. Mkoa wa Manyara ni moja kati ya mikoa inayonufaika na ongezeko hilo la bajeti. Katika kipindi cha mwaka 2018 – 2020, Serikali imetumia kiasi cha shilingi 1,925,438,420.13; kati ya fedha hizo shilingi 600,000,000 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na shilingi 505,159,420.00 zimetumika kununua nyumba za watumishi katika chuo cha *VETA* Manyara kutoka Shirika la Nyumba la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Chuo cha *VETA* Gorowa, kiasi cha shilingi 337,081,677.13 kimetumika kwa ajili ya ujenzi wa karakana, ofisi ya utawala na madarasa. Vilevile, katika Chuo cha *VETA* Simanjiro Serikali imetumia kiasi cha shilingi 223,981,323.00 kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kujenga bweni la wasichana. Aidha, shilingi 259,279,000.00 zimetumika kugharamia mafunzo ya muda mfupi katika Vyuo vya *VETA* Manyara na Gorowa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya kuboresha utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi katika mkoa wa Manyara na mikoa mingine kwa ujumla kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali, uliza swali la nyongeza.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna uhitaji mkubwa wa elimu ya mafunzo ya ufundistadi hapa nchini ni nini *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha inaongeza msukumo wa pekee ili vijana wengi wa kike na wa kiume kupata elimu hiyo hususan katika Mkoa wetu wa Manyara? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Kipanga, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Manyara peke yake *VETA* ina vyuo vifuatavyo: tuna Chuo hiki cha Mkoa cha Manyara, tuna Chuo cha Ufundi Simanjiro, vile vile tuna Chuo cha Ufundi Babati kilichopo Babati Vijijini ambacho kinaitwa Gorowa. Vile vile tunafanya upanuzi katika Chuo cha Wananchi cha Tango ambacho baada ya upanuzi huo zaidi ya wanafunzi 228 wanaweza wakapata udahili. Katika vyuo hivi vyote nilivyovitaja ambavyo viko katika Mkoa wa Manyara jumla ya wanafunzi 1,000 ambao wanaweza kuchukua kozi za muda mrefu na muda mfupi wanaweza wakapatiwa mafunzo katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali vile vile kupitia bajeti yake ya mwaka 2019/2020, imepeleka fedha jumla ya shilingi bilioni 48.6 kwa ajili ya kujenga vyuo mbalimbali vya *VETA* nchini kwa lengo la kuhakikisha kwamba elimu hii ya ufundi inawafikia wananchi wengi na vijana wengi kwa lengo la kupeleka Serikali au nchi yetu katika uchumi wa kati. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa, uliza swali lako la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga chuo cha *VETA* katika Kata ya Chamazi eneo ambalo limetolewa bure na *UVIKYUTA* zaidi ya ekari 30 ili kuwawezesha vijana wengi wa Kitanzania kuweza kujijiri na kuweza kupata ajira katika fani mbalimbali?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Kipanga, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Serikali ina mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba katika kila mkoa na katika kila wilaya tunakuwa na Chuo cha *VETA*. Katika awamu ya kwanza tumefanya ujenzi ambao mpaka hivi ssa unaendelea katika wilaya 29, lakini katika awamu ijayo tunatarajia katika kila wilaya kupeleka vyuo hivyo. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kila wilaya tutafikia kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tunaenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka. Pole kwa msiba.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba swali langu namba 68 liweze kujibiwa.

Na. 68

Ujenzi wa Mradi Mkubwa wa Maji - Chunya

MHE. MASACHE N. KASAKA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Chunya Mjini na kata za jirani utanza kutekelezwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Engineer Maryprisca Wilfred Mahundi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Chunya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto inayoukabili Mji wa Chunya. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, hatua mbalimbali za muda mfupi na mrefu zimeendelea kuchukuliwa. Kwa upande wa muda mfupi, Serikali imejenga mradi wa uboreshaji huduma ya maji katika Mji Mdogo wa Chunya uliogharimu kiasi cha shilingi milioni 946.8. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa tanki la ukubwa wa mita za ujazo 500, ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilometa 10.49. Mradi umekamilika kwa asilimia mia moja mwaka 2019 na umesaidia kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 36 hadi 51.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hatua za muda mrefu, Serikali kupitia Wizara ya Maji ina mpango wa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kwa ajili ya wananchi wa Mji wa Chunya. Mradi huo utatekelezwa kupitia fedha za mkopo kiasi cha dola za Marekani milioni 500 kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* kwa ajili ya miji 28 Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa sasa mradi upo katika hatua ya manunuzi ya Wakandarasi wanaotarajiwa kuwepo eneo la mradi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi ifikapo Aprili, 2021 na ujenzi wa miradi unatarajiwa kuchukua miezi 24. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Kasaka, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia nashukuru Serikali kwa kuweza kutekeleza Mradi wa Maji kwa Mji wa Chunya uliogharimu zaidi ya milioni 900 lakini mradi huu mpaka sasa hivi haujaweza kuwanufaisha wananchi wa

Wilaya ya Chunya na hata kiwango cha upatikanaji wa maji bado kiko chini ya asilimia 30. Tatizo kubwa tukiuliza tunaambiwa mara umeme unakuwa ni mdogo, mara maji ni machache. Sasa Serikali itueleze, je, tatizo ni nini mpaka mradi huu uliotumia fedha nyingi za Serikali haujaweza kuwanufaisha watu wa Chunya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye mradi mkubwa wa maji wa bwawa la Matwiga *design* ya mwanzo ilikuwa inasema itanufaisha vijiji 16, lakini kwenye *review* ilivyokuja utekelezaji wake ni vijiji nane. Je, Serikali haioni haja sasa kuweza kurudisha hii *design* ya mwanzo kurudisha vijiji 16 ili wananchi wa Tarafa ya Kipendao waweze kunufaika na mradi huu wa maji? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Masache Kasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia na lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama na ya kutosheleza. Niseme tu msimamo wa Serikali ni kuona kwamba miradi iliyokamilika na matunda yale ya mwisho maji bombani yanapatikana. Kwa mradi huu wa Chunya Mjini nipende tu kusema kwamba Mheshimiwa Mbunge nilifika Chunya na tulitembea pamoja, mradi ule umekamilika tatizo ni hili la umeme ambalo linaendelea kushughulikiwa ili liweze ku-*support* ile *pump* maji yaweze kwenda ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa swali la Bwawa la Matwiga, niseme kwamba, katika miradi ambayo ilichukua muda mrefu kutekelezwa ni pamoja na huu, lakini kwa nia njema ya Serikali hii na mkakati mkubwa wa Wizara chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri mradi ule sasa hivi unatekelezwa vizuri na mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge tulifika pale tukiongozana na Mtendaji Mkuu wa *RUWASA* kwa maana

ya *Director General*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, yale maji ambayo tuliyaona pale kwa pamoja kwenye kile chanzo hayatatoa tu kwa vijiji vile nane, tayari kama Wizara tumekubaliana tutakuja kutoa maji katika vijiji vyote 16.

SPIKA: Kama kumbukumbu zangu ziko sawa, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa *DC* Chunya, kwa hiyo anajua mradi huo vizuri. Kwa hiyo Masache mambo mengine mnatafutana tu, mtakuwa mnazungumza mambo ya nyumbani. Mheshimiwa Mtemvu nilikuona.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mradi wa Maji Chunya unafanana na ule mradi wa *2F2B* pale Tegeta A, ujazo wa lita milioni sita. Je, Wizara inaweza ikatuambia ni lini mradi ule utakamilika ili uweze kusaidia wananchi wote wa Goba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ule mradi wa tanki Mshikamano kwa ajili ya wananchi wa Mpiji Magohe, Makabe yote na Msakuzi.

Je, ni lini pia mradi huo utakamilika ili wananchi wapate maji salama?

SPIKA: Swali sio lako, kwa hiyo unapaswa kuuliza swali moja tu, sasa chagua mojawapo katika hayo ya kwako.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Niweze kufahamu mradi unaotaka kujengwa mshikamano kwa ajili ya wananchi wa Mbezi, Makabe na Mpiji Magohe utakamilika lini?

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri. Majibu ya swali hilo la Mradi wa Mbezi, Makabe na kadhalika *Engineer Maryprisca Wilfred Mahundi*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Mtemvu kutoka Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara sasa hivi inapitia miradi hii yote ambayo usanifu wake ulikamilika. Kwa hiyo nipende tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge huo mradi upo katika miradi ambayo inakwenda kutekelezwa awamu hii kabla mwaka huu wa fedha haujaisha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mkitazama saa yetu pale, bado tuna dakika 20 tu tumalize hii *portion*. Swali la Mheshimiwa Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi.

Na. 69

Ukamilishaji wa Mradi wa Maji - Nyashimo

MHE. NOAH L. S. MOLLEL aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa maji kwenye Vijiji vya Engutukoiti, Losineni, Juu, Losineni kati, Oldonyawasi, Lemanda, Lemengrass, Oldonyosambu, Likurat, Olkeejulbendet, Lenigjape, Olkokula, Lemanyati, Lenjani, Seuri, Ekenywa na Ngaramtoni na Kata za Kimyak, Sambasha Tarakwa, Oloirien, Kiranyi, Likidingla, Sokon II, Olturito, Bangata, Mlanganini, Nduruma, Bwawani, Oljoro na Lahni Musa, Kisango, Mwandet Wilayani Arumeru?

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Lemburis haya ndiyo yale maswali marefu, ingawa ni fupi lakini refu sana. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli vijiji hivi vilikuwa na changamoto ya huduma ya maji, lakini kuanzia mwezi Disemba, 2020, Vijiji vya Lengijave, Olkokola, Seuri, Ekenywa

na Ngaramtoni vimeanza kupata huduma ya maji kutoka kwenye mradi uliofadhiliwa na Shirika la Uingereza la *DFID* kupitia Shirika la *Water Aid Tanzania*. Aidha, Vijiji vingine vya Oldonyosambu, Oldonyowasi, Lemanda, Losinani Kati na Juu na Ilkuroti vinatarajiwa kupata huduma ya maji kutoka kwenye mradi huu kupitia upanuzi unaofanywa na Mamlaka ya Majisafi na Mazingira Jiji la Arusha kutoka kwenye tanki la maji lililopo kijiji cha Lengijave, lenye ukubwa wa mita za ujazo 450. Kijiji cha Lemanyata kina huduma ya maji kupitia Mradi wa Olkokola – Mwandeti.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.13 kwa Wilaya ya Arumeru kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na ukarabati wa Mradi wa Maji wa zamani wa Nduruma – Mlangarini na kukarabati Mtandao wa Bomba unaopeleka maji Vijiji vya Themu ya Simba, Kigongoni na Samaria na ukarabati wa Mradi wa Manyire – Maurani – Majimoto utakaonufaisha Vijiji vya Maurani, Manyire na Maji moto kuwa na maji ya uhakika na Miradi ya Likamba na Oloitushura & Nengungu.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri inatosha. Mbunge mwenyewe hakutaka swali lake lijibiwe vizuri. Huwezi kuuliza vijiji vyote hivyo vikajibiwa kwa dakika mbili *unless, you have to focus somewhere*.

Mheshimiwa, kama una swali la nyongeza.

MHE. NOAH L. S. MOLLE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali ina nia njema ya kutoa huduma ya maji, kulikuwa na miradi ya mwaka 2009 miradi ya Likamba, Musa, Nengu, Olotushura na Loskito, je, ni lini sasa Serikali itakamilisha miradi hiyo ya muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Maji katika kukarabati Mradi wa Ilmuro inayohudumia Kata za Oljoro na

Laroy. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Lemburis Saputu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mradi huu ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2009, nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge miradi hii tunakuja kutekeleza na nimeshafika eneo lake. Nimwahidi namna ambavyo tuliongea pale *site* tutakuja kufanyia kazi haraka iwezekanavyo na pamoja na hii ahadi ya Mheshimiwa Waziri aliyepita, ukarabati wa Mradi huo wa Ilmuro pia unakuja kufanyiwa kazi hivi karibuni. Fedha tayari zipo na mgao unaofuata na mgao unaofuata na Mheshimiwa Mbunge upo na atakwenda kutekelezewa mradi huo.

SPIKA: Bado tuko Wizara hii hii. Swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega.

Na. 70

Ukamilishaji wa Mradi wa Maji – Nyashimo

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Nyashimo, Kata ya Nyashimo ambao ulitegemewa kukamilika mwezi Oktoba, 2020 utakamilika ili wananchi waweze kupata maji safi na salama?

SPIKA: Bado tuko Wizara ya Maji, Mheshimiwa Naibu Waziri Maryprisca, majibu ya swali namba 70, tafadhali na leo una maswali matatu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Nyashimo ulianza kutekelezwa mwezi Julai, 2019 na ulitegemewa kukamilika tarehe Oktoba, 2020 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.58. Wakati utekelezaji wa mradi, Mkandarasi alipata changamoto zilizosababisha kuomba kuongezewa muda na hivyo mradi huu unatekelezwa kufikia mwaka huu 4 Aprili, 2021 ambapo ombi lake lillikubaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa utekelezaji wa mradi huo upo katika hatua ya majaribio ya kusukuma maji kupeleka kwenye tanki baada ya kufanikiwa kufunga umeme tarehe 9 Januari, 2021. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2021 na kuhudumia wakazi wapatao 12,000. (*Makofi*)

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Lusengekile.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali na niipongeze Serikali kwa namna inavyochukua hatua juu ya mradi ule. Pamoja na hayo mradi ule katika Kijiji cha Mwagulanja umeacha sehemu kubwa sana ya wananchi wa Isuka takriban kilometa nne kufikia *point* ambapo maji yamewekwa.

SPIKA: Mheshimiwa swali lako ni Nyashimo...

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, ni Kata ya Nyashimo sasa hicho Kijiji nilichokisema. Naomba tu kuuliza Serikali nini mpango sasa wa kufanya *extension* kutoka kwenye ule mradi kwenda kwenye Kijiji cha Mwagulanje kule Isuka ili wananchi wa kule nao waweze kupata maji? Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Hivi Nyashimo pale si mnachota pale pale ziwani tu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Simon Lusengekile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huu mradi unaendelea kutekelezwa. *Extension* ni kazi ambayo hata yule Meneja aliyeko pale anaweza kufanya, kwa hiyo nimwaminishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kufika mwezi Machi, tutaanza kuzitekeleza *extension*, lakini kwa kutumia wataalam wetu ambao wako kule.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa, uliza swali la nyongeza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kyerwa kuna changamoto kubwa ya maji na hasa Kata za Kibale, Bugomora na Mrongo ila ninavyoongea hapa Kijiji cha Mgorogoro kuna tanki kubwa la maji ambalo tangu limewekwa...

SPIKA: Ni wapi huko unakokuulizia?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, Kata ya Kibale.

SPIKA: Kata hiyo iko kwenye Wilaya gani?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kyerwa, Jimbo la Kyerwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tanki limewekwa kama urembo halijawahi kutoa maji. Kila siku wananchi wakiona habari za maji wananitumia *message* na sasa wamenikumbusha. Ni lini lile tanki katika Kijiji cha Mgorogoro litaanza kutoa maji? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui swali hili la Kyerwa kama una majibu. Hebu jaribu ukishindwa basi Waziri yupo. Mheshimiwa Naibu Waziri, tanki la Kyerwa kule. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia kuhusu tenki kubwa lililokamilika lakini halitoi maji. Mkakati wa Wizara ni kuona kwamba miradi hii ambayo miundombinu imekamilika kufikia mwezi wa tatu kwenye Wiki ya Maji tunataka kuona kwamba maji yanatoka.

Mheshimiwa Spika, nimuahidi Mheshimiwa Anatropia kwamba nitafika huko Kyerwa na kuona nini kinasababisha maji hayatoki. Lengo ni kuona kwamba maji yanapatikana bombani. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tutoke maji sasa Waheshimiwa twende Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa swali la Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Nachingwea.

Na. 71

Ujenzi wa Barabara ya Masasi – Nachingwea

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea kwa kiwango cha lami utaanza?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi Uchukuzi, Eng. Geoffrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa barabara ya Masasi – Nachingwea inayounganisha makao makuu ya wilaya ya Masasi na Nachingwea, imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tangu mwaka 2015. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta

fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, barabara yenye urefu wa kilometa 45. Katika mwaka wa fedha huu 2020/2021, jumla ya shilingi bilioni 1.43 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha za ujenzi pia imeendelea kutenga fedha za matengenezo mbalimbali kwa barabara hii ambapo katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, jumla ya shilingi milioni 232.66 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili barabara hii iendelee kupitika katika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Kwa kweli barabara hii inahitaji lami jamani, Masasi – Nachingwea. Mheshimiwa Chinguile, swali la nyongeza.

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali yetu yenye kutia matumaini lakini bado kwa umuhimu wa barabara hii wananchi wa Jimbo la Nachingwea watapenda kusikia *commitment* ya Serikali. Kwa kweli, katika hili viongozi wengi wanahukumiwa kutokana na barabara hizi pamoja na mambo mengine. Je, nini *commitment* ya Serikali juu ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, viko vijiji vya Ikungu, Chiola kuelekea Ruangwa, hapa tayari walifanyiwa tathmini na wenzetu wa *TANROADS*. Watu wa *TANROADS* walikuja wakafanya tathmini wakiamini kwamba barabara itapita upande wa kulia baada ya muda wakarudi tena wakafanya tathmini upande wa kushoto. Kwa hiyo, hawa wananchi wamezuliwa kwenye maeneo yale wasifanye maendelezo. Ni lini Serikali itakwenda kutoa ufafanuzi wa jambo hili, ili wananchi wa maeneo yale waweze kuendelea na shughuli zao? Ahsante sana.

SPIKA: Hiyo ni kwa barabara ya Nachingwea – Ruangwa?

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Eng. Msongwe.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Chinguire, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *commitment* ya Serikali ni kwamba tayari fedha ya awali za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami zimeshatengwa. Pia barabara hii imeahidiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na pia ni kati ya barabara ambayo Mheshimiwa Rais ameahidi kujenga kwa kiwango cha lami katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ambalo ameuliza kwamba kuna wananchi ambao wameshindwa kuendeleza maeneo yao kwa sababu ya watu wa *TANROADS* waliokwenda kupima, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea kwamba suala hili linaendelea kufanyiwa kazi. Naomba kama kuna changamoto yoyote tofauti ambayo pengine mimi nitakuwa siifahamu basi tuwasiliane naye ili niweze kujua changamoto halisi ni ipi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka nilikuona, barabara ya kwenda Liwale.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sambamba na barabara ya Masasi – Nachingwea, barabara hii vilevile ina jina la Lukuledi – Liwale yenye jumla ya kilometa 175 kwa maana kutoka Masasi mpaka Liwale kilometa 175. Barabara hii tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Wanaliwale wanataka kusikia barabara Nachingwea – Liwale lini itajengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

SPIKA: Na hasa pale Lukuledi pale, hata ukimwaga ndoo ya maji tu gari linakwama. (*Kicheko*)

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara hii inatoka Masasi – Lukuledi – Nachingwea – Liwale.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja kama nilivyosema tunatambua ni muhimu na zimeahidiwa kujengwa katika bajeti ambayo tutaanza kuijadili. Kwanza ni barabara ambayo ipo kwenye Mpango wa Miaka Mitano na tunategemea katika bajeti inayoanza itatengewa fedha ili ianze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa ili tumalize *on time*, linaulizwa na Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa.

Na. 72

Ujenzi wa Barabara ya Njia Panda ya Kongwa – Mpwapwa

MHE. GEORGE N. MALIMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kuanzia Njia Panda ya Kongwa hadi Mpwapwa Mjini yenye urefu wa takribani kilometa 30 ambayo ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025?

SPIKA: Majibu ya swali hili la miaka mingi sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi. Ukijibu hilo ujue Mheshimiwa Simbachawene anakusikiliza kwa hamu sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Njia Panda ya Kongwa hadi Mpwapwa ulianza kutekelezwa kwa kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014. Ujenzi huu ulianza baada ya kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2013 uliohusisha barabara ya Mbande – Kongwa *Junction*. Kongwa *Junction* – Ugogoni kilometa 17.5, Kongwa *Junction* – Mpwapwa – Ving’awe kilometa 38.85 na Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe kilometa 46.93.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ujenzi kwa kiwango cha lami ulianza, ambapo hadi sasa ujenzi wa sehemu ya Barabara ya Mbande – Kongwa *Junction* kilometa 16.7 umekamilika. Serikali kwa sasa inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njia Panda ya Kongwa hadi Mpwapwa. Katika mwaka wa fedha huu tunaendelea nao Serikali imetenga shilingi bilioni 4.95 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami katika mji wa Mpwapwa. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njiapanda ya Kongwa hadi Mpwapwa utaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kutenga fedha za matengenezo mbalimbali ya barabara hizi ili ziendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi bilioni 1.1 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Pandambili – Saguta – Mpwapwa – Ng’ambi na shilingi milioni 751.596 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Manchali – Ng’ambi – Kongwa *Junction* – Hogolo *Junction* ambapo barabara ya Njiapanda ya Kongwa hadi Mpwapwa imezingatiwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Malima ameridhika. Swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa. *(Kicheko)*

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni adhama ya Serikali kuunganisha miji yote ya mikoa na wilaya kwa barabara za lami; na kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii kiuchumi kwa wananchi wa Mpwapwa, je, Serikali ipo tayari kuipa kipaumbele maalum barabara hii ili ikamilike mapema?

SPIKA: Kwenye majibu Mheshimiwa Naibu Waziri barabara hii haijatengewa hela za kuwekewa lami. Ni kilometa 4 tu za pale Mpwapwa Mjini, lakini Kongwa – Mpwapwa haina chochote. Anachouliza Mheshimiwa kwenye bajeti inayokuja mtaikumbuka kidogo barabara hii ya Kongwa – Mpwapwa? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu na ndiyo maana hata hapa tunapoongea yeye atakuwa ni shahidi kwamba mkandarasi yuko *site* akiwa anajenga hizo kilometa 5. Naamini katika bajeti ijayo tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza hiyo barabara.

SPIKA: Mheshimiwa George Simbachawene unauliza swali la nyongeza? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, muda hauruhusu. Mheshimiwa Simbachawene anatamani angekuwa Mbunge wa kawaida kwa leo lazima angesimama hapa kwenye hii barabara.

Waheshimiwa Wabunge, wageni tuliona asubuhi ya leo ni wageni 48 wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni Umoja wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Nchini wanaotoka Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Erasto Rock. Wasomi wa Mbeya simameni pale mlipo; eeh, karibubi sana mjengoni. Mwenyeji wenu Mheshimiwa Naibu Spika mmemuona anapokaa? Inawezekana hamjamuona? Hebu Naibu wakuone au ametoka kidogo? Ametoka kidogo, basi karibuni sana Waheshimiwa, karibuni mjengoni. *(Makofi)*

Wageni 52 wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni Diwani, Wachungaji na Kwaya ya Vijana wa Kanisa la KKKT Ilula wakiongozwa na Mheshimiwa Yohanes Muhanga, Diwani wa Kata ya Nyalumbu, lakini hawa niwatambua mwishoni. Wale wageni wote wa 52 wa Mheshimiwa Nyamoga msimame. Karibuni sana. Wanakwaya wa KKKT Ilula wako wapi? Ooh, hongereni sana, mnaweza mka-tune kidogo? Baadaye kidogo hapo nje. *(Kicheko)*

Naomba tuwatambue Diwani wa Kata ya Nyalumbu Yohanes Muhanga. Karibu sana Diwani. Pia Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Kilolo, Kefa John Walesi, karibu sana. Mchungaji General Kivamba wa Usharika wa Ilula, karibu sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jackson Nkulikwa. *UDOM*, wageni wa Mheshimiwa Hasunga, karibuni sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Fakharia Shomar, ni mtoto wake Ndugu Omar Daudi Khamis. Yuko wapi Omar? Ahsante sana, karibu sana. Huyu ni mtoto wa Mheshimiwa Fakharia ametoka kule Uingereza, karibu sana Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambao wamekuja kushuhudia uapisho wake, wakiongozwa na mume wake Ndugu Edwin Kileo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Flatey Massay ambao ni Madiwani kutoka Mbulu, Mkoa wa Manyara, wakiongozwa na Mheshimiwa Elizabeth Bayo. Karibuni sana Waheshimiwa. *(Makofi)*

Wageni maalum kwa ajili ya mafunzo ni wanachuo 100 kutoka Chuo cha Mipango kutoka hapa Dodoma ambao wamekuja kujifunza. Mipango, ooh karibuni sana na mmekuja siku nzuri, mshinde hapa kutwa nzima ili msikilize Mpango wa Taifa na mjadala wa Wabunge kuchambua huo Mpango. Kwa vile nyie ni Wanamipango ni vizuri mkatumia muda mrefu leo asubuhi hata jioni ya leo kusikiliza masuala ya mipango ya nchi. *(Makofi)*

Wanachuo 40 kutoka Chuo cha Ufundi *High Score* kilichoko Jijini Dodoma. Karibuni sana wana ufundi, mmechagua njia iliyo njema kusomea masuala ya ufundi, hongereni sana. Naona watoto wa kike nao ni wengi katika kujifunza mambo ya ufundi. Hongereni sana. *(Makofi)*

Nimemaliza kwa upande huo, sasa Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa
kwa Miaka Mitano, yani 2021/2022 mpaka 2025/2026 na
Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa
Mwaka 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya
Muongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti
ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022**

SPIKA: Ahsante. Anachotuongoza Katibu ni kwamba sasa Bunge lipokee, ili baada ya kupokea mjadili na kushauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026, wa miaka mitano na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022. Kwa hiyo, kuna wa miaka mitano na wa mwaka mmoja, ikiwa ni pamoja na

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

Baada ya Mheshimiwa Waziri kuwasilisha kutakuwa na mjadala kama kawaida. Tunaanza na dakika kumi – kumi na tutaendelea mpaka Ijumaa. Kwa wale wenzangu mimi mnaotaka kuja mwishoni mtaambulia dakika tatu – tatu kule mwisho kama kawaida yetu. Wale wanaotaka kuanza kwa dakika kumi – kumi tuanze leo.

Moja kwa moja sasa nimuite Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchemba ili aweze kutuwasilishia hoja hiyo ya Serikali. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu lipokee, kujadili na kuidhinisha mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2020/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kuendelea kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha leo hii kukutana kwa ajili ya kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kulijalia Taifa letu amani, utulivu, umoja na mshikamano na kutuwezesha kukamilisha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge wote, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Mheshimiwa Martha Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM. Tunamwomba kwa Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake kwa amani. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa napenda kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa tena kwa ushindi wa kishindo kuwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kuteuliwa kushika nafasi muhimu katika uongozi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe pia kuchaguliwa na ushindi wa kishindo kwa 99.7% kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Mbili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inaashia kuwa Waheshimiwa Wabunge wana imani kubwa na utendaji wako katika kuliongoza Bunge hili Tukufu. Aidha, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuishukuru kamati ya kudumu ya Bunge ya bajeti chini ya uenyekiti wake Sillo Daniel Baran Mbunge wa Babati vijijini na Makamu mwenyekiti Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi CCM kwa muongozo wao na maoni waliotupatia kuboresha mapendekezo ya mpango huu ushauri wao umezingatiwa kikamilifu katika taarifa ya mpango ninayoiwasilisha Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022, 2025/2026 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika kipindi cha mwaka 2025, hotuba za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja na la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania Novemba, 2015 na 2020 mtawalia; Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (2011/2012 - 2025/2026), Matokeo ya Tathmini Huru ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 hadi 2020/2021, Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, matokeo ya tafiti zilizofanywa na vyuo na taasisi mbalimbali hapa nchini, Dira ya Afrika Mashariki ya mwaka 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu Mwaka 2030 na Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Mheshimiwa Spika, dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango huu utakuwa na maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara, kuchochea maendeleo ya watu, kuendeleza rasilimali watu. Aidha, jumla ya shilingi trilioni 114.8 zinahitajika kugharamia miradi na program zitakazotekelezwa katika mpango huu kwa kipindi cha muda wa miaka mitano. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 74.2 ni mchango wa sekta ya umma na shilingi trilioni 40.6 ni mchango wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, viashiria vya ujumla vya uchumi jumla tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 na 2020/2021) ilifanywa na tathmini huru ya taasisi za kitafiti za kiuchumi na kijamii (*ESRF*) inaonesha kuwa katika kipindi cha miaka minne utekelezaji wa mpango wa miaka mitano kwa upande wa pato la Taifa ilikuwa na wastani wa 6.9%, mfumuko wa bei ulikuwa na wastani wa 4.1% kwa mwaka, ikiwa ni ndani ya lengo la kutokuzidi 5%, akiba ya fedha za kigeni ilitosheleza uagizaji wa bidhaa wa huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9, ikiwa ni ndani ya lengo la miezi minne na nakisi ya bajeti ilikuwa ndani ya lengo la kutokuzidi 3% kwa kipindi chote. Katika kipindi hicho deni la Serikali lilikuwa himilivu katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, vile vile pato la wastani la kila Mtanzania liliongezeka kutoka shilingi 2,225,099 sawa na dola za Kimarekani 1,022 kwa mwaka 2016 hadi shilingi 2,577,967 sawa na dola za kimarekani 1,080 kwa mwaka 2019. Kielelezo kikuu cha mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa ni Tanzania kufanikiwa kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati kwa mwezi Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 hadi 2020/2021) ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 107 ambapo shilingi trilioni 59 ni kutoka sekta ya umma na trilioni 48 kutoka sekta binafsi. Katika miaka minne ya utekelezaji wa mpango huo sekta ya umma imetumia jumla ya shilingi trilioni 34.9 sawa na 76.5% ya lengo la miaka minne la kutumia shilingi trilioni 45. Aidha, sekta binafsi imetumia jumla ya trilioni 32.6%, sawa na 85% ya lengo la miaka minne ya kutumia shilingi trilioni 38.4%.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa ujenzi wa uchumi wa viwanda utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umejikita katika kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini hususani malighafi za kilimo, madini na gesi asilia. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uzalishaji viwandani mafanikio ni kujengwa kwa jumla ya viwanda 8,477 kati ya mwaka 2015 hadi 2019 ambapo viwanda vikubwa ni 201, vya kati ni 460, vidogo 3,406 na vidogo sana ni 4,410. Ujenzi wa viwanda umeongeza idadi ya viwanda hapa nchini kutoka 52,633 mwaka 2015 hadi viwanda 61,110 mwaka 2019. Viwanda hivyo vimechangia ongezeko la uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa soko la ndani na la nje ikijumuisha bidhaa za ngozi, ujenzi (nondo, mabati, saruji, misumari na rangi) *plastic*, zana za kilimo, vinywaji na marumaru. Baadhi ya viwanda vilivyojengwa ni kiwanda kipya cha bidhaa za

ngozi *Kilimanjaro International Lather Industries* na kuanza maandalizi ya awamu ya pili ya Kiwanda cha Nguru kilichopo Mvomevo Morogoro kwa ajili ya kuchakata nyama. Kiwanda cha *Pipe Industries Limited* kinachozalisha mabomba kilichopo Vingunguti Dar es Salaam, Majengo ya viwanda kwa ajili ya wajasiriamali katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Geita, Mtwara, Ruvuma pamoja na Kiwanda cha Chai cha Kabambe.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingine ni Kiwanda cha *Yalin Cashewnut Company* kinachobangua korosho kilichopo Mikindani Mtwara, Viwanda vya *Goodwill Tanzania Limited Ceramic* na *KEDA Ceramic Companies* vilivyoko Mkoa wa Pwani vinavyozalisha marumaru, Kiwanda cha *Plasco Pipe Lines* kilichoko Dar es Salaam kinachozalisha bidhaa za *plastic*, Kiwanda cha *African Dragon Enterprises* kinachozalisha mabati, jengo la Kiwanda kipya cha Kuunganisha Matrekta *TAMCO* kilichoko Kibaha, Kiwanda cha Kuchakata Mazao katika Mkoa wa Dodoma na kuanza kwa ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huo umeleta mafanikio yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa kutoka asilimia 7.9% mwaka 2015 hadi 8.5% kwa mwaka 2019; Kukuua kwa sekta ya uzalishaji viwandani kwa wastani wa asilimia 8.3 kwa mwaka ambapo kumechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani ikijumuisha saruji, marumaru, nondo na bati; Kuzalishwa kwa fursa za ajira kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi ajira 482,601 kwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la 47.2%; na Kuchangia katika mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka 13.8% mwaka 2016/2017 hadi 14.2% kwa mwaka 2019/2020. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kiasi cha shilingi bilioni 45.3 kimetumika kuboresha na kuendeleza miradi ya uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo; Kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji ambayo imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 kwa mwaka 2015 hadi hekta 694,715 kwa mwaka 2020. Kuendelea kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu za Kigugu ambayo iko Morogoro zenye hekta 200 ambapo utekelezaji umefikia 98%; Mvumi Kilosa yenye hekta 249 ambayo imefikia 100%; Msolwa Ujamaa Morogoro yenye hekta 675 ambayo imefikia 98%; Njange Kilombero yenye hekta 325 ambayo imeshakamilika kwa 100%; Shamba la Mbegu Kilangani Kilosa lenye hekta 400 ambayo limeshafikia 80%; na kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 71,000 kwa mwaka 2020; Kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa mbegu za kilimo Morogoro; Kuzalishwa kwa kilo 14,700 za mbegu za mpunga za daraja la awali aina ya *TXD 306*, *TXD 88*, *Komboka*, *Super* na *Nerika 1*; Kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,450 mwaka 2015 hadi tani 727,719 kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, mengine ni; Kukamilika kwa ujenzi wa maghala matano ya kuhifadhia mpunga kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga; Kusambazwa kwa tani 40,592.6 za *sulphur* na lita 1,314,465 za viuatilifu maji kwa wakulima wa korosho; Kuendeshwa kwa minada minane ya kahawa katika Mkoa wa Kilimanjaro miwili, Songwe minne, Ruvuma miwili; na kukaguliwa kwa viwanda 24 na maghala 30 na kutolewa leseni za kuendesha biashara ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, htua hizi zimechangia kupatikana kwa mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula kufikia 118%, pamoja na kuongezeka utoshelevu kwa mwaka 2019/2020; Kupungua kwa mfumuko wa bei za chakula kufikia wastani wa 5% kwa mwaka 2020 na kupungua kwa umaskini wa chakula kutoka 9.7% mwaka 2011/2012 hadi 8.0% mwaka 2017/2018. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kiasi cha shilingi bilioni 188.9 kimetumika kuboresha na kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo mafanikio yamekuwa ni pamoja na: Kujenga kiwanda kipya cha Kilimanjaro *International Lather Industries* chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka na kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka; Kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha *NAIC* kilichopo Usa River Arusha kwa kununua kifaa kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha *nitrogen*; Kujengwa kwa Viwanda vipya vya kimkakati vya Nyama vya *TANCHOICE* kilichoko Pwani, Elia *food Oversees Limited* kilichoko Arusha na *Binjan Company Limited* cha Shinyanga; Kujengwa kwa Kiwanda cha Maziwa cha *Galaxy Food Beverages Company Limited* kilichoko Arusha; Kujengwa kwa Kiwanda cha Kuzalisha Chanjo cha *Hester Bioscience Africa Limited* kilichoko Pwani chenye uwezo wa kuzalisha chanjo aina 37 na kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji huu umewezesha mafanikio yafuatayo: Kuongezeka kwa viwanda vya kusindika nyama nchini kutoka 25 mwaka 2015/2016 hadi viwanda 32 mwaka 2019/2020 na viwanda vya kusindika maziwa kutoka 82 kwa mwaka 2015/2016 hadi 99 kwa mwaka 2019/2020; Kuongezeka kwa usambazaji wa mitamba katika mashamba ya Serikali kutoka mitamba 11,449 kwa mwaka 2015/2016 hadi mitamba 18,255 kwa mwaka 2019/2020; Kuongezeka idadi ya majosho ya kuogeshea mifugo kutoka majosho 2,428 mwaka 2015/2016, hadi majosho 2,513 kwa mwaka 2019/2020; Kuongezeka kwa maeneo ya malisho ya mifugo kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015/2016 hadi hekta milioni 2.85 mwaka 2019/2020; Kuendelea kukamilika kwa ujenzi wa machinjio ya kisasa iliyoko Vingunguti; kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na zao la ngozi kutoka shilingi bilioni 1.73 kwa mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 9.1 kwa mwaka 2019/2020. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano shilingi bilioni 5.66 zimetumika kuboresha na kuendeleza sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi mafanikio ni: Kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani laki 362,645 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.48

kwa mwaka 2015/2016 hadi tani 497,567 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.34 kwa mwaka 2019/2020; Kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya sangara kutoka tani elfu 23.58 mwaka 2015/2016 hadi tani 27,596.27 mwaka 2019/2020; Kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/20 jumla ya kilo 777,750 za mabondo zilisafirishwa; Kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mauzo ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.25 kwa mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 506.24 kwa mwaka 2019/2020; na Kuendelea na maandalizi ya ujenzi ya bandari ya uvuvi Mbegani, na ununuzi wa meli nne za uvuvi. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano shilingi bilioni 33.5 zimetumika kuboresha na kuendeleza sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini: Kupitia na kutunga sheria sera na mikataba ya madini; Kuanzishwa kwa kampuni mpya ya *Twiga Minerals Corporation*, inayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania ambayo ina hisa ya 16% na kampuni ya *Barrick* ambayo ina hisa 84% ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; Kusainiwa kwa mkataba wa ubia wa kampuni ya *LZ Nickel* na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuendeleza na kuchimba madini ya *nicol* ambapo chini ya mkataba huo imeundwa kampuni ya ubia inayoitwa *Tembo Nickel Corporation Limited* kwa umiliki wa hisa 84 kwa kampuni ya *LZ Nickel* na Serikali ya Tanzania kwa 16%.

Mheshimiwa Spika, mengine ni kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 41 vya kuuzia madini; Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne na vituo 41 vya kuuzia madini vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; Kuimarishwa kwa ulinzi wa rasilimali za madini kwa kujenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24 wa Mererani Mkoani Manyara pamoja na kujenga *One Stop Center*, kufunga vifaa vya ulinzi ikiwa ni pamoja na *CCTV camera* kuzunguka ukuta wa barabara ya kuzunguka ukuta wa ndani; Kuimarisha taasisi zilizochini ya Wizara kwa kuzipatia vitendea kazi na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu vya mfano wa

uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Rwamgasa (Geita), Katente (Bukombe) na Itumbi (Chunya). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zimechangia sekta ya madini kukua kwa wastani wa asilimia 8.0 kati ya mwaka 2016 hadi 2019; mchango wa Sekta ya Madini katika pato la Taifa kufikia asilimia 5.2 kwa mwaka 2019/2020 kutoka asilimia 4.6 ya mwaka 2015/2016 na kuimirika kwa huduma kwa jamii zinazozunguka migodi. Aidha, mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,912 sawa na shilingi bilioni 4,464.71 kwa mwaka 2015/2016 hadi Dola za Kimarekani milioni 2,898.8 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 6,769.0 kwa mwaka 2019/2020 na maduhuli kutoka shilingi bilioni 196 kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia shilingi bilioni 528.3 kwa mwaka 2019/2020 na kukusanya shilingi bilioni 317 sawa na asilimia 120.6 ya lengo la shilingi bilioni 263.36 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, shilingi bilioni 82.2 zimetumika kuboresha na kuendeleza miradi ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maliasili na utalii: Kujengwa na kukarabatiwa viwanja vya ndege, kununuliwa kwa ndege, kuongezwa kwa safari za ndege ndani na nje ya nchi, kudhibiti ujangili, kuongeza idadi ya watalii na mapato kupitia miradi ya kujenga uwezo katika hifadhi za Taifa, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili na Mradi wa Kuendeleza Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania, kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Burigi ambapo jumla ya watalii 1,171 wameitembelea hifadhi kati yao 996 ni wa ndani na 175 ni wa nje, ambapo jumla ya shilingi milioni 492,741,622 zimekusanywa kuanzia Novemba, 2019 hadi Desemba, 2020.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa hifadhi ya Taifa ya Nyerere ambapo jumla ya watalii 9,938 kati yao 6,189 ni wa nje na 3,749 ni wa ndani wameitembelea hifadhi hii tangu Novemba, 2019 hadi Desemba, 2020 ambapo jumla ya shilingi za Kitanzania 1,552,712,660 zimekusanywa na kuendelea kutangazwa kwa

vivutio vya utalii katika nchi mbalimbali duniani ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana. Hatua hizi zimechangia kuongezaka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi watalii 1,527,230 kwa mwaka 2019. Aidha, wastani wa idadi ya siku zinazotumiwa na watalii kukaa nchini zimeongezeka kufikia siku 13 mwaka 2019 ikilinganishwa na iliyokuwa siku 10 kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotokana na utalii yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.9 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 4,436.7 mwaka 2015 hadi Dola za Kimarekani bilioni 2.6 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 6,071.3 kwa mwaka 2019. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha shilingi bilioni 269.7 kimetumika kuboresha na kuendeleza maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za afya, maji, elimu umeongeza kasi ya ufungamanishaji wa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kufangamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, kuendelea kutoa huduma za kupandikiza uloto yaani *bone marrow transplant* na kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Wodi Na.18 la Sewahaji pamoja na ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa binafsi katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili, kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la *X-ray* katika Hospitali ya Rufaa ya Dodoma. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa hospitali ya huru iliyopo hapa Dodoma, kununuliwa kwa mashine ya *digital X-ray* na *Ultra Sound* na vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea 960. Haya ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na ununuzi wa mashine ya *Positron Emmission Tomography* pamoja na *scan* kwa ajili ya Hospitali ya *Ocean Road*, kujenga na kuboresha miundombinu ikijumuisha jengo la

huduma za upasuaji la radiologia na jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje. Vilevile kujenga maabara na jengo la mama na mtoto katika Hospitali za Rufaa za Mara, Geita, Songwe, Katavi, Sekou Toure iliyoko Mwanza na Hospitali za Rufaa za Kanda ya Kusini yaani Mtwara na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaani Mbeya na Hospitali ya Kanda ya Kaskazini yaani *KCMC* na Hospitali ya Kanda ya Ziwa yaani Burigi Geita.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya ambayo imefikia hatua mbalimbali ikiwemo kufikia asilimia 98 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo la wagonjwa wa nje, kufikia asilimia 73 ya ujenzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Rufaa ya Njombe na ujenzi wa jengo la ghorofa moja la huduma za upasuaji la radiologia na maabara na kufikia asilimia 50 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya Rufaa ya Simiyu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na ununuzi wa dawa chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuongeza idadi ya zahanati kutoka 4,922 kwa mwaka 2015 hadi 6,120 kwa mwaka 2020 na vituo vya afya kutoka 535 kwa mwaka 2015 hadi kufikia vituo 710 kwa mwaka 2020. Pia hospitali za halmashauri na za wilaya kutoka 77 mwaka 2015 hadi 179 kwa mwaka 2020. Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 62 kwa mwaka 2015/2016 hadi miaka 66 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka wastani wa vifo 67 kwa vizazi hai 1000 kwa mwaka 2014/2015 hadi vifo 50.3 kwa mwaka 2019/2020, kupungua kwa vifo vya kinamama wajawazito wakati wa kujifungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2015/2016 hadi vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2019/2020. Pia kuongezeka kwa watoto waliozaliwa kwa kuhudumiwa na wahudumu wa afya wenye ujuzi kutoka asilimia 51 kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 80 kwa mwaka 2019/2020. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha

shilingi bilioni 736.67 zimetumika katika utekelezaji wa miradi ya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu mafanikio ni pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu katika shule 3,904 zikiwemo za msingi 3,021 na sekondari 883, mabweni 547, nyumba za walimu 101, majengo ya utawala 25 na maktaba 43. Pia kukamilika kwa ujenzi maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133, kuendelea kugharamia posho ya madaraka kwa walimu wakuu, fidia ya ada kwa wanafunzi, ruzuku na uendeshaji wa shule ambapo shilingi trilioni 1.2 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia elimu ya msingi bila ada.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kukarabatiwa shule kongwe 84 kati ya 89, kuboreshewa miundimbinu ya Vyuo ya 54 ya Maendeleo ya Wananchi, kutolewa kwa mikopo ya elimu ya juu ya jumla ya shilingi trilioni 2.26, kuanzishwa kwa vyuo vya umahiri vya mafunzo katika taasisi za elimu ya ufundi na kuimarishwa kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika taaluma za anga na Chuo cha Ufundi Arusha katika taaluma ya nishati na kukamilika na kuzinduliwa kwa maktaba ya kimataifa yenye uwezo kuhudumia wanafunzi 2,600 kwa wakati mmoja pamoja na hostel za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi hizi zimechangia kuongezeka kwa viwango vya uandikishaji wa wanafunzi wa elimu msingi kutoka asilimia 93.3 mwaka 2015 hadi asilimia 110 kwa mwaka 2020. Pia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojunga na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 196,091 kwa mwaka 2015/2016 waliojiunga na mafunzo hadi 320,143 kwa mwaka 2019/2020 na elimu ya ufundi kutoka 117,067 kwa mwaka 2015/2016 hadi 151,379 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojunga na vyuo vikuu hapa nchini kutoka 65,064 kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia wanafunzi 87,813 kwa mwaka 2019/2020 na kuongezeka kwa wanufaika kwa mikopo ya elimu juu kutoka wanafunzi 125,126

kwa mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 132,392 kwa mwaka 2020. Aidha, kiwango cha ufaulu wa mitihani ya darasa la saba kimeongezeka kutoka asilimia 67 ya mwaka 2015 hadi asilimia 81.5 kwa mwaka 2019 na sekondari yaani kidato cha nne kutoka asilimia 68 ya mwaka 2015 hadi asilimia 80.7 kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, aidha, wanafunzi waliohitimu elimu ya juu walifikia 60,940 kwa mwaka 2019/2020 na elimu ya mafunzo stadi 90,847 kwa mwaka 2018/2019 na elimu ya ufundi stadi 86,547 kwa mwaka 2019/2020. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kiasi cha shilingi trilioni 3.15 zimetumika kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji, kukamilika kwa miradi 1,423 ya maji iliyotekelezwa miji na vijijini ni moja ya mafanikio yaliyopatikana. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa miradi ya maji katika Miji ya Geita, Njombe na Songwe, kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika Mji wa Kigoma ambao umeshafika asilimia 90, utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Viktoria kwenda katika miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui, Nzega ambao imeshafikia asilimia 98. Aidha, kukamilika kwa asilimia 76 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza, kukamilika kwa asilimia 62 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Arusha, kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same, Mwanga, Korogwe ambapo utekelezaji wake umeshafikia asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika eneo la linalohudumiwa na DAWASA kwa maana ya Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na umehusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze, Kisarawe, Pugu hadi Ukonga, Mbezi Louise, Kiluvia, Tegeta, Wazo, Madale, Mvumoni, Mabwepande, Bagamoyo maeneo ya Vikawe, Zinga, Mapinga pamojana na Kilege.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla miradi yote iliyotekelezwa imewezesha wananchi zaidi ya milioni 25

kupata huduma ya maji ambapo wastani ya idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 74 ya mwaka 2015 hadi asilimia 84 kwa mwaka 2020. Kwa mijini kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri muda wako *almost* umekwisha lakini nakuongeza robo saa hadi tano nusu kamili pale, kwa hiyo, jitahidi kwenda kwa muhtasari zaidi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanzishwa Mahakama za Makosa ya Rushwa pamoja na Uhujumu Uchumi, ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi wa Taifa na kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama Kuu mbili katika Mikoa ya Mara na Kigoma na ukarabati wa Mahakama Kuu tatu katika Mikoa ya Mbeya, Tanga na Rukwa.

Vilevile kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi tano kwa Mikoa ya Pwani, Geita, Simiyu, Manyara, Njombe, kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama za Wilaya 15 katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkuranga na Wilaya zote kama ambavyo zimeorodheshwa. Hatua hizi zimechangia kuongeza kwa idadi ya kesi hizi za rushwa zilizotolewa uamuzi kutoka asilimia 10 kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 82 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazingira wezeshi kwa utekelezaji na uendeshaji kibiashara, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni kama ifuatavyo. Kwa upande wa nishati ya umeme; kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ambazo ni *megawatt* 2,015 ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 25.8. Kwa ujumla kiasi cha shilingi trilioni 1.85 kimetumika katika utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara, ujenzi wa barabara na madaraja makubwa, mafanikio yaliyopatikana ni kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu kilomita 3,537 yaani barabara kuu na barabara za mikoa kilomita 2,209 na barabara za halmashauri kilomita 1,328. Hii imefanya mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami hadi mwaka 2019/2020 kufikia kilomita 13,044 ambapo kilomita 10,939 ni barabara kuu na kilomita 2105 ni barabara za mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli, Serikali inaendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa yaani *Standard Gauge Railway (SGR)* ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro, kilomita 300 umeshafikia asilimia 90 na kipande cha Morogoro - Makutupora, kilomita 422 umeshafikia asilimia 49.2.

Vilevile kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka kilomita 341 wenye thamani shilingi trilioni 3.7. Kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora - Tabora kilomita 294 na Tabora – Isaka kilomita 133 hadi Desemba, 2020 ni moja ya majukumu ambayo yatazingatiwa katika mpango huu. Kiasi cha shilingi trilioni 3.79 kimetumika katika kutekeleza mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, katika bandari ya Dar es Salaam shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuboreshwa kwa gati namba moja hadi nne kwa ajili ya mizigo mchanganyiko na gati namba nne kwa ajili ya mizigo ya kichele mfano ngano na mbolea, kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari na kuendelea na uboreshaji wa gati namba tano hadi saba, namba tano ni kwa ajili ya mizigo ya kichele na gati namba sita na saba ni kwa ajili ya makontena. Hatua hizi zimechangia kupungua kwa idadi ya siku za meli kukaa bandarini kutoka siku saba hadi siku tano na kuongezeka kwa shehena za mizigo iliyohudumiwa kutoka tani milioni 15.4 hadi milioni 19.52. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha shilingi bilioni 253.7 kimetumika kuboresha mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanja vya ndege na rada, kukamilika kwa Jengo la Tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere chenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka, kuendelea kwa ujenzi wa viwanja vya Geita asilimia 86.6, Songea asilimia 91 na Mtwara asilimia 49. Pia kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha kimataifa cha Msalato ambapo utagharimu Dola za Kimarekani milioni 330 sawa na shilingi bilioni 759, uzinduzi wa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vinavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuanza kwa ujenzi na upanuzi wa uwanja wa Musoma, kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege na kununuliwa kwa magari mapya matatu ya zimamoto yenye uwezo wa kubeba lita za maji 10,000 kwa ajili ya viwanja vya ndege vya kimataifa Kilimanjaro. Vilevile kupanuliwa kwa barabara ya kuruka na kutua kwa ndege katika viwanja vya ndege vya Dodoma na kufungwa kwa mifumo ya kuongoza ndege, ni moja ya maeneo ambayo yamezingatiwa katika mapendekezo ya mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa miaka mitano ni kama ifuatavyo. Masuala ya msingi yatakwawezesha kufikia shabaha ya uchumi jumla ni pamoja na: Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani, kuhimili athari za majanga ya asili kama vile mafuriko, magonjwa ya mlipuko, ushiriki mpana wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi, hali nzuri ya hewa inayowezesha uzalishaji wa chakula cha ziada na kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, shabaha ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ni pamoja na: Kiwango cha ukuaji wa uchumi kuongezeka kutoka 6% kwa mwaka 2021 hadi kufikia wastani wa 8% ifikapo 2020/2026; Mapato ya ndani nikijumlisha mapato ya

halmashauri kuongezeka kutoka 15.9% ya pato la Taifa kwa mwaka 2021/2022 hadi 16.8% kwa mwaka 2025/2025; Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ya wastani wa 3% hadi 3.5% kwa kipindi cha muda wa kati; Akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji wa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mine; na sekta binafsi kuzalisha ajira zipatazo milioni nane katika Julai, 2021 hadi 2026.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano unajengwa katika misingi ya nguzo kuu tatu ambazo ni utawala bora; ukuaji wa uchumi; na maendeleo ya watu ambazo zinategemea maeneo makuu matano, kipaumbele kimojawapo katika maeneo makuu matano ni kama ifuatavyo: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; cha pili, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; ya tatu, ni kukuza biashara; ya nne ni kuchochea maendeleo ya watu; na tano ni kuendeleza rasilimaliwatu .

Mheshimiwa Spika, vile vile Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano kwa maana ya 2020/2022 hadi 2025/2026, utajumuisha utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kipaumbele, miradi hiyo ni pamoja na: Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *SGR*; Kufua umeme wa maji kwa maana ya Julius Nyerere ambazo ni *megawatt* 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima hadi Tanga kuchakata na kusindika gesi asilia; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Kufua umeme wa maji Ruhudji *megawatt* 358; Kufua umeme wa maji Rumakali *megawatt* 222; Makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga; ikijumuisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa. Mpango huu unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi tirioni 114.8 zikijumuisha mchango wa sekta binafsi trilioni 40.6 na sekta ya umma shilingi trilioni 74.2.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yamezingatia maoni yaliyotolewa katika mkutano na mijadala maalum na Kamati ya Uongozi wa Bunge, Wizara, Idara na Taasisi

mbalimbali za Serikali, Washirika wa Maendeleo wa sekta binafsi. Mapendekezo ya wadau ni kuwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uandaliwe kwa kuzingatia *model* zinazoendana na uchumi na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mpango yanapatikana katika kitabu cha Mapendekezo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano kwa maana ya 2021/2025 hadi 2025/2026. Katika kuhitimisha mapendekezo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano yatawezesha nchi yetu kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya mapendekezo ya maendeleo yaani 2025 ikiwemo: Kuboresha na kuimarisha hali ya maisha ya wananchi; Ukuaji wa uchumi wenye uwezo wa kuhimili ushindani; Kuimarika kwa misingi ya uchumi wa viwanda; Kudumisha mazingira ya amani, usalama na umoja; na Kuimarika kwa uongozi bora na utawala wa sheria, pamoja na kulenga jamii iliyoelimika na inayojifunza.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kimegawanyika katika sura kuu nane kama ambavyo mtaziona katika kitabu chenyewe. Hoja ninayoiwasilisha leo hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ina lengo la kuomba maoni na ushauri wa Waheshimiwa Bunge ili kuboresha mpango tunaouandaa. Hivyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge wakati wa majadiliano ya mapendekezo ya mpango huu pamoja na mambo mengine ni vyema wakajikita zaidi katika sura tatu ambazo ni sura ya tano inayohusu hatua mahususi za kuchukuliwa katika maeneo ya kipaumbele; sura ya sita inayohusu ugharamiaji na utekelezaji wa mpango; na sura ya nane inayohusu ufuatiliaji, tathimini ambazo ndiyo mpango halisi unaotekeleza mipango ya maendeleo kwa miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono kweli kweli. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchemba kwa uwasilishaji mzuri sana (*Makofi*)

Kama nilivyosema hapo awali amewasilisha kuwaombeni mpokee, mjadili na mtoe ushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/2026) ambao mpango huo humo kwenye *tablets* zenu, lakini pia amewasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2021/2022 ambao pia humo. Pia amewasilisha mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali wa mwaka 2021/2022, vitu vitatu. Cha nne ambacho kipo kwenye *tablets* zenu ni hotuba yake ambayo ameisoma hapa, kwa hiyo vimechambuliwa na kuainisha kwa mapana ya kutosha. Mtaona mpango ule wa miaka mitano ni rasimu imewekwa pale rasimu, kwa hiyo maana yake ni kwamba mapendekezo yenu yanaweza yakachukuliwa ili baadaye Bunge hili likiidhinisha sasa basi uweze kuwa mpango kamili.

Waheshimiwa Wabunge, muda si mrefu tutaanza mjadala na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa profesa Muhongo atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma na wengine watafuata. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Kamati ya mipango naomba tusimame wote.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Jambo hili tunaloliandea ni jambo la kikatiba na kwenye *tablets* zetu tunayo nakala ya Katiba, mle mtaona Bunge hili limepewa jukumu la kujadili mipango yote mikubwa ya nchi, ambalo hili ni jukumu mojawapo kubwa na zito.

Sasa baada ya Waziri kuwasilisha Kamati yetu ya Bajeti ilipitia mapendekezo haya, kwa hiyo itakuja kwanza. Baada ya Kamati ya Bajeti ndiyo wachangiaji watakapoanza, kwa hiyo nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili aje awasilishe na tumsikilize kwa makini kwa sababu amechambua kwa undani, inatusaidia sana wachangiaji tunaofuata baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti au mwakilishi wake, anakuja Mwenyekiti mwenyewe, karibu sana una nusu saa. *(Makofi)*

MHE. SILLO D. BARAN - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa uhai, afya njema na kuniwezesha kusimama hapa leo. Pia napenda kukishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kunitua ili niipeperusha bendera kwenye uchaguzi mkuu wa Bunge kwa ajili ya Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nitoe shukurani za dharti kwa wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa imani yao kubwa kwangu waliyonionesha kwa kura nyingi sana na kunipa ushindi wa kishindo ili niwe Mbunge wao. Napenda kuwaahidi kuwa sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kukushukuru wewe kwa kunitua kuwa Mjumbe wa Kamati hii ya Bunge ya Bajeti, kamati ambayo imeniwezesha leo kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa imani yao kwangu waliyonionesha kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati

hii. Nawashukuru sana, naahidi ushirikiano mkubwa katika utendaji wa majukumu yetu. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayoisoma hapa ni *summary* tu ya taarifa ya kamati yangu, hivyo naomba taarifa yote kama ilivyowekwa mezani asubuhi na Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua, Mbunge, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya awali, naomba sasa niwasilishe taarifa yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021). Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu, pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025, ulipangwa kwa kufuata mfumo wa kutekeleza Mipango ya Maendeleo

ya Miaka Mitano Mitano, hivyo tulianza kwa kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa (2011/2012 - 2015/2016) uliokuwa na dhima ya Kufungulia Fursa ya Ukuaji wa Uchumi; ukafuata Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/2017 – 2020/2021) wenye dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu na sasa tunajielekeza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/2022- 2025/2026) wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda Kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini zinaonyesha kuwa, utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na huu wa Pili tunaomaliza kutekeleza sasa umesaidia katika kujenga msingi wa uchumi imara na hivyo kupelekea nchi yetu uchumi wa kipato cha kati cha chini (*Lower - Middle Income Country*) mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); viashiria vya uchumi jumla; kwa kuwa huu ndio mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/2017 - 2020/2021), Kamati iliona ni vema kufanya tathmini na mapitio ya hali ya ukuaji wa uchumi wa Taifa katika vipindi vya utekelezaji wa Mpango wa Pili (Miaka minne) kwa kuangalia mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi pamoja na utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Lengo ni kuona kwa kiasi gani tumeweza kufikia malengo tuliyojiwekea pamoja na kuona changamoto zilizojitokeza na hivyo kuwa na nafasi ya kubainisha nini kifanyike kwenye Mpango wa Tatu tunaotegemea kuanza kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa pato la Taifa; katika kipindi cha miaka minne (2016 - 2019) ukuaji wa pato la Taifa umeendelea kuwa imara, ambapo pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.9. Ukuaji huu umekuwa ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji hasa katika miundombinu ya usafirishaji na

nishati; uchimbaji madini; uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato na kubana matumizi yasiyo ya lazima pamoja na hali nzuri ya hewa ambayo imepelekea kuongezeka kwa mazao katika sekta ya kilimo. Hata hivyo, pamoja na ukuaji huu unaoridhisha bado nchi haijaweza kufikia malengo yake ya ukuaji wa uchumi wa zaidi ya asilimia nane kama ilivyoainishwa katika malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kiwango ambacho kingesaidia kupunguza umaskini nchini kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa sekta zilizokua na ukuaji wa juu ni kama zinavyoonekana katika ukurasa wa tatu na nne wa Taarifa yetu. Kwa mwaka 2020, pato la Taifa lilikuwa kwa wastani wa asilimia 4.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 mwaka 2019. Kushuka kwa ukuaji huku kumechangiwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu uliochangiwa na mafuriko yaliyotokea katika maeneo mengi nchini pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa *COVID-19* ambao umeathiri ukuaji wa uchumi wa nchi nyingi duniani ikizingatiwa kuwa uchumi wetu pia unategemea ukuaji wa uchumi wa dunia. Hivyo, kutokana na mwenendo huu tutegemee ukuaji wetu wa pato la Taifa kuwa chini wa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Serikali; hadi Desemba, 2020, Deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 59 ikilinganishwa na shilingi trilioni 54.8 kipindi kama hicho mwaka 2019, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Kati ya kiasi hicho deni la ndani lilifikia shilingi trilioni 16.2 na deni la nje shilingi trilioni 42.8. Ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2020; deni letu ni himilivu kwa vigezo vyote vya Kimataifa. Hata hivyo, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali ione haja ya kujipima uhimilivu wake kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa pato la Taifa ambacho kwenye mpango hakijaripotiwa. Hii ni kwa sababu deni la Taifa huhudumiwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima

(*first charge*) katika matumizi ya Serikali. Vile vile Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa *credit rating* ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathmini ya viashiria vingine vya Uchumi ni kama inavyoonekana katika Taarifa yetu ukurasa wa nne, tano, sita na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/2017 – 2020/2021; mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ni kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, lakini pia katika Taarifa yetu unaonekana katika ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta zilizopewa kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/2017 – 2020/2021) wenye dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu umejielekeza katika kutekeleza vipaumbele vinavyohusu miundombinu (reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na nishati); Kilimo (mazao, mifugo, uwindaji, misitu na uvuvi); Viwanda; Madini; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii (afya, elimu na maji) na miradi maalum ya kimkakati (*Flagship Projects*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele yanayohusu miundombinu, kilimo, viwanda na huduma za jamii na ingependa kueleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Miundombinu; Barabara; katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa, Serikali imepiga hatua kubwa na ya kuridhisha katika kuboresha miundombinu ya barabara nchini ukizingatia kuwa nchi yetu yenye mtandao wa barabara (vijijini, wilaya, mkoa na barabara kuu) unaokadiriwa kufikia kilometa 143,279 ilikuwa

na barabara za lami kilometa 9,781 tu mwaka 2015. Hii inaonyesha kuwa katika maisha yote ya nchi yetu hadi kufikia mwaka 2015 tuliweza kujenga barabara za lami kilometa 9,781 tu sawa na asilimia saba ya mtandao wote wa barabara tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa inaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka mitano cha mwaka 2015 hadi Machi, 2020, Serikali imeweza kujenga kilometa 3,537.0 za lami katika maeneo mbalimbali nchini; kilometa 82.6 za kupunguza foleni katika miji mikubwa na hadi kufikia mwezi Juni, 2020 barabara zenye urefu wa kilometa 1,298.44 zilikuwa zipo katika hatua ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami, Serikali imeweza kukarabati kilometa 300.9 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja makubwa 12. Kiasi cha shilingi trilioni 8.60 kilitumika katika ujenzi huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya ya kuridhisha, bado kuna changamoto kubwa ya uwepo wa barabara bora na za kutosha nchini. Aidha, maeneo mengi hayafikiki kwa urahisi hasa kipindi cha masika kutokana na ubovu wa barabara na madaraja au kutokuwa na barabara kabisa. Hali hii inapelekea kuongeza gharama ya maisha hasa kwa upande wa upatikanaji wa huduma ya usafiri kwa wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwa barabara ambazo zinazofungua fursa za kiuchumi na barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa lengo la kukuza shughuli za kilimo, biashara na uwekezaji mathalani barabara ya Songea – Muhukulu - Mkenda na upanuzi wa barabara inayoelekea katika mpaka wa Tanzania na Zambia (Barabara ya Igawa-Tunduma; Matai – Kasesha *Border*;) na nyinginezo. Hivyo ni

mategemeo ya Kamati kuwa Mpango wa Tatu Maendeleo utazingatia maoni haya ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kujenga reli mpya ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge (SGR)* itakayogharimu Dola za Kimarekani Biloni 7.69 kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Reli hii itakapokamilika itasaidia sana kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda mikoani na nchi za jirani zinazotumia bandari zetu na hivyo kuchochea kilimo, uzalishaji, biashara na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali kwenye miundombinu ya reli nchini kwa kukarabati reli (DSM – Mwanza; DSM – Tanga – Arusha), ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa mapya. Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana, Kamati inaishauri katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo Serikali izingatie mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ikamilishe haraka mapitio ya Mkataba na Sheria inayosimamia Reli ya *TAZARA* ili kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha Tanzania kuisimamia na kuiendesha reli hiyo pamoja na miundombinu yake kwa upande wa Tanzania;

(ii) Serikali ione uwezekano wa kuunganisha reli zake zote ili kuwa na mtandao mmoja wa reli ikiwemo ujenzi wa reli ya *TAZARA* kutoka Tunduma kwenda Kasanga;

(iii) Serikali itafute haraka fedha za kukamilisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha *SGR* kutoka Makutopora – Tabora – Isaka, Isaka – Kigoma, Isaka – Katavi – Kalema ambazo hazijaanza kujengwa. Mapato yatakayopatikana kutoka katika uendeshaji wake yatumike kulipia deni la mkopo wa ujenzi;

(iv) Serikali ione uwezekano wa kujenga Bandari kavu katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma, Mwanza, Arusha na Shinyanga (Isaka) ili mizigo ya nchi jirani (*On Transit Cargo*) itakayosafirishwa na reli zetu ipokelewe na kupakiwa huko badala ya kuwalazimu kuja Dar es salaam; na (*Makofi*)

(v) Serikali ione uwezekano wa kuunganisha Eneo Maalum la Uwekezaji la Bagamoyo na Reli ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zitakazozalishwa hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa anga. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha usafiri wa anga nchini kwa kukarabati viwanja vya ndege, kujenga viwanja vipya katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kununua na kufunga Rada nne (4) za kuongoza ndege za kiraa katika viwanja vya ndege vya *Julius Nyerere International Airport, Kilimanjaro International Airport, Songwe* na Mwanza. Hatua hii imeweza kuboresha usafiri wa anga kuongeza hamasa ya maendeleo hasa katika sekta ya usafirishaji, biashara na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha Shirika letu la Ndege (*ATCL*) kwa kununua ndege 8, kuendelea na mchakato wa kununua ndege nyingine 3 na imepanga kununua ndege nyingine zikiwemo ndege za mizigo. Kamati inaishauri *ATCL* kuongeza safari zake za ndani pamoja na kusafirisha mizigo zaidi hasa mbogamboga, maua nyama na samaki kutoka hapa nchini kwenda nchi za nje. Aidha, Serikali iongeze kasi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Songea, Iringa, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nishati. Serikali imepata mafanikio makubwa katika usambazaji wa umeme vijijini kutoka vijiji 2,018 mwaka 2015 hadi kufikia vijiji 10,018 Desemba, 2020. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini umefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto ya uunganishwaji wa umeme katika

nyumba (*households connection*) ambao ni asilimia 39.9 tu za nyumba katika maeneo ya mijini na asilimia 24.3 tu ya nyumba maeneo ya vijijini. Pia, bado kuna upotevu wa umeme wakati wa usafirishaji kutoka eneo la uzalishaji hadi eneo la usambazaji. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia ya haraka ya kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipanga ifikapo mwaka 2020/2021 uzalishaji wa umeme nchini uwe umefikia kiwango cha 4,915 MW kutoka 1,308 MW mwaka 2015/2016. Hata hivyo, hadi kufikia mwaka 2019/20 uzalishaji umefikia kiwango cha 1,602.3 MW tu. Ni matumaini ya Kamati kuwa ukamilishaji wa Mradi wa kipekee wa kuzalisha umeme wa Maji wa Julius Nyerere utakaozalisha 2,115 MW, Mradi wa Rusumo 80 MW; *Kinyerezi I Extension* 185 MW; Mradi wa Ruhudji 358 MW na Mradi wa Rumakali 222 MW itaweza kusaidia kupunguza kiwango cha upungufu wa umeme na hivyo kufikia lengo lililokusudiwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hatua hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa uhakika wa umeme wa gharama nafuu kwa wenye viwanda na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ndiyo msingi wa uchumi wa viwanda kwa sababu ndiyo sekta zalishi ya malighafi ambazo zinatumiwa viwandani na ndiyo yenye kuajiri zaidi ya asilimia 66 ya wananchi wa Tanzania. Kilimo si tu kina athari kubwa katika uchumi wa nchi lakini pia kina mchango mkubwa sana katika kuamua hatma ya maisha ya kila siku na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa ilikuwa ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 7.6 kwa mwaka 2020. Hata hivyo, hadi sasa ukuaji wa Sekta ya Kilimo umefikia asilimia 4.4 kwa mwaka 2019, chini ya lengo lililokusudiwa la asilimia 7 kwenye Mpango wa Pili. Aidha, uchangiaji wa Pato la Taifa umeweza kufikia asilimia 26.6 na hivyo kushindwa kufikia lengo la uchangiaji wa asimilia 29.4 kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali wakati ikitekeleza Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo izingatie yafuatayo:-

(i) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi;

(ii) Kuendelea kuhamasisha na kukuza kilimo cha umwagiliaji;

(iii) Kuboresha masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;

(iv) Kuendelea kufanya utafiti kwa lengo la kuzalisha mbegu bora za asili zinazopatikana kwa bei nafuu kwa wakulima;

(v) Kuendelea kuhamasisha upatikanaji wa pembejeo na madawa ya kilimo kwa wakati na gharama nafuu;

(vi) Kuanzisha vituo/masoko ya kukusanyia au kufanyia mauzo ya mazao katika kila wilaya na baadaye Kata ili kuwapunguzia wakulima gharama ya kutafuta masoko. Aidha, Vituo hivi viunganishwe na Soko la Mazao (*Tanzania Mercantile Exchange – TMX*);

(vii) Kuendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kuboresha shughuli za Kilimo hasa ile ya *ASDP II*;

(viii) Serikali ikamilishe haraka mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi pamoja na viwanda vya samaki; na

(xi) Kuboresha utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani na uhusishe mazao yote ya biashara ili kurahisisha mazao hayo kuuzwa katika soko la mazao (*TMX*)

(x) Serikali ifanyie ukarabati wa haraka machinjio za kisasa na kupata ithibati (hati ya ubora) kwa nyama inayozalishwa nchini ili kuwezesha kuweza kuuza nyama yetu

moja kwa moja katika masoko ya Ulaya, Asia na Uarabuni badala la kutegemea kupitia nchi jirani; (*Makofi*)

(xi) Serikali ianzishe hapa nchini Masoko ya mazao makuu ya biashara kama vile chai, kahawa, pareto na kakao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda na Biashara. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mazingira bora yaliyowezesha kuanzisha viwanda vingi nchini. Takwimu zinaonesha kwamba katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kiasi cha viwanda 8,477 vimeanzishwa. Kati ya viwanda hivyo, 201 ni vikubwa, 460 vya kati, 3,406 ni vidogo na 4,410 ni vidogo sana na kusababisha ajira katika viwanda kuongezeka kutoka 254,687 mwaka 2015 hadi 482,601 mwaka 2019. Ongezeko la idadi ya viwanda na uzalishaji imewezesha nchi yetu kuweza kujitoshesha katika baadhi ya bidhaa muhimu zikiwemo saruji, marumaru, nondo, vifaa vya umeme, mabomba ya plastiki, mahindi, mchele na vyandarua. Haya ni mafanikio yanayotia moyo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulinda viwanda vyetu na kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya viwanda ni vema Serikali ikaja na mkakati utakaoviwezesha viwanda vyetu vya ndani kuwa shindani na kuzalisha zaidi. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuzuia uingizaji wa bidhaa kwa wingi (*dumping*) pamoja na kuzuia kuingiza bidhaa zisizo na ubora. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Kuwezesha Biashara (*Business Facilitation Act*) pamoja na Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (*Trade Remedies Act*) kabla ya Julai 01, 2021. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya mipakani yanatoa mchango mkubwa sana wa uchumi kupitia biashara. Mfano halisi ni mipaka ya Namanga na Tunduma. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya mipaka yetu na nchi jirani bado hayajaweza kuleta mchango unaostahili wa manufaa ya kibiashara na kiuchumi. Kwa mfano, nchi yetu imepakana

na nchi ya Msumbiji katika Mkoa wa Ruvuma. Kwa kutambua umuhimu wa eneo hili, Serikali imejenga Soko la Kimataifa la Mkenda, ambalo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ubovu wa barabara ya Songea – Mhukulu – Mkenda (*Border*) soko hili halijaweza kufanya kazi. Mpaka wa Tanzania na Msumbiji Mkoani Ruvuma katika eneo la Mkenda unaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi Kusini mwa nchi yetu endapo utaboreshwa kwa kujengewe miundombinu ya muhimu hasa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iweze kuwa na ushindani wa kibiashara katika ukanda wa *SADC, EAC*, Africa na dunia kwa ujumla, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo inazingatia yafuatayo:-

(i) Kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kuchakata mazao ya mifugo na mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kuyatafutia masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi yetu;

(ii) Serikali ikamilishe haraka uanzishwaji wa masoko ya mipakani ikiwemo kuanza matumizi ya Soko la Mkenda lililopo katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji Mkoa wa Ruvuma;

(iii) Serikali ianzishe viwanda vya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya matumizi yetu na kuuza katika Nchi cha *SADC*, Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla; na

(iv) Serikali ikiwezeshe Kiwanda cha *Biotech Production Limited* kilichopo Kibaha ili kiendeleo kuzalisha viluilui wa kuua vijidudu wa mbu wanaoeneza malaria na magonjwa mengine ili kutokomeza kabisa malaria nchini na hivyo kupunguza vifo na gharama kubwa inayotumika kutibu ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ardhi na Mazingira. Ardhi ni rasilimali muhimu katika kuleta maendeleo. Hivyo, kuna umuhimu wa kuzingatia upatikanaji wa ardhi na haki

ya kuitumia katika maendeleo. Aidha, takwimu za sasa zinaoneesha kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa asilimia 3.1 kila mwaka na hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya ardhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji na uwekezaji. Aidha, takribani ya asilimia 70 ya watu wa Tanzania wanaishi maeneo ya vijijini wanategemea ardhi katika upatikanaji wa mahitaji yao ya maisha. Hali hii imesababisha kuwa na migogoro mikubwa ya ardhi pamoja na uharibifu mkubwa wa misitu na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa mpango tunaotekeleza sasa haujaweza kusaidia katika kutatua matatizo yanayohusu ardhi na usimamizi wa mazingira. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kunakuwepo mipango ya matumizi bora ya ardhi, uhifadhi wa mazingira na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hata hivyo, nguvu zaidi inahitajika ili kuendana na kasi ya ongezeko la watu ambao hadi mwaka 2019 wamefikia takribani watu milioni 55.9. Serikali lazima ihakikishe utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa upande wa vijiji, wilaya na mikoa unakamilika haraka, pia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya utatuzi wa migogoro ya ardhi wahakikishe yanatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, kwa upande wa mazingira, Serikali ihakikishe inaendeleza juhudi za kuhamasisha utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na kusimamia programu na sera za usimamizi wa mazingira, mafunzo ya uchambuzi na athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii. Tanzania ndiyo nchi pekee duniani ambayo imetenga eneo lake kubwa kiasi cha asilimia 25 kwa ajili shughuli za kuhifadhi na kuendeleza shughuli za utalii kama vile Hifadhi ya Taifa, maeneo tengefu na maeneo ya uhifadhi. Aidha, sekta hii imeendelea kufanya vizuri katika kuchangia Pato la Taifa (asilimia 17.7) pamoja na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi (asilimia 24).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inaona kuwa juhudi mahsusi zinahitajika ili tuweze

kufikisha malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa upande wa kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni 1.7 na mchango katika Pato la Taifa kufikia asilimia 18.3. Haya yote yanaweza kufikiwa kwa:-

(i) Kuendelea kuhamasisha na kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi;

(ii) Kuongeza bidhaa za huduma na utalii pamoja na kuendelea kuaninisha maeneo mapya ya utalii;

(iii) Kuboresha miundombinu katika hifadhi za taifa, maeneo tengefu na maeneo ya uhifadhi; na

(iv) Kuendelea kuboresha mafunzo yanayotolewa na vyyo vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi. Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushauri kwa sababu ya muda ungeenda kwenye maoni sasa.

MHE. SILLO D. BARAN - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya jumla ya Kamati kuhusu Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/2022-2025/2026). Uanzishaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano umejielekeza katika kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazoweza kushindana kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa hizo ndani na nje

ya nchi. Lengo likiwa ni kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini pamoja na kuongeza uuzaji wa bidhaa shindani nje ya nchi. Kamati inaona kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunaanza na viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazotumia malighafi zinazopatikana nchini.

MWENYEKITI: Bado dakika tano. Ungeenda tu kwenye maoni ya jumla ingetuweka pazuri zaidi, nyingine hizi watasoma Waheshimiwa Wabunge na *Hansard* imeshachukua.

MHE. SILLO D. BARAN - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nihitimishe. Napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Aidha, kipekee napenda kumshukuru, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Mbunge, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Katibu Mkuu Fedha, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara na wataalam wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili mapendekezo ya mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua kama walivyoorodheshwa katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuipongeza Sekretarieti ya Kamati yangu kwa ushauri mzuri unaotusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21), MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22-2025/26) PAMOJA NA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/17-2020/21), Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22-2025/26) pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wenye dhima ya **“Kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”** pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025 ulipangwa kwa kufuata mfumo wa kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano Mitano, hivyo tulianza kwa kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa (2011/2012 -2015/2016) uliokuwa na dhima ya **“Kufungulia fursa ya Ukuaji wa Uchumi” (Unleashing Tanzania’s Latent Growth Potential)**; ukafuata Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/2017 – 2020/21) wenye dhima

“Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”(Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development) na sasa tunajielekeza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/2022- 2025/2026) wenye dhima ya **“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda Kwa Maendeleo ya Watu” (Realising Competitiveness and Industrialisation for Human Development).**

Mheshimiwa Spika, tathmini zinaonyesha kuwa utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na huu wa Pili tunaomaliza kutekeleza sasa umesaidia katika kujenga msingi wa Uchumi imara na hivyo kupelekea kufanikiwa kutimiza azma ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ya kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati (***Lower - Middle Income Country***) mwaka 2020.

2.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21)

2.1. Viashiria vya Uchumi Jumla


Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ndio mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/17-2020/21), Kamati iliona ni vema kufanya tathmini na mapitio wa hali ya ukuaji wa Uchumi wa Taifa katika vipindi vya utekelezaji wa Mpango wa Pili (Miaka 4) kwa kuangalia mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi pamoja na utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Pili na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Lengo ni kuona kwa kiasi gani tumeweza kufikia malengo tuliojiwekea pamoja na kuona changamoto zilizojitokeza na hivyo kuwa na nafasi ya kubainisha nini kifanyike kwenye Mpango wa Tatu tunaotegemea kuanza kuutekeleza.

2.1.1. Ukuaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 4 (2016-2019) ukuaji wa Pato la Taifa umeendelea kuwa imara, ambapo Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa **asilimia 6.9**. Ukuaji huu umekuwa ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji hasa katika miundombinu ya usafirishaji na nishati; uchimbaji madini; uimarishaji wa

ukusanyaji wa mapato na kubana matumizi yasiyo ya lazima pamoja na hali nzuri ya hewa ambayo imepelekea kuongezeka kwa mazao katika sekta ya kilimo. Hata hivyo, pamoja na ukuaji huu unaoridhisha bado nchi haijaweza kufikia malengo yake ya ukuaji wa uchumi wa zaidi ya **asilimia 8** kama ilivyoainishwa katika malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kiwango ambacho kingesaidia kupunguza umaskini nchini kwa kasi zaidi.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha Miaka 4



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kati ya kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 takwimu zinaonesha kuwa sekta zilizokuwa na ukuaji wa juu ni ujenzi (**asilimia 14.4**); uzalishaji (**asilimia 8.3**), usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (**asilimia 8.2**); uchimbaji wa madini na mawe (**asilimia 8**); habari na mawasiliano (**asilimia 6.2**). Hii ina maana kwamba ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa unachochea na shughuli za ujenzi, uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma. Kwa upande wa wa sekta ya kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uvuvi) ukuaji wake umekuwa sio wa kuridhisha licha ya kuwa inaajiri watazania wengi (**asilimia 66**). Takwimu inaonyesha kuwa sekta hii imekuwa kwa wastani wa chini ya **asilimia 5**, ukuaji ambao ni chini ya malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa kukua kwa **asilimia 7.6**. Vilevile uchangiaji wa sekta hii katika Pato la Taifa

umeshuka kutoka **asilimia 29.0** mwaka 2016 hadi **asilimia 26.6** mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020 Pato la Taifa lilikuwa kwa wastani wa **asilimia 4.7** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 6.9** mwaka 2019. Kushuka kwa ukuaji huku kumechangiwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu uliochangiwa na mafuriko yaliyotokea katika maeneo mengi nchini pamoja mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambao umeathiri ukuaji wa uchumi wa nchi nyingi duniani ikizingatiwa kuwa uchumi wetu pia unategemea ukuaji wa uchumi wa dunia. Hivyo, kutokana na mwenendo huu tutegemee ukuaji wetu wa Pato la Taifa kuwa chini wa wastani wa **asilimia 6.9** kwa mwaka 2020/21.

2.1.2. Wastani wa Pato la Kila Mtu

Mheshimiwa Spika, Kutokana na ukuaji imara wa uchumi kwa wastani wa zaidi ya **asilimia 6** katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, mwezi Julai 2020 Benki ya Dunia ilitangaza Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za kipato cha kati cha chini. Hatua hii ilitokana na kuongezeka kwa pato la mtu (GNI) kutoka **shilingi 2,452,406 (sawa na dola za Marekani 1,020)** mwaka 2018 hadi **shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,080)** mwaka 2019, kiasi hicho ni juu ya kiasi kilichowekwa na Benki ya Dunia cha **dola za Marekani 1,036** ili nchi iweze kufikia hadhi ya kipato cha kati cha chini (Lower-middle income status). Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha Nchi imefikia lengo la kuwa nchi ya kipato cha kati miaka mitano kabla wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.


Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yamechangiwa na kasi ya ukuaji wa uchumi wa wastani wa **asilimia 6.9** kwa kipindi cha miaka minne (2016-2019); utegemezi wa kibajeti kutoka **asilimia 14.0** ya bajeti halisi mwaka 2014/15 hadi **asilimia 9.3** mwaka 2019/20; ujenzi wa miundombinu muhimu ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi (miundombinu, umeme, elimu, afya na maji) pamoja na utawala bora. Aidha, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 23 za Afrika zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini.

2.1.3. Mfumuko wa bei

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha chini na kubaki katika wigo wa tarakimu moja **asilimia 4.4** katika kipindi cha miaka minne 4 (2016-2019) na hivyo kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa kiwango cha kutokuzidi **asilimia 5** ya Mfumuko wa Bei. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kudhibiti mwenendo wa ukuaji wa mfumuko wa bei kwa utekelezaji thabiti wa sera za fedha na kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Kwa kiasi kikubwa Mfumuko wa bei nchini huchangiwa kwa kiwango kikubwa na upatikanaji wa chakula nchini na nchi jirani pamoja na bei ya mafuta katika soko la dunia. Kwa kuwa Nchi yetu haina uwezo wa kuamua bei ya mafuta katika soko la duniani ni vema tukajikita katika kuhakikisha Taifa linakuwa na chakula cha kutosha kwa ajili ya watu wake na kuweza kuuza kwa majirani zetu.

Kielelezo Na.2: Mfumuko wa Bei



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.


2.1.4. Mwenendo wa viwango vya ubadilishaji wa fedha

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miaka 4 iliyopita thamani ya Shilingi imeendelea kuwa imara dhidi ya Sarafu kubwa. Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2019/20 inaonyesha kwamba hadi mwishoni mwa mwaka 2016/17 kiwango cha kubadilisha dola moja ya Kimarekani ilikuwa ni **Shilingi 2,230.1** na mwishoni mwa mwaka 2019/20 dola moja

ya marekani ilibadirishwa kwa **Shilingi 2,295.5**. Utulivu wa thamani ya fedha yetu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa urari wa biashara kati yetu na washirika wetu wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Utulivu huu umepelekea uwepo wa fedha za kigeni za kutosha na hivyo kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 5.6** (Desemba, 2020) na hivyo kumeiwezesha nchi yetu kuendana na vigezo vilivyowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC) vya miezi 4.5. Mafanikio haya yanastahili pongezi.

Kielelezo Na.3. Mwenendo wa Viwango vya Riba



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.


2.1.5. Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2020, Deni la Serikali lilifikia **shilingi trilioni 59** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 54.8** kipindi kama hicho mwaka 2019 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 7.6**. Kati ya kiasi hicho deni la ndani lilifikia **shilingi trilioni 16.2** na deni la nje **shilingi trilioni 42.8**. Ongezeko la deni limetokana na Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2020, deni letu ni himilivu kwa vigezo vyote vya Kimataifa na hivyo, Nchi yetu ina uwezo

wa kukopa ndani na nje, na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi. Pamoja na kwamba deni hilo ni himilivu kwa viashiria vyote muhimu, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali ione haja ya kujipima uhimilivu wake kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa Pato la Taifa ambacho kwenye mpango hakijaripotiwa. Hii ni kwa sababu deni la Taifa huhudumiwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima (*first charge*) katika matumizi ya Serikali. Vile vile Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa *credit rating* ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi.

Kielelezo Na.4. Mwenendo wa Deni la Serikali.



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.

2.1.6. Mwenendo wa Huduma za kibenki na viwango vya riba

Mheshimiwa Spika; Katika kipindi cha miaka minne (2016 - 2019), viwango vya riba katika masoko ya fedha vimeendelea kutegemea nguvu ya soko na hali ya ukwasi unaotokana na sera za fedha na kibajeti. Viwango vya riba za dhamana za Serikali umepungua kutoka **asilimia 16.7** mwaka 2016 hadi **asilimia 7.71** mwaka wa fedha 2019. Aidha, Riba za mikopo kwenye mabanki ya biashara katika kipindi hicho ziliongezeka kutoka **asilimia 15.96** mwaka wa fedha

2016 na kufikia **asilimia 16.97** mwaka 2019. Riba za amana za akiba zilipungua kutoka **asilimia 3.35** katika mwaka 2016 na kufikia **asilimia 2.44** mwaka 2019. Hatua hii ilifikiwa baada ya Benki Kuu kutekeleza sera ya fedha kwa kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kilichotakiwa kuwekwa Benki Kuu na Mabenki (Statutory Minimum Reserve) kutoka **asilimia 7** kwenda **asilimia 6** ya amana zote za kila Benki. Vilevile Benki kuu ilipunguza kiwango cha riba kwa Mabenki yanapokopa Benki Kuu (Discount Rate) kutoka **asilimia 12** kwenda **asilimia 9** na mwaka 2020 ilipunguzwa na kufikia **asilimia 5**, lengo lilikuwa kuongeza ukwasi ili kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na hatimaye ukuaji wa uchumi. Hata hivyo pamoja na hatua hizi zilizofanywa na Serikali kupitia Benki Kuu, bado mabenki ya biashara yamekuwa yakitoa mikopo kwa sekta binafsi katika kiwango cha riba kisichovutia mkopaji. Aidha, bado tofauti kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja imekuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kupelekea kuongezeka kwa gharama za fedha kwa wawekezaji katika sekta binafsi.

2.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/17 – 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ulikadiriwa kugharimu **Shilingi trilioni 107**, sawa na wastani wa **Shilingi trilioni 21.4** kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano. Sekta ya umma ilitarajiwa kuchangia kiasi cha **Shilingi trilioni 59**, huku sekta binafsi ikitarajiwa kuwekeza **Shilingi trilioni 48**.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo kwa miaka minne ya kwanza umebaini kuwa sekta ya umma ilichangia Shilingi **trilioni 34.9**, sawa na **asilimia 76.5** ya lengo la miaka minne ya **Shilingi trilioni 45.6**. Aidha, katika kipindi hicho, Sekta Binafsi ilichangia kiasi cha **Shilingi trilioni 32.6** sawa na **asilimia 85** ya matarajio ya **Shilingi trilioni 38.4**. Maeneo makuu yaliyowekezwa na sekta binafsi ni pamoja na maendeleo ya viwanda, shule binafsi, hospitali, hoteli, madini, usafirishaji na uhifadhi.

2.3. Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17 – 2020/21)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17 – 2020/21) wenye dhima ya **“Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”** umejielekeza katika kutekeleza vipaumbele vinavyohusu Miundombinu (Reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na nishati); Kilimo (Mazao, Mifugo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi); Viwanda; Madini; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii (Afya, Elimu na Maji) na miradi maalum ya kimbakati (Flagship Projects).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imechambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele; muda wa kati na mrefu wa utekelezaji wa kila kipaumbele; na uwajibikaji wa wataalamu wa sekta husika katika kila kipaumbele. Mchanganuo huu umetoa picha halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo mpaka sasa. Kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inatoa tathmini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya kissekta kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele yanayohusu miundombinu, kilimo, Viwanda na Huduma za jamii na ingependa kueleza yafuatayo;

2.3.1. Sekta ya Miundombinu

2.3.1.1. Barabara

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa, Serikali imepiga hatua kubwa na ya kuridhisha katika kuboresha miundombinu ya barabara nchini ukizingatia kuwa Nchi yetu yenye urefu wa mtandao wa barabara (vijijini, wilaya, mikoa na barabara kuu) unaokadiriwa kufikia kilometa 143,279 ilikuwa na barabara za lami kilometa 9,781 tu mwaka 2015. Hii inaonyesha kuwa katika maisha yote ya nchi yetu hadi kufikia mwaka 2015 tuliweza kujenga barabara za lami

kilometa 9,781 tu sawa na asilimia 7 ya mtandao wote wa barabara tulionao.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa inaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka mitano cha Mwaka 2015 hadi Machi, 2020 Serikali imeweza kujenga kilometa 3,537.0 za lami katika maeneo mbalimbali nchini, kilometa 82.6 za kupunguza foleni katika miji mikubwa na hadi kufikia mwezi Juni, 2020 barabara zenye urefu wa kilometa 1,298.44 zilikuwa zipo katika hatua ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Pamoja na ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami, Serikali imeweza kukarabati kilometa 300.9 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja makubwa 12. Kiasi cha **shilingi trilioni 8.60** kilitumika katika ujenzi huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya ya kuridhisha, bado kuna changamoto kubwa ya uwepo wa barabara bora na za kutosha nchini. Aidha, maeneo mengi hayafikiki kwa urahisi hasa kipindi cha masika kutokana na ubovu wa barabara na madaraja au kutokuwa na barabara kabisa. Hali hii inapelekea kuongeza gharama ya maisha hasa kwa upande wa upatikanaji wa huduma ya usafiri kwa wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwa barabara ambazo zinazofungua fursa za kiuchumi na barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa lengo la kukuza shughuli za kilimo, biashara na uwekezaji mathalani barabara ya Songea – Muhukulu - Mkenda na upanuzi wa barabara inayoelekea katika mpaka wa Tanzania na Zambia (Barabara Igawa- Tunduma; Matai – Kasesha border;) na nyinginezo. Hivyo ni mategemeo ya Kamati kuwa Mpango wa Tatu Maendeleo utazingatia maoni haya ya Kamati.

2.3.1.2. Reli

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kujenga Reli mpya ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge

(SGR) itakayo gharimu **Dola za Kimarekani Bilioni 7.69** kutoka Dar es salaam hadi Mwanza. Reli hii itakapokamilika itasaidia sana kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Mikoani na nchi za jirani zinazotumia bandari zetu na hivyo kuchochea kilimo, uzalishaji, biashara na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali kwenye miundombinu ya reli nchini kwa kukarabati reli (DSM-Mwanza; DSM-Tanga-Arusha), ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa mapya. Hata hivyo pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana, Kamati inaishauri Katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo Serikali izingatie mambo yafuatayo;

(i) Serikali ikamilishe haraka mapitio ya Mkataba na Sheria inayosimamia Reli ya TAZARA ili kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha Tanzania kuisimamia na kuiendesha reli hiyo pamoja na miundombinu yake kwa upande wa Tanzania;

(ii) Serikali ione uwezekano wa kuunganisha reli zake zote ili kuwa na mtandao mmoja wa reli ikiwemo ujenzi wa reli ya TAZARA kutoka Tunduma kwenda Kasanga;

(iii) Serikali itafute haraka fedha za kukamilisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha SGR kutoka Makutupora-Tabora-Isaka, Isaka – Kigoma, Isaka – Katavi-Kalema ambazo hazijaanza kujengwa. Mapato yatakayopatikana kutoka katika uendeshaji wake yatumike kulipia deni la mkopo wa ujenzi;

(iv) Serikali ione uwezekano wa kujenga Bandari kavu katika Mikoja ya Mbeya, Kigoma, Mwanza, Arusha na Shinyanga (Isaka) ili mizigo ya nchi jirani (On Transit Cargo) itakayosafirisha na reli zetu ipokelewe na kupakiwa huko badala ya kuwalazimu kuja Dar es salaam; na

(v) Serikali ione uwezekano wa kuunganisha Eneo Maalum la uwekezaji la Bagamoyo na Reli ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zitakazozalishwa hapo.

2.3.1.3. Usafiri wa Anga

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha usafiri wa anga nchini kwa kukarabati viwanja vya ndege, kujenga viwanja vipya katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kununua na kufunga Rada nne (4) za kuongoza ndege za kiraia katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, Songwe na Mwanza. Hatua hii imeweza kuboresha usafiri wa anga kuongeza hamasa ya maendeleo hasa katika sekta ya usafirishaji, biashara na utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha Shirika letu la ndege (ATCL) kwa kununua ndege 8, kuendelea na mchakato wa kununua ndege nyingine 3 na imepanga kununua ndege nyingine zikiwemo ndege za mizigo. Kamati inaishauri ATCL kuongeza safari zake za ndani pamoja na kusafirisha mizigo zaidi hasa mbogamboga, maua nyama na samaki kutoka hapa nchini kwenda nchi za nje. Aidha, serikali iongeze kasi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Songea, Iringa, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga.

2.3.2. Sekta ya Nishati

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio makubwa katika usambazaji wa umeme vijijini kutoka vijiji 2,018 mwaka 2015 hadi kufikia vijiji 10,018 Desemba, 2020. Aidha ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini umefanyika. Pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto ya uunganishwaji wa umeme katika nyumba (Households connection) ambao ni **asilimia 39.9** tu za nyumba katika maeneo ya mijini na **asilimia 24.3** tu ya nyumba maeneo ya vijijini. Pia, bado kuna upotevu wa umeme wakati wa usafirishaji kutoka eneo la uzalishaji hadi eneo la usambazaji. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia ya haraka ya kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga ifikapo mwaka 2020/21 uzalishaji wa umeme nchini uwe umefikia kiwango cha 4,915 MW kutoka 1,308 MW mwaka 2015/16. Hata hivyo hadi kufikia mwaka 2019/20 uzalishaji umefikia kiwango cha 1,602.3 MW tu. Ni matumaini ya Kamati kuwa ukamilishaji wa Mradi wa

kipekee wa kuzalisha umeme wa Maji wa Julius Nyerere utakaozalisha 2,115 MW, Mradi wa Rusumo 80 MW; Kinyerezi I Extension 185 MW; Mradi wa Ruhudji 358 MW na Mradi wa Rumakali 222 MW itaweza kusaidia kupunguza kiwango cha upungufu wa umeme na hivyo kufikia lengo lililokusudiwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hatua hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa uhakika wa umeme wa gharama nafuu kwa wenye viwanda na wananchi.

2.3.3. Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, Sekta ya kilimo ndio msingi wa uchumi wa Viwanda kwasababu ndio sekta zalishi ya malighafi ambazo zinatumika viwandani na ndiyo yenye kuajiri zaidi ya **asilimia 66** ya wananchi wa Tanzania. Kilimo si tu kina athari kubwa katika Uchumi wa Nchi lakini pia kina mchango mkubwa sana katika kuamua hatma ya maisha ya kila siku na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa ilikuwa ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka **asilimia 3.4** kwa mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 7.6** kwa mwaka 2020. Hata hivyo, hadi sasa ukuaji wa Sekta ya kilimo umefikia **asilimia 4.4** kwa mwaka 2019 chini ya lengo lililokusudiwa la **asilimia 7** kwenye Mpango wa Pili. Aidha uchangiaji wa Pato la Taifa umeweza kufikia **asilimia 26.6** na hivyo kushindwa kufikia lengo la uchangiaji wa **asilimia 29.4** kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa bado utekelezaji wa miradi ya sekta ya kilimo ipo nje ya malengo tuliyojiwekea hasa kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya thamani. Bado kuna changamoto ya kufikia malengo ya kuuza mazao yetu nje ya nchi. Aidha, kwa upande wa kilimo cha Umwagiliaji kimeongezeka kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020, ukilinganisha na lengo la mpango wa Pili wa kufikia hekta 700,000.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutofikia kwa malengo kwenye sekta ya kilimo, Serikali inaendelea na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, kujenga viwanda vya kuongeza thamani

mazao. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali wakati ikitekeleza Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo izingatie yafuatayo;

i) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi;

ii) Kuendelea kuhamasisha na kukuza kilimo cha umwagiliaji;

iii) Kuboresha masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;

iv) Kuendelea kufanya utafiti kwa lengo la kuzalisha mbegu bora za asili zinazopatikana kwa bei nafuu kwa wakulima;

v) Kuendelea kuhamasisha upatikanaji wa pembejeo na madawa ya kilimo kwa wakati na gharama nafuu;

vi) Kuanzisha vituo/masoko ya kukusanyia au kufanyia mauzo ya mazao katika kila wilaya na baadae Kata ili kuwapunguzia wakulima gharama kutafuta masoko. Aidha, Vituo hivi viunganishwe na Soko la Mazao (*Tanzania Mercantile Exchange – TMX*);

vii) Kuendelea na utekelezaji wa program mbalimbali za kuboresha shughuli za Kilimo hasa ile ya ASDP II;

viii) Serikali ikamilishe haraka mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi pamoja na viwanda vya samaki; na

ix) Kuboresha utaratibu wa Stakabadhi ya mazao gharani na uhisishie mazao yote ya biashara ili kurahisisha mazao hayo kuuzwa katika soko la mazao (TMX)

x) Serikali ifanyie ukarabati wa haraka machinjio za kisasa (arbor-tour) na kupata ithibati (hati ya ubora) kwa nyama inayozalishwa nchini ili kuwezesha kuweza kuuza nyama yetu moja kwa moja katika masoko ya Ulaya, Asia na Uarabuni badala la kutegemea kupitia nchi jirani;

xi) Serikali ianzishe hapa nchini Masoko ya Mazao Makuu ya Biashara kama vile Chai, Kahawa, Pareto na Kakao.

2.3.4. Sekta ya Viwanda na Biashara

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mazingira bora yaliyowezesha kuanzisha viwanda vingi nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kiasi cha viwanda 8,477 vimeanzishwa. Kati ya viwanda hivyo, 201 ni vikubwa, 460 vya kati, 3,406 ni vidogo na 4,410 ni vidogo sana na kupelekea ajira katika viwanda kuongezeka kutoka 254,687 mwaka 2015 hadi 482,601 mwaka 2019. Ongezeko la idadi ya viwanda na uzalishaji imewezesha nchi yetu kuweza kujitoshesha katika baadhi ya bidhaa muhimu zikiwemo saruji, marumaru, nondo, vifaa vya umeme, mabomba ya plastiki, mahindi, mchele na vyandarua. Haya ni mafanikio yanayotia moyo sana.

Mheshimiwa Spika, Ili kulinda viwanda vyetu na kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya Viwanda ni vema Serikali ikaja na mkakati utakaoviwezesha Viwanda vyetu vya ndani kuwa shindani na kuzalisha Zaidi. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuzuia uingizaji wa bidhaa kwa wingi (Dumping) pamoja na kuzuia kuingiza bidhaa zisizo na ubora. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Kuwezesha Biashara (Business Facilitation Act) pamoja na Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedies Act) kabla ya Julai 1, 2021.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Mipakani yanatoa mchango mkubwa sana wa uchumi kupitia biashara. Mfano halisi ni Mipaka ya Namanga na Tunduma. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya mipaka yetu na nchi jirani bado hajaweza kuleta mchango unaostahili wa manufaa ya kibiashara na kiuchumi. Kwa mfano Nchi yetu imepakana na nchi ya Msumbiji katika mkoa wa Ruvuma. Kwa kutambua umuhimu wa eneo hili, Serikali imejenga Soko la Kimataifa la Mkenda, ambalo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ubovu wa barabara ya Songea – Mhukulu – Mkenda (Border) soko hili halijaweza kufanya kazi. Mpaka wa Tanzania na Msumbiji

Mkoani Ruvuma katika eneo la Mkenda unaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kusini mwa nchi yetu endapo utaboreshwa kwa kujengewe miundombinu ya muhimu hasa barabara.

Mheshimiwa Spika, Ili nchi yetu iweze kuwa na ushindani wa Kibiashara katika ukanda wa SADC, EAC, Africa na Dunia kwa ujumla, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo inazingatia yafuatayo;

(i) Kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kuchakata mazao ya mifugo na mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kuyatafutia masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi yetu;

(ii) Serikali ikamilishe haraka uanzishwaji wa masoko ya mipakani ikiwemo kuanza matumizi ya Soko la Mkenda lililopo katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji Mkoa wa Ruvuma (Mpaka huu umesahaulika sana);

(iii) Serikali ianzishe Viwanda vya Dawa na Vifaa tiba kwa ajili ya matumizi yetu na kuuza katika nchi cha SADC, Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla; na

(iv) Serikali ikiwezeshe Kiwanda cha *Biotech Production Limited* kilichopo Kibaha ili kiendelee kuzalisha viluilui wa kuua vijidudu wa mbu wanaoeneza malaria na magonjwa mengine ili kutokomeza kabisa malaria nchini na hivyo kupunguza vifo na gharama kubwa inayotumika kutibu ugonjwa huu.

2.3.5. Sekta ya Ardhi na Mazingira

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu katika kuleta maendeleo. Hivyo kuna umuhimu wa kuzingatia upatikanaji wa ardhi na haki ya kuitumia katika maendeleo. Aidha, takwimu za sasa zinaonyesha kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa **asilimia 3.1** kila mwaka na hivyo kupelekea mahitaji makubwa ya ardhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji na uwekezaji. Aidha, takribani ya **asilimia 70** ya watu wa Tanzania wanaishi maeneo ya vijijini wanategemea ardhi

katika upatikanaji wa mahitaji yao ya maisha. Hali hii imepelekea kuwa na migogoro mikubwa ya ardhi pamoja na uharibifu mkubwa wa misitu (*Deforestation*) na vyanzo vya maji (*source of water*).

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa Mpango tunaotekeleza sasa haujaweza kusaidia katika kutatua matatizo yanayohusu ardhi na usimamizi wa mazingira. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kuna kuwepo mipango ya matumizi bora ya ardhi, uhifadhi wa mazingira na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hata hivyo nguvu zaidi inahitajika ili kuendana na kasi ya ongezeko la watu ambao hadi mwaka 2019 wamefikia takribani watu milioni 55.9. Serikali lazima ihakikishe utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa upande wa vijiji, wilaya na mkoa unakamilika haraka, pia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya utatuzi wa migogoro ya ardhi yanatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, kwa upande wa mazingira, Serikali ihakikishe inaendeleza juhudi za kuhamasisha utunzaji wa mazingira ikiwa pamoja na kusimamia programu na sera za usimamizi wa mazingira, mafunzo ya uchambuzi na athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

2.3.6. Sekta Utalii

Mheshimiwa Spika, Tanzania ndio nchi pekee duniani ambayo imetenga eneo lake kubwa kiasi cha asilimia 25 kwa ajili shughuli za kuhifadhi na kuendeleza shughuli za utalii kama vile hifadhi ya Taifa, maeneo tengefu na maeneo ya uhifadhi. Aidha sekta hii imeendelea kufanya vizuri katika kuchangia Pato la Taifa (asilimia 17.7) pamoja na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nje (asilimia 24). Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inaona kuwa juhudi mahususi zinahitajika ili tuweze kufikisha malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa upande wa kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni 1.7 na Mchango katika Pato la Taifa kufikia asilimia 18.3. haya yote yanaweza kufikiwa kwa :-

i. Kuendelea kuhamasisha na kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi;

- ii. kuongeza bidhaa za huduma na utalii pamoja na kuendelea kuaninisha maeneo mapya ya utalii;
- iii. kuboresha miundombinu katika hifadhi za taifa, maeneo tengefu na maeneo ya uhifadhi; na
- iv. Kuendelea kuboresha mafunzo yanayotolewa na vyo vya utalii.

2.3.7. Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 Sekta ya madini imekuwa kwa wastani wa **asilimia 8.0** na kuchangia Pato la Taifa kwa **asilimia 5.2** mwaka 2019/20 kutoka **asilimia 4.6** kwa mwaka 2015/16 na hivyo kufikia malengo tuliojiwekea kwenye Mpango wa Pili wa Taifa. Aidha mapato ya fedha kigeni kutoka kwenye mauzo ya madini yameongezeka kutoka **Dola za Kimarekani milioni 1,912 (trilioni 4.46)** kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia **Dola za Kimarekani Milioni 2,898.8 (trilioni 6.76)** mwaka 2019/20.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali imefanikiwa kulipa fidia katika eneo linalotakiwa kujengwa kiwanda cha ubia cha kubadilisha gesi asilia iwe katika hali ya kimiminika (LNG). Kamati inaishauri Serikali kukamilisha kwa haraka majadiliano na wabia walioonyesha nia ya kuwekeza katika mradi huu ambao ni wa muda mrefu. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya usambazaji wa gesi asilia viwandani ili kupunguza gharama za uzalishaji na kupunguza matumizi ya mkaa majumbani.

Mheshimiwa Spika, hatua hii nzuri imefikiwa baada ya kuwepo na ushiriki wa Serikali katika Tasmania ya uchimbaji wa madini uliochangiwa na mabadiliko makubwa ya sheria zinazosimamia uchimbaji wa madini kama vile Sheria ya Madini, 2017 (The Minerals Act, 2017), Sheria ya Mamlaka ya Kudumu ya Tanzania juu ya Rasilimali na Utajiri wa Nchi (Natural Resources (Permanent Sovereignty) Act of 2017, Tamko la Uanzishwaji wa Mashirika ya Umma (The Public Corporations(establishment Amendment) Order, 2015) na Sheria ya Mafuta (The Petroleum Act of 2015). Hatua hii pia,

imetoa mamlaka kwa shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) kushiriki katika biashara za madini na nishati hapa nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri hasa pamoja na ile ya kuanzishwa kwa Kampuni Mpya Twiga Minerals Corporation inayomikiwa kwa ubia kati ya Tanzania (Hisa **asilimia 16**) na Kampuni ya Barrick (Hisa **asilimia 84**) ambapo imetoa gawio la shilingi Bllioni 100. Pia, kuanzishwa kwa kampuni mpya ya Tembo Nickel Corporations Limited ambapo Tanzania ina hisa ya umiliki wa **asilimia 16**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hii nzuri ni wakati wa mashirika ya STAMICO na TPDC kuhakikisha yanafanya biashara na kupata faida na kutoa gawio linalostahili kwa Serikali na hivyo kuchangia Mapato. Aidha, bado kunahitajika upatikanaji wa takwimu sahihi za mapato yatokanayo na shughuli za uzalishaji wa gesi pamoja na makinikia yake.

2.3.8. Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu

2.3.8.1. Afya

Mheshimiwa Spika, Serikali imepiga hatua kubwa katika kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini kwa kujenga zahanati, vituo vya Afya na Hospitali nyingi katika maeneo yote nchini. Serikali pia imeweza kuongeza idadi ya Watoa huduma wa afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano imepungua kutoka 67 kila vizazi 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 50 katika kila vizazi 1,000 mwaka 2019/20 hata hivyo ikiwa chini ya lengo la kufikia vifo 45 tu, Idadi Vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua ilipungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 321/100,000 mwaka 2020 hii ikiwa ni chini ya lengo la kufikia vifo 250 tu iliyowekwa kufikiwa katika Mpango wa Pili ifikapo mwaka 2021. Serikali pia imeongeza upatikanaji wa mashine za kisasa za kupima ugonjwa wa kifua kikuu (TB) (GeneXpert) kutoka 65 mwaka 2015/16 hadi mashine 239 mwaka 2020 (Machi, 2020), vifo vya malaria vimepungua kutoka watu 6,311 mwaka 2015 hadi 2,079 mwaka 2020 (Machi, 2020).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto za upatikanaji wa vifaa tiba vya kutosha kama vile X-Ray machines, MRI, Mashine ya kutibu saratani (Chemotherapy) katika baadhi ya Hospitali na Taasisi za Afya kama vile Ocean Road Cancer Institute, Hospitali za Rufaa na Hospitali za Mikoa. Aidha, bado kuna changamoto katika usambazaji na usimamizi wa dawa na vifaa tiba katika hospitali zetu nchini pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya zahanati na vituo vya Afya katika baadhi ya maeneo nchini ambayo yalijengwa kwa nguvu za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua madhubuti na zinazoendana na mazingira ya nchi yetu katika kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19. Hatua hizi madhubuti zimewezesha nchi yetu kutopata athari kubwa za kiuchumi kwa kuruhusu wananchi kuendelea kufanya shughuli zao za kila siku. Msisitizo ukiwa ni kufuata maelekezo yote yanayotolewa na Serikali na Wataalamu wa Afya ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya kuridhisha yaliyopatikana katika Sekta ya Afya, Kamati ingependa kutoa maoni yafuatayo ili Serikali iyazingatie wakati wa kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo;

i. Serikali ikamilishe haraka ujenzi wa Maboma ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali ambazo bado ni maboma na kuzipatia watumishi, dawa na vifaa tiba;

ii. Serikali itenge fedha za kutosha kwa bohari kuu ya madawa (MSD) ili iweze kusambaza dawa na vifaa tiba nchini pamoja na kuiwezesha kusambaza dawa na vifaa tiba katika nchi za SADC na hivyo kujiongezea mapato;

iii. Serikali ihakiki madeni ya MSD na ifanye utaratibu wa kuyalipa ili iweze kuendelea kusambaza dawa na vifaa tiba;

iv. Pamoja na kupambana na ugonjwa wa Covid-19, Serikali iendeele kutilia mkazo katika kupambana na magonjwa

mengine hasa Malaria na Kansa magonjwa ambayo yanachangia sana katika idadi ya vifo nchini; na

v. Serikali itekeleze agizo la Mheshimiwa Rais la kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kununua dawa inayozalishwa na kiwanda cha Biotech Production Limited kwa ajili ya kuua viluilui wanaoua vijidudu wanaoeneza malaria pamoja na magonjwa mengine kama Dengue, Zika, Matende, Homa ya Manjano (Yellow Fever), Chikungunya na Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley)

2.3.8.2. Elimu

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa, Serikali imepiga hatua kubwa katika kuboresha elimu nchini kwa kuongeza uandikishwaji wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari baada ya kupitisha Sera ya Elimu bila Malipo. Takwimu zinaonyesha kuwa kwa upande wa shule za msingi udahili (Gross Enrollment Ratio) umeongezeka kutoka **asilimia 91.3** kwa mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 110.3** kwa mwaka 2019. Kwa upande wa shule za sekondari (O-level) udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka **asilimia 36** mwaka 2016 hadi kufikia **asilimia 43.9** mwaka 2020. Aidha, sambamba na udahili, Serikali imeweza kuongeza ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara, nyumba za walimu, utengenezaji wa madawati na kupunguza uhaba wa vitabu katika Shule za Msingi na Sekondari. Pia Serikali imeweza kuongeza idadi kubwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015/16 hadi wanafunzi 132,392 mwaka 2020. Pamoja na mafanikio haya, changamoto iliyopo ni kuona kwa namna gani mikopo ya elimu ya juu itapatikana kwa wanafunzi wote wanaomaliza elimu ya sekondari ili waweze kuendelea elimu ya chuo kikuu. Aidha, bado kuna mahitaji ya walimu wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu ili kuweza kukidhi utolewaji bora wa elimu kwa wanafunzi wanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa hamasisha na kujenga vyuo vya ufundi stadi kwa lengo la kutoa elimu itayowawezesha wahitimu kujajiri

wenyewe hasa katika maeneo yanayohusu mafundi mchundo, maafisa ugani, stadi za mikono na ujasiliamali.

2.3.8.3. Maji

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwekeza kwenye maendeleo ya rasilimali maji na kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa gharama nafuu. Hata hivyo pamoja na juhudi hizi bado hatujaweza kufikia malengo ya Mpango wa Pili ya kutoa huduma ya maji safi na salama kwa **asilimia 80** kwenye maeneo ya vijijini na **asilimia 90** kwenye maeneo ya mijini. Takwimu zinaonyesha kuwa hali upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka kutoka **asilimia 47** mwaka 2015 hadi **asilimia 70.1** mwaka 2020 na mijini imeongezeka kutoka **asilimia 74** mwaka 2015 hadi **asilimia 84** mwaka 2020. Hivyo Serikali inahitajika kufanya juhudi zaidi za kuhakikisha kuwa malengo ya Mpango wa Tatu kwenye miradi ya maji yanafikiwa ikiwa pamoja na kuongeza usimamizi wa miradi ya maji hususan kwenye Halmashauri zetu nchini. Aidha, wizara ya Maji iendelee kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji kwa kiwango kinachotakiwa na kwa utaalum madhubuti ikiwa ni pamoja na:-

- i. Kulinda vyanzo vya maji vilivyopo kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji;
- ii. Kuweka mizania sahihi ya mgao wa fedha za mfuko wa maji vijijini na mijini; na
- iii. Kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maji vijijini ili kuhakikisha kwamba inakuwa na tija iliyokusudiwa.

2.3.8.4. Mapitio ya Sera ya Kuondoa Umaskini

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya hatua kubwa ya kupiga maendeleo ni kuona kwa namna gani ukuaji wa uchumi unasaidia kuondoa umaskini wa kipato. Takwimu zinaonyesha kuwa viashiria vya umaskini yaani; umaskini wa kipato (umaskini wa mahitaji ya msingi), pengo la umaskini; na tofauti ya kipato utagundua kuwa bado jamii ya wanaoishi vijijini ndio imeendelea kuathirika na viashiria vya umaskini. Mfano,

takwimu zinaonyesha kuwa umaskini wa msingi (**income poverty**) kwa Dar es Salaam ni **asilimia 8**, maeneo mengine ya mijini ni **asilimia 15.8** na maeneo ya vijijini ni **asilimia 31.3**; aidha, pengo la umaskini (**poverty gap**) kwa Dar es Salaam ni **asilimia 2**, maeneo mengine ya mijini ni **asilimia 3.5** na vijijini ni **asilimia 7.4**; na kwa upande wa tofauti ya kipato (**poverty inequalities**) imeendelea kuwa kubwa kati ya jamii inayoishi mjini na ile ya vijijini. Kwa takwimu hizi utaona bado ukuaji wa uchumi wetu unahitajika kutatua tatizo la umaskini hasa kwa jamii ya vijijini. Ni mategemeo ya Kamati kuwa ukuaji wa uchumi uliosababisha Tanzania kuwa Nchi ya kipato cha kati (middle-income-country) utasaidia kuimarisha Pato la Mtu hasa kwa jamii ya vijijini. Hatua hii inaweza kufikiwa ikiwa Serikali itahakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unabebwa zaidi na sekta zinazohusisha idadi kubwa ya watu mathalani sekta ya kilimo na viwanda ili ukuaji huu uweze kutiririka na kuwafikia wananchi walio wengi vijijini. Kwa hali ilivyo sasa ukuaji wetu wa uchumi unategemea sekta za ujenzi, mawasiliano, na huduma za fedha n.k ambazo zinajumuisha idadi mdogo ya watu na pia shughuli nyingi za sekta hizi zinafanyika katika maeneo ya mijini tu ambapo kuna idadi ndogo ya watu

3.0. MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22- 2025/26)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua kwa kina mapendekezo ya Muundo wa Mpango wa Tatu Maendeleo wa Taifa (2021/22-2025/26) wenye dhima ya ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***. Uchambuzi wa Kamati umejielekeza kwenye maeneo ambayo hayakufanya vizuri kwenye Mpango wa Pili na nini kifanyike kwenye Mpango huu wa Tatu; uzingatiaji wa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 tuliojiwekea; Mpango Mkakati wa Maendeleo wa muda Mrefu (Long Term Perspective Plan), Hotuba ya Rais alipokuwa akizindua Bunge la 12 pamoja na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025. Hivyo ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itazingatia maoni na ushauri huu wakati wa maboresho ya Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa

3.1. Malengo na Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kuchambua Mpango huu ambao umeainisha maeneo makuu yafuatayo;

- i) kuchochea uchumi shindani na shirikishi;
- ii) kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma;
- iii) kukuza biashara
- iv) kuchochea maendeleo ya watu; na
- v) Kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuainisha maeneo haya, jambo la msingi ni kuona Mpango huu unatimiza shabaha zake zilizoainishwa ifikapo mwaka 2026 hasa katika upande wa ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 8, sekta binafsi kuzalisha ajira milioni nane na akiba ya fedha ya kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Aidha, mpango huu pia ujelekeze kujibu changamoto zilizosababisha kutofikiwa kwa baadhi ya malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo.

3.2. Uchambuzi na Vyanzo vya Mapato vya ugharamiaji wa Mpango

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya mpango wa Tatu wa Maendeleo kwa kiasi kikubwa utategemea upatikanaji wa rasilimali fedha na usimamizi wa matumizi ya fedha. Ugharamiaji wa mpango umegawanyika katika vyanzo vikuu vitatu; **kwanza**, mapato kutoka Serikali kuu yatakatokana na mapato ya kodi, yasio ya kodi; **Pili**, Mikopo (ndani na nje); **Tatu**; Sekta Binafsi kutoka ndani na ile inayotokana na uwekezaji kutoka nje (Foreign Direct Investment). Mpango huu utagharimu kiasi cha shilingi **trilioni 114.8** ukilinganisha na shilingi **trilioni 107** zilizotarajiwa kugharamia Mpango wa Pili (**Ongzeko la trilioni 7.8**). Kati ya fedha hizo, Serikali itatoa

kiasi cha shilingi **trilioni 74.2 (Ongezeko la trilioni 15.2)** ikiwa sawa na kuchangia **trilioni 14.84** kila mwaka; na sekta binafsi itatoa kiasi cha shilingi **trilioni 40.6 (pungufu ya shilingi trilioni 4)** katika kugharamia utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu inayotufanya tusifikie malengo ya mpango ni kutopatikana kwa rasilimali fedha za kutosha na kwa wakati kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mpango. Tathmini inaonyesha kuwa bado fedha zilizotengwa kwenye utekelezaji wa Mpango wa Pili zilikuwa chini ya lengo na wakati mwingine fedha zilizotengwa hazikuelekezwa kwenye maeneo ya kipaumbele cha Mpango. Hivyo, Kamati inaona kuwa Serikali iongeze juhudi za upatikanaji wa fedha za ziada za ugharamiaji wa miradi ya maendeleo ukizingatia kwa upande wa sekta binafsi kiwango kimeshuka kwa kiasi cha **trilioni 4** na kwa Serikali kimeongezeka kwa **trilioni 15.2**. Hivyo, ni vema Mpango huu wa Tatu ukajielekeza kutatua changamoto za upatikanaji wa fedha za kugharamia Mpango ili kufikia malengo na shabaha tuliyojiwekea.

Jedwali Na. 1: Ugharamiaji wa Mpango wa Pili ukilinganisha na Mpango wa Tatu

(Trilioni)

Na.	Bajeti	Serikali	Sekta Binafsi	Jumla ya Bajeti yote
1.	Jumla ya Fedha zilizotengwa kugharamia Mpango wa Pili 2016/17 -2020/21	59	48	107
2	Jumla ya Fedha zilizotengwa kugharamia Mpango wa Tatu 2021/22 -2025/26	74.2	40.6	114.85
3	Asilimia Ongezeko/Punguzo	25.8	(8.8)	6.7

3.3. Upatikanaji wa Mapato na Mwenendo wake

Mheshimiwa Spika, Mpango huu utagharamiwa na mapato yatakayotokana na mapato ya kodi, yasio ya kodi pamoja na Mikopo (ndani na nje). Hivyo, Serikali ijielekeze katika kuhakikisha kodi, ada na tozo zinalipwa pamoja na kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuweza kupata kiasi cha **trilioni 14.84** kila mwaka. Aidha, mwenendo wa upatikanaji wa

Mikopo yenye masharti nafuu na misaada unaonyesha kushuka kutoka mikopo ya **shilingi trilioni 1.75** mwaka 2021/22 hadi kufikia **shilingi trilioni 1.596** mwaka 2025/26; Na misaada kutoka **shilingi trilioni 1.12** mwaka 2021/22 hadi kufikia **shilingi milioni 520,261**. Hali hii inaashiria kuwa *''W Tanzania lazima tulipe kodi kwa maendeleo ya Taifa letu''*

Jedwali Na. 2. Baadhi ya vyanzo vya mapato na mwenendo wake

Mwaka	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Mapato ya Kodi	22,097,676	24,104,998	26,269,832	28,574,140	30,658,286
Mapato yasio ya Kodi	3,071,042	3,192,899	3,606,752	3,885,388	4,299,588
Mapato ya Halmashauri	863,858	917,022	975,558	1,043,847	1,101,700
Misaada	1,127,188	959,108	865,416	745,557	520,261
Mikopo ya Masharti nafuu	1,757,802	1,706,574	1,663,106	1,627,871	1,596,144
Mikopo ya Biashara	2,352,107	2,421,900	1,840,650	1,745,450	1,646,775

Chanzo: Wizara ya fedha namipango

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iendeleo kuchukua hatua madhubuti ya kuziba mianya ya ukwepaji kodi ili kukahikikisha uhakika wa ukusanyaji wa mapato ikiwa pamoja na kuongeza wigo wa mapato. Vyanzo vingine vya mapato ambavyo Serikali inaweza kutumia ni mifuko maalum ya serikali, mikopo maalum ya maendeleo, hati fungani za miundombinu na mapato yatokanayo na sekta ya madini mafuta na gesi.

3.4. Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati (Flagship Project).

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Tatu umejielekeza kukamilisha miradi ya kimkakati na kipaumbele ili kuhakikisha tunafikia malengo na shabaha ifikapo mwaka 2026. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza kwa kiwango kikubwa miradi ya Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji-Julius Nyerere MW 2,115; Uboreshaji wa Shirika la Ndege na kuendelea miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja; Ununuzi wa Meli; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere; Mnazi Bay kaskazini na ziwa Tanganyika; na kuendelea na mchakato wa kutekeleza mradi wa Ujenzi wa

Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua kubwa iliyofikiwa katika kupeleka umeme vijijini kupitia mpango wa usambazaji umeme vijijini (REA). Hata hivyo, Mpango huu wa Tatu ujielekeze zaidi kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme kwenye vitongoji na mitaa na maeneo yanayokua kwa kasi ili kuwafikia wananchi wengi pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo vya uchakataji wa mazao vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu ujielekeze katika kuondoa urasimu wa utekelezaji wa miradi ya maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ/SEZ) hasa kwa upande wa kukamilika mikataba na ulipaji wa fidia mfano mradi wa bagamoyo, eneo la uwekezaji kigoma, Mtwara na mengine. Pia bado kuna uendelezaji hafifu wa maeneo ya Kanda maalumu za uwekezaji katika maeneo ya Dodoma, Ruvuma, Manyara, Mara, Manyoni na Tanga.

3.5. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufadhili miradi ya maendeleo.

Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi kuwekeza. Ushiriki wa Sekta binafsi katika miradi ya maendeleo unapunguza gharama ya Serikali katika kugharamia miradi ya maendeleo na pia inachochea kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi. Hata hivyo sekta binafsi bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali hasa zinazohusu maeneo yafuatayo:-

i) Uwingi wa mamlaka za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi;

ii) Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi;

iii) Uwingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja;

iv) Kuboresha mazingira ufanyaji wa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hizi ni baadhi tu ya changamoto zinazoikabili sekta binafsi katika ushiriki wa miradi ya maendeleo. Hivyo kuna umuhimu kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo kujielekeza kutatua changamoto hizi ikiwa pamoja na kuhuisha mwongozo wa ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini (Blue Print) kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa inayohusu biashara na uwekezaji. Aidha Muswada wa Sheria ya uwezeshaji wa Biashara (Business facilitation Act) uwasilishwe Bungeni haraka ili uweze kusaidia kutatua changamoto hizi.

3.6. Sekta za Huduma ya Elimu na Afya

Mheshimiwa Spika, Kama nilivyokwisha sema awali kwamba mpango huu una dhima ya *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*. Hivyo ni wazi huwezi kuongelea maendeleo ya watu bila kutaja sekta za elimu, maji na Afya japo sekta zote za miundombinu na biashara nazo zina lenga maisha ya watu ila sekta hizi ni msingi kwa maendeleo ya watu.

3.6.1. Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa mpango wa pili limeonekana ombwe katika sekta yetu ya Elimu ambayo imeonekana kuzalisha wataalamu wasio endana na mahitaji ya soko. Hii imesababishwa na mambo makuu matatu; **Kwanza**, ni mabadiliko ya uchumi wa Taifa na Dunia ambao unaenda kwenye mageuzi ya nne ya Viwanda (*Fourth Industrial Revolution “Digital Economy”*); **Pili**, ni uwekezaji mdogo kwenye elimu za Ufundi; na **Tatu**, ni mitaala yetu kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapungufu hayo Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya haraka ya mitaala yetu kabla ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mpango haujaisha na kufanya uwekezaji mkubwa katika vyuo vya ufundi na veta ili maendeleo ya viwanda yaendane na ujuzi. Aidha, kamati inaishauri serikali kufanya uwekezaji wa haraka katika miundombinu ya shule kwa sababu hivi sasa shue nyingi

zimezidiwa kutokana na Sera njema kabisa ya Serikali ya awamu ya Tano ikiongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Elimu bila Ada "Free fee Education".

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna umuhimu wa kutathmini Mfumo na Mitaala ya Elimu yetu (Education Structure and Curriculum) ili kuona kama inaleta tija tunayoitegemea katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. Ni lazima tufanye tathmini ili kuona je tunahitaji kuendelea kuongeza Idadi ya Vyuo Vikuu nchini na kuongeza Idadi kubwa ya wahitimu wa vyuo vikuu katika fani nyingi zaidi au tunahitaji kubadili mtazamo na uelekeo kwa kuwekeza zaidi katika Elimu ya kati ya ufundi stadi ili kuweza kupata wataalamu watakaoweza kujajiri wenyewe na wengine watakaotumika katika viwanda vyetu ambavyo vingi vipo katika kundi la viwanda vidogo na viwanda vidogo sana. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini hii haraka, ili tunapoanza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa 2021/22 – 2025/26 tuanze tukijielekeza katika mtazano mpya wenye lengo la kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kukuza biashara na kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wanufaika wa mikopo ya Elimu ya Juu kwamba Riba ya mikopo hii ipo juu sana na kiwango wanachokatwa kila mwezi ni kikubwa sana. Kamati inaishauri Serikali irejee upya viwango hivyo.

3.6.2. Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha kwa kasi Hospital za kanda za Rufaa, Mikoa, Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya. Katika Mpango huu wa Tatu, kama viashiria na malengo yaliyowekwa yatafikiwa basi nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa katika kuimarisha utolewaji wa huduma ya Afya. Aidha, kasi hii iendane pia na ununuzi wa madawa na vifaa tiba, kuongeza watumishi wa afya kulingana na mahitaji, kuweka mkakati maalumu wa kupambana na magonjwa

mbalimbali hasa yale yasiyo ambukiza ambayo matibabu yake yameendelea kuwa ya gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mpango huu wa Tatu ujielekeze katika kuhakikisha kuwa majengo yote ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali yaliyoanza kujengwa (Maboma) yakamilishwe na kupatiwa vifaa tiba na watumishi kabla ya kuanza ujenzi mpya.

3.7. Tathmini, Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Mpango wa Tatu imeonyesha kwamba Serikali inakusudia kutumia Nyanja zote za utawala katika kusimamia utekelezaji. Hata hivyo kamati imebaini kwamba utaratibu uliopendekezwa haukufanya vizuri katika Mpango wa Pili kwa sababu hakukuwa na rasilimali za kutosha za usimamizi na ufuatiliaji na vilevile utembelezaji wa miradi haukufanyika kikamilifu. Tatizo hili linaweza kuwa kubwa kwa upande wa miradi inayotekelezwa na utaratibu wa *Force Account* ambapo hakuna fedha yoyote inatengwa ya tathmini na ufatiliaji hivyo inaweza kusababisha tukawa na miradi mingi ambayo imetekelezwa kwa kiwango cha chini

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa mpango ni jambo muhimu sana ili kujua wapi tumetoka, wapi tulipo na wapi tuendako na hivyo kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa. Katika Mpango huu wa Tatu, Kamati inaishauri Serikali ijikite zaidi katika mambo yafuatayo:-

i) Serikali ihakikishe kunakuwepo na upatikanaji wa taarifa endelevu za utekelezaji (miradi na bajeti) dhidi ya hatua au malengo ya mpango;

ii) Serikali iweke utaratibu maalumu wa kuchanganua kwa kina taarifa za utekelezaji wa miradi zitakazokuwa zinawasilishwa kwa kila kipindi maalumu cha utekelezaji. Hatua hii, itasaidia kujua hatua inayofikiwa kwa kila mradi husika;

iii) Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zitoe takwimu sahihi za utekelezaji wa miradi ili kusaidia ufanyaji wa tathimini kwa ufanisi;

iv) Serikali ihakikishe inatekeleza Mpango huu kulingana na Sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA (2021/22-2025/26)

4.1. Uanzishaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi

Mheshimiwa Spika, kimsingi Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano umejielekeza katika kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazoweza kushindana kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa hizo ndani na nje ya nchi. Lengo likiwa na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini pamoja na kuongeza uuzaji wa bidhaa shindani nje ya nchi. Kamati inaona kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunaanza na viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazotumia malighafi zinazopatikana nchini.

4.2. Sekta ya Ujenzi

Mheshimiwa Spika, Miradi mingi mikubwa ya maendeleo imekuwa ikitekelezwa na makampuni ya nje na sababu zilizotajwa ni makampuni ya ndani kukosa mtaji na kutokuwa na uwezo wa kutekeleza miradi husika ambayo hufadhiliwa kwa fedha za nje. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango mizuri ya kusaidia makampuni ya ndani kuweza kuwa shindani, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, utoaji wa vivutio vya kikodi kwenye mitambo inayotumika na vifaa vya ujenzi. Matumizi ya wakandarasi wa ndani badala ya wakandarasi wa nje yatainufaisha nchi kiuchumi kwa kuwezesha fedha kubaki nchini na kuchochea uwekezaji na uzalishaji na kuongeza mzunguko wa fedha.

4.3. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Miundombinu suala la msingi la kuzingatia ni kuhakikisha kwamba miundombinu ya

msingi inajengwa katika maeneo ya kimkakati ili Taifa linufaike na fursa na nafasi yake kijiografia (*Strategic Geographical Location*) ya kuzungukwa na kuhudumia nchi 6 zisizo na bandari (*landlocked countries*). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati mahsusi kutekeleza yafuatayo kwa kuzingatia malengo ya Mipango ya Maendeleo yaliyowekwa:-

a) Kuanzisha na kukamilisha ujenzi wa barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za mijini na vijijini zenye jumla ya urefu wa km 8,506.

b) Kugharamia uboreshaji wa miundombinu ya Reli ya TAZARA na Reli ya Kati kwa vipande vilivyobaki ili reli hizo ziwe na manufaa ya uchumi wa usafirishaji.

c) Kupanua na kuboresha Bandari za Tanga na Mtwara, na Bandari za ndani za Mwanza, Kigoma na Itungi.

d) Ununuzi wa haraka wa *Cranes* na *Converyer Belt* kwa ajili ya kupakia na kushusha shehena za mizigo kwenye Gati za Bandari ya Dar es salaam zilizokamilika. Ni vema zikanunuliwa haraka kwa sababu hivi sasa kazi kubwa inafanywa na Kampuni ya binafsi kwa gharama kubwa.

4.4. Ukarabati na ujenzi wa Viwanja vya Ndege

Mheshimiwa Spika, Kasi ya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege nchini haiendani na kasi ya ununuzi wa ndege hali ambayo inaweza kusababisha kupungua wa miruko ya ndege (*few flight routes*) husika na hatimaye kullitea hasara kubwa za kiuendeshaji Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Aidha, imedhihirika kwamba uwepo wa changamoto za kiusalama duniani kama vile milipuko ya magonjwa (Mfano COVID-19) husababisha safari za ndani za ndege ziwe na faida kuliko safari za nje. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege unaohusisha ujenzi, upanuzi na uboreshaji barabara za lami za ndege (*airport runways*) na uwekaji wa mifumo ya taa za kuongozea ndege (*aeronautical ground lighting systems*)

ambazo zinaruhusu shughuli za viwanja wa ndege kuendelea kwa masaa 24.

4.5. Mzingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoiwezesha Sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, na viwanja vya ndege), kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuanzisha maeneo ya uwekezaji, kuweka sheria za fedha na kanuni zinazotabirika na kutekeleza mipango mbalimbali kama *ROAD map for improving Bussiness Enviroment Strengthening in Tanzania (BEST na Blue Print)*. Pamoja na juhudi hizo, Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji, Tanzania imeendelea kushuka kutoka nafasi ya 131 mwaka 2015 hadi 141 mwaka 2020 tofauti na lengo tulilojiwekea la kuwa wa 100 kati ya nchi 189 duniani katika jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kubainisha maeneo (indicators) ambayo nchi haifanyi vizuri na kuweka mikakati madhubiti ya kuboresha maeneo husika. Mikakati hiyo ihusishe pia namna bora ya kuunganisha mamlaka za udhibiti (Regulatory Authorities) chini ya **Regulatory Ombudsman** ambazo zinafanya majukumu yanayoshabihiana, pamoja na Wizara ya Fedha kukamilisha uanzishaji wa **Office of Tax Ombudsman** itakayoshughulikia malalamiko kuhusu kodi na ushuru suala ambalo ni muhimu katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

4.6. Ushirikishwaji wa Watanzania katika Miradi ya Maendeleo na Uwekezaji nchini (Local Content)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuweka sera na kutunga sheria mbalimbali kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa watanzania katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uwekezaji nchini kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi. Changamoto kubwa iliyopo ambayo hata Mipango ya Maendeleo ya Taifa haujaweza

kutanzua kikamilifu ni kubainisha ushirikishwaji wa watanzania (local content) katika kila sekta badala ya kitaifa. Kamati inaona ni vema Serikali ikaliweka suala la Ushirikishwaji wa Wananchi wote kwenye shughuli za kiuchumi kwenye Sheria na Sera moja ya Ushirikishwaji au Uwezeshaji wa Wananchi ili iwe rahisi kusimamia, kufuatilia pamoja na sekta zote kuwajibika kwenye Sheria moja tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo hata ufuatiliaji unakuwa mgumu.

4.7. Uzingatiaji wa Mapinduzi ya Kidijiti (Digital revolution) katika Mipango ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Mapinduzi ya kidijiti (*Digitalization*) yamesababisha pamoja na mambo mengine wananchi kufanya miamala ya kibiashara na kiuwekezaji kwa kutumia mitandao mbalimbali hususani mitandao ya simu, mitandao ya taasisi za fedha na kibenki na mitandao ya taasisi za serikali. Matumizi ya mitandao yamesababisha changamoto za ukwepaji wa kodi na utakatishaji wa fedha zilizopatikana kwa njia zisizo halali. Makampuni mengi ya kigeni na hata ya wazawa yamekuwa yakikwepa kodi kubwa kwa kutotoa takwimu sahihi za faida inayopatikana au kuhamisha faida kwa kampuni tanzu (*BEPS- Base Erosion and Profit Shifting*). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali wakati tukiendelea kuboresha mifumo ya kieletroniki na matumizi ya mtandao katika kutekeleza shughuli za serikali na za sekta binafsi, ni vema tukaweka mikakati madhubuti (*National Digitization Strategy*) ya kutumia fursa na kuzuia athari za matumizi ya mtandao hasa za kimapato na kiusalama pamoja na kuwapa mafunzo ya kidijiti wataalamu wetu

4.8. Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Bahari Kuu

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza mchakato wa kuandaa mkakati wa taifa wa uchumi wa bluu na kuipa uzito sula la uvuvi wa bahari kuu kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano awamu ya Tatu ili kuwa na uendelevu wa ukusanyaji wa mauzo nje ya nchi. Aidha, kutokana na ukubwa wa sekta hii na *complexity* ni vema Sekta Binafsi na watalaam wenye uzoefu wa eneo hili kushirikishwa kwa upana wake ili hatimaye kuleta mafanikio

yanayotokana na sekta hii hasa ukizingatia soko kubwa la mazao ya baharini duniani.

4.9. Maboresho katika kituo cha uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilianzishwa ili kuratibu, kuhamasisha, kukuza na kuwezesha uwekezaji nchini Tanzania na kuishauri Serikali juu ya sera ya uwekezaji na mambo mengine yanayohusiana na uwekezaji nchini. Kimsingi, TIC ilianzishwa ili iwe *One-Stop Shop* kwa ajili ya kusaidia na kuharakisha uwekezaji nchini. Kamati imeelezwa kwamba kwa sasa kwa sehemu kubwa suala ya utoaji wa maamuzi ya uwekezaji nchini limehamishiwa kwa Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka husika na hivyo kusababisha kuongezeka kwa urasimu katika sekta ya uwekezaji. Mfano mzuri Kituo cha Uwekezaji ambacho kinafanya kazi kwa ufanisi kama *One-Stop Shop* ni *Rwanda Development Board*. Kamati inaona ni muhimu kwa serikali kuliangalia upya suala ya ufanyaji wa maamuzi kuhusu shughuli za uwekezaji na uongezaji tija kwa shughuli za TIC.

5.0. MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.

5.1. Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/22 uliooandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia sera, vipaumbele, mpango mkakati wa Taasisi husika na maelekezo ya Serikali iliyopo wakati wa uandaaji, utekelezaji, uwasilishaji na utoaji taarifa wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kati ya masuala yaliyotiwa mkazo katika Mwongozo ni pamoja na uandaaji wa mipango na bajeti inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha ikiwa ni kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima. Aidha, Maafisa masuuli na mipango wanatakiwa kutumia mifumo ya kielektroniki

Iliyopo ikiwa ni pamoja na mfumo wa uhasibu Serikalini (MUSE), mfumo wa ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao (GePG), mfumo wa uingizaji wa takwimu za Bajeti ya Serikali CBMS na PlanRep.

5.2. Utekelezaji wa Bajeti katika Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya shilingi **trilioni 34.87**. Kiasi hicho kinajumuisha, shilingi **trilioni 22.1** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **trilioni 12.77** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi **bilioni 32.14** ni fedha za ndani na shilingi **trilioni 2.73** ni fedha za nje. Aidha, Serikali ilipanga kukusanya mapato yake ya ndani kiasi cha Shilingi **trilioni 24.065** na kukopa katika vyanzo vya ndani na nje kiasi cha shilingi **trilioni 10.81** ambapo kati ya mikopo hiyo kiasi cha shilingi **trilioni 2.73** ni kutoka nje na shilingi **trilioni 8.08** ni kutoka katika vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 15.84** Hata hivyo kiasi cha fedha kilichokusanywa katika kipindi hicho kutoka vyanzo vya ndani na nje ni shilingi **trilioni 13.85** sawa na **asilimia 87.4** ya makadirio. Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi **trilioni 10.46** sawa na **asilimia 89.0** ya lengo la kukusanya shilingi **trilioni 11.75** Kati ya mapato hayo: mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi **trilioni 9.06** sawa na **asilimia 89.7** ya lengo la kukusanya shilingi **trilioni 10.10**; mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yalikuwa **shilingi trilioni 1.02** sawa na **asilimia 83.6** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 1.22**; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia **shilingi bilioni 376.5** ikiwa ni **asilimia 89.0** ya lengo la kukusanya shilingi **bilioni 422.8**.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo takwimu zinavyoonyesha hapo juu Serikali haikuweza kukusanya kwa asilimia moja (100%) mapato iliyopanga kukusanya katika kipindi hicho cha

nusu mwaka. Kutofikia lengo la makusanya kuliathiri utekelezaji wa baadhi ya shughuli ambazo zilipangwa kutekelezwa katika kipindi husika. Ni maoni ya Kamati kuwa ili Serikali iweze kupunguza ama kuondoa kabisa changamoto hii ya kutofikia malengo ya makusanyo yake ni vema ikafanya yafuatayo;

- i. Kuhamasisha na kuhakikisha matumizi ya Risiti za Kielektroniki;
- ii. Kuboresha utaratibu wa kukusanya Kodi ya Majengo (Property Tax);
- iii. Kuboresha utaratibu wa kukusanya kodi ya ardhi;
- iv. Kuongeza kasi na kuboresha utaratibu wa kurasimisha biashara zisizo rasmi ili ziweze kuingia katika utaratibu wa kulipa kodi stahiki.
- v. Kuandaa Kanzidata ya Biashara zote za Mtandao (database of online businesses) na kusajili na kuzipa TIN biashara zote zinazofanyika katika mtandao;

5.3. Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2021/22 ndio bajeti ya kwanza inayoenda kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Tatu wa Taifa (2021/22-2025/26) uliobeba dhima ya ***“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”***. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22 utajumuisha ukamilishaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati ambayo utekelezaji wake haukukamilika katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa 2021/22 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 36.2** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 4** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21 ya **shilingi trilioni 34.8**. Mapato ya ndani yanatarajia kuwa **shilingi trilioni 26.03** ikiwa ni sawa na **asilimia 72** ya bajeti. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni **shilingi**

trilioni 21.46, mapato yasiyo ya kodi yakijumuisha mapato ya halmashauri, mapato ya utalii na mapato mengine yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 4.56**. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha **shilingi trilioni 10.21** zikiwa ni fedha kutoka Washirika wa Maendeleo, fedha zitakazo kopwa kwenye soko la ndani na mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Mwongozo Serikali katika mwaka 2021/22 haitapokea Misaada ya Kibajeti kupitia utaratibu *General Budget Support* (GBS) kutokana na kufika ukomo wa Mkataba wa Programu ya GBS katika sekta ya Fedha na Uchumi kutoka Jumuiya ya Ulaya iliyojumuisha nchi za Denmark na Sweden. Badala yake fedha hizo zitakuwa zinapelekewa moja kwa moja kwenye Miradi suala ambalo sio preference ya Serikali kwa kuwa yenyewe ndio inayojua mahitaji halisi ya kimaendeleo na utoa fedha hizo kulingana na mahitaji. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kufanya mazungumzo na Washirika na kushawishi kuendelea na utaratibu wa awali wa GBS. Aidha, Serikali iendelee kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuondokana kabisa na utegemezi wa kibajeti ambao hupelekea kuchelewa kukamilika kwa utekelezaji wa miradi au kukwama kabisa. Aidha, msisitizo uelekezwe kwenye kuimarisha mifumo ya tehama katika ukusanyaji mapato kwa Serikali Kuu na Halmshauri, usimamizi madhubuti wa Sheria za Kodi, kuimarisha taarifa za walipa kodi kutoka katika kanzidata mbalimbali na utoaji wa elimu kwa walipa kodi ili kuwa na mapato endelevu pamoja na kuimarisha makusanyo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, eneo la maoteo ya Mapato na Matumizi limekuwa changamoto kubwa kwa nchi. Aidha, katika mwaka 2020/21, Serikali ilianza kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kibajeti hususan katika kukokotoa, kuandaa maoteo ya mapato na matumizi ili kuiwezesha Serikali kuwa na bajeti endelevu ambapo pamoja na mambo mengine tathmini hii itaiwezesha Serikali kubuni vyanzo vipya vya mapato. Aidha, uchambuzi wa kina wa matumizi ya Serikali utafanyika ili kuongeza ufanisi endelevu katika utekelezaji wa bajeti. Ni matumaini ya Kamati kuwa hatua hizi zitazaa

matunda na hatimaye kuikwamua nchi kutoka kwenye utegemezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua inazoendelea kuchukua katika kuimarisha mapato yake na kudhbiti upotevu wa mapato na wakwepaji kodi ambapo mwezi Desemba, 2020 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya kiwango cha juu ambacho hakijawahi kukusanywa cha **shilingi trilioni 2.089**. Hatua hii sio ya kubeza hasa ukizingatia changamoto ya kiulimwengu iliyopo katika kuuwainisha mapato na matumizi ya nchi. Hata hivyo, Serikali imeweza kuongeza mapato yake ya ndani kutoka **shilingi bilioni 850** (2016/17) kwa mwezi iliyokuwa inakusanywa hapo nyuma hadi kufikia wastani wa **shilingi trilioni 1.5** kwa mwezi kinachokusanywa sasa hivi.

6.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imeusoma na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22 yanayotoa mwanga wa jinsi Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021/22 utakavyokuwa katika kuimarisha azma ya **“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”**. Kwa upande wa mwelekeo wa mpango, Serikali imepanga kujikita katika vipaumbele vya kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na kuchochea maendeleo ya watu. Aidha, mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti unatoa taswira ya uandaaji wa mipango na bajeti itakayotumika katika kugharamia maeneo ya vipaumbele vitakavyotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo huu yameainisha maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na maafisa masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala

za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa, kutekeleza, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha vyanzo mbalimbali vya kugharamia mpango wa maendeleo wa mwaka 2021/22 ambavyo jumla vitatoa takribani **shilingi trilioni 13.25**. Hii ni sawa na **asilimia 37** ya bajeti yote. Aidha, Kamati imebaini kuwa bado serikali inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hali inayosababisha kuwepo kwa mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa katika mpango uliopita, pamoja ya kuwa Serikali ilionyesha wapi itapata fedha katika kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo ile ya kitaifa ya kimakakati, bado fedha hizo hazikupatikana kwa wakati uliopangwa au kutofika kabisa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi husika. Kamati inashauri kuwa Serikali ijipange vyema kuhakikisha inasimamia ipasavyo mapato ya ndani, misaada, mikopo pamoja na sekta binafsi ili kuhakikisha inapata kiasi hicho cha fedha za kugharamia mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi mikubwa ya kielelezo, kamati inakubaliana na Serikali kwa kuweka miradi mikubwa kumi na saba (17) ya kielelezo kama kipaumbele kikuu kimojawapo katika mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21. Hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia na kutekeleza kwa mafanikio miradi mikubwa ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya Viwanda, Kamati inaipongeza serikali kwa kupiga hatua katika sekta ya viwanda na hivyo kuongeza fursa za ajira, uzalishaji na mapato. Sekta ya viwanda ni kichocheo muhimu katika maendeleo ya uchumi na ndio iliyobeba dhima ya Mpango

wa Tatu wa maendeleo ya Taifa ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Aidha, Moja ya shabaha ya mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/22 ni Uanzishaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa ndani kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini. Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba tunaanza na bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa kwa kutumia malighafi za ndani. Hivi sasa bidhaa hizo tunaziagiza toka nje kwa kutumia fedha zetu za kigeni. 3

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri serikali kundeleza mikakati mbalimbali ya kupanua sekta za viwanda vidogo vidogo, kuongeza thamani ya bidhaa zetu pamoja na kuongeza mauzo nje. Pia ni muhimu mpango huu ukajielekeza pia katika kufikilia namna mchakato wa ujenzi wa viwanda vipya, kufufua na kukarabati viwanda ambavyo havifanyi vizuri na kufufua vile vilivyokufa

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ujielekeze katika kufungamisha shughuli za kilimo pamoja na shughuli za viwandani. Uzoefu unaonyesha kuwa nchi nyingi duniani zimepiga hatua za uchumi wa viwanda baada ya kupiga hatua katika mapinduzi ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwa pamoja na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaona ni muhimu serikali ikasimamia ipasavyo miradi iliyoainishwa kwenye sekta hizi kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda pamoja na kulinda viwanda vya ndani na hivyo kupata fursa ya kukuza uchumi wetu (Pato la Taifa) na ushindani wa kikanda na kimataifa kupitia sekta husika.

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoiwezesha Sekta binafsi kuwekeza pamoja na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege); kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika; kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji; kuweka sheria za fedha na kodi zinazotabilika (zisisobadilika mara kwa mara); kuhakikisha

kunakuwa na upatikanaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda na sheria bora za ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati thabiti ya utekelezaji wa mradi kituo cha viwanda cha kurasini (Kurasini Logistic Hub) ambacho kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha ushirikano wa kibiashara kati ya Tanzania na Mataifa mengine, kupitia uwekezaji katika miundombinu ya biashara na ujenzi wa viwanda. Hivyo ni vema Serikali ikajikita katika kufuata mipango yake inayojiwekea kila mwaka ili kuwezesha utekelezaji na ukamilishwaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, Mpango huu wa maendeleo wa mwaka 2021/22 ujikite katika kutoa majibu ya changamoto ambazo hazikutatuliwa katika mpango wa maendeleo wa Taifa uliopita wa mwaka 2020/21. Hii itaisaidia serikali kufanya tathimini na ufuatiliaji katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Aidha, Mpango huu ujikite katika kutatua changamoto zilizopo sasa za hali ngumu ya maisha na umaskini wa kipato.

7.0. MAONI YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsusi, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla yafuatayo:-

7.1. Serikali iendeele kutoa kipaumbele stahiki katika nishati mbadala kama vile joto ardhi, umeme wa upepo na umeme wa jua ili kuboresha uzalishaji na usambazaji wa nishati nchini.

7.2. Serikali itatue haraka changamoto ya bei na kuchelewa kufika kwa pembejeo za kilimo katika maeneo mbalimbali, upatikanaji wa mbegu bora za mazao nchini na kuaandaa ramani itakayoonyesha ni mazao yanayoweza kustawi katika kila Wilaya nchini.

7.3. Serikali iainishe Mkakati wa kutafuta masoko ya mazao nje ya nchi kwa kuingia mikataba na wanunuzi au nchi ili ziweze kununua mazao yetu. Balozi zetu ziongeze kasi katika

utafutaji wa masoko ya mazao yanayolimwa hapa nchini na kuuzwa nchi za nje.

7.4. Serikali iweke katika Mpango wake wa Miaka Mitano unaokuja mikakati ya moja kwa moja itakayowezesha zao la korosho na mazao yake (cashnut product and by product) pamoja na mazao mengine ya biashara kuongezewa thamani kwa kutengeneza bidhaa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwaongezea kipato wakulima, wafanyabiashara na Taifa kwa ujumla.

7.5. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ueleze kinagaubaga ni namna gani nchi yetu itavuna manufaa na kukabiliana na changamoto zinazoletwa na uchumi wa kidijiti (*Digital Economy*) huku tukiendelea kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;

7.6. Serikali iendeele kuhamasisha malipo kwa njia ya kielektroniki (electronic payments) na kuandaa Kanzidata ya Biashara zote za Mtandao (database of online businesses) na kusajili na kuzipa TIN biashara zote zinazofanyika.

7.7. Serikali iweke utaratibu mzuri utakaoboresha zaidi ufanyaji kazi wa biashara itokanayo na *Export Processing Zones* (EPZs) ili ilete faida iliyokusudiwa bila kuathiri viwanda na biashara za ndani.

7.8. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha Michezo ya kubahatisha (Gaming Sector) kuendelea kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi pasipo kuleta athari kubwa za kijamii na kitamaduni lakini kwa kuiwezesha iendeele kukua na kuwa endelevu.

7.9. Serikali itatue changamoto zinazojitokeza kwenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

7.10. Serikali itoe Waraka utakaozitaka Ofisi na Taasisi za Umma kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kabla ya kutumia bidhaa za nje. Kwa mfano Taasisi zetu za Polisi, Jeshi

la Wananchi, Idara ya Uhamiaji, Magereza kutumia bidhaa za ngozi (viati, mikanda, mabegi n.k) vinavyozalishwa katika kiwanda cha ngozi cha Karanga, kiwanda kinachomilikiwa na Magereza.

7.11. Mifuko ya Jamii pamoja Taasisi kama vile JWTZ, Jeshi la Magereza zihamasishwe na kuwezeshwa ili ziwekeze katika kujenga Viwanda vya kuongeza thamani Mazao mbalimbali kama vile Parachichi, Michikichi, Korosho na mazao ya korosho (Cashewnut product and by product).

7.12. Kamati inashauri Serikali kutafuta njia ya kupunguza kukopa katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya Bajeti kwa kupitia dhamana ya Serikali na hati fungani. Badala yake Serikali ijikite zaidi katika kuongeza udamini wa wakopaji wadogo (credit gurantee schemes) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenyewe (lease finance). Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi Soko la Mitaji (Liberization of Capital Market) ili kupunguza athari za Serikali kukopa kwenye soko la ndani.

8.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kipekee napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu Fedha, Mawaziri, Manaibu Waziri, Mkatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara na wataalamu wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

- | | |
|---------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |

3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Sillo Daniel Baran (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

08 Februari, 2021

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Sillo Daniel Baran kwa kutupitisha katika maoni ya Kamati hiyo. Kama nilivyowaambia mapema, tayari maoni ya Kamati yamo katika *tablets* zenu na yamechambuliwa vizuri sekta kwa sekta. Niwapongeze Kamati ya Bajeti kwa kukaa kwa saa nyingi kuchambua Mpango wa Maendeleo wa Taifa ule wa Miaka Mitano na huu wa Mwaka Mmoja na mapendekezo yanayoambatana nayo; nawashukuru sana. (*Makofi*)

Kwa sababu ileile ya muda, naomba ukipata nafasi ya kuchangia basi jaribu kwenda moja kwa moja, dakika kumi si nyingi. Tutaanza asubuhi hii na leo jioni tutaendelea tena na uchangiaji wetu kama ilivyo ada. Nina majina mengi kwelikweli lakini basi twende hivyo hivyo kidogo kidogo, wengine watapata nafasi kesho, kesho kutwa tunaendelea. Nina uhakika karibu wote tutapata nafasi ya kuchangia mpango huu ambao ni muhimu sana wa maendeleo ya taifa. Kwa sababu hata ukilaumu baadaye jambo ambalo halikuwa kwenye mpango basi unatwanga maji kwenye kinu. Kwenye mpango ndiyo mahali pa kuhakikisha kwamba mpango unakaa vizuri ili utekelezaji nao uweze kuwa sawasawa.

Kama nilivyokwishaahidi mwanzo, anaanza Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo na atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Jerry Silaa ajiandae. Mheshimiwa Profesa, kwa sababu unaanza basi tutakupa dakika 15. *(Makofi)*

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuanzisha mjadala huu. Nianze kwa kushukuru Wizara kwa kufanya kazi nzuri. Vilevile nimshukuru Rais na timu ya Serikali kwa mipango mizuri waliyotuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango wa Mwaka Mmoja ni sehemu ya Mpango wa Miaka Mitano. Kwa upande wangu niseme kwamba naunga mkono, miradi yote itatekelezwa na hasa ya Jimbo la Musoma Vijijini, ikiwemo na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema na tunavyopaswa kufanya ni kutoa mapendekezo. Kwa hiyo, nianze kwa kusema hivi; kwenye mambo ya uchumi na maendeleo, ukitaka kupunguza umaskini popote duniani, ni lazima uchumi ukue siyo chini ya asilimia 8. Ndiyo maana Ilani yetu ya CCM wale waandishi walikuwa ni wataalam wazuri, tumecheza na asilimia 6 mpaka 7 kwa muda, tumekwenda mbele, lakini wataalam wanasema usiwe chini ya asilimia 8.

Ukitaka kwenda kama China ilivyofanya toka miaka ya themanini mpaka leo hii, ni lazima uchumi wako ukue kwa zaidi ya asilimia 10 na siyo chini ya miaka kumi, ishirini, ndiyo unaweza kuwa nchi yenye kipato kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchango wangu mimi ni namna gani sisi Tanzania tutafanya tuendeleo kuwa nchi ya kipato cha kati. Waheshimiwa Wabunge, kipato cha kati kuna madaraja mule; kuna *lower middle income*, ndimo sisi tumo. Daraja hili maana yake unakuwa na pato ambalo ni kati ya dola 1,026 mpaka dola 4,035. Ndiyo maana Mpango wa Pili ulikuwa unasema Tanzania twende kwenye *GDP per capita* ya Dola 3,000, tulitegemea hivyo kama miaka ya nyuma huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tumeingia tukiwa na Dola 1,122 na sasa hivi tuko watu milioni 60. Tukifika mwaka 2025 tutakuwa watu takriban milioni 70. Sasa tuchukue kwamba pato letu kwa mmoja mmoja, *GDP per capita* iwe ni Dola 1,200. Maana yake tatizo la kubaki kwenye 1,100, uchumi ukitetereka kidogo tu, unaanguka chini, unarudi kuwa kwenye nchi ya kipato cha chini. Ndiyo tatizo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Waheshimiwa Wabunge, tunapaswa kuishauri Serikali tuzidi kwenda mbele. Kwa hiyo, tukiwa na pato la 1,200 kwa watu milioni 70, tunapaswa kuwa na *GDP* ya Dola za Kimarekani bilioni 68, sasa hivi tuko 50. Tukisema tunasogea kidogo ili tubaki pale katikati, twende kwenye *GDP per capita* ya 1,500, ukizidisha kwa 70 tunapaswa Serikali yetu na sisi wote tuwe na *GDP* ambayo iko kwenye Dola za Marekani bilioni 105. Angalia hiyo safari, kutoka *GDP* ya Dola bilioni 50 kwenda 84, kwenda 104, siyo kazi nyepesi, lakini tunaweza kwenda huko. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni tuone tufanyaje ili tuwe na uchumi unaokua kwa zaidi ya 8%. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha kuweka maanani ni kwamba daima; na nashukuru ripoti imeweka maanani kwamba sisi ni sehemu ya hii dunia na kwamba tutaauza bidhaa zetu kwenye Soko la Dunia. Hiyo ni muhimu

sana. Kwenye mambo kama haya ni lazima ujilinganishe na mwenzako. Nami nimechukua nchi mbili tu za kujilinganisha nazo. Nimechukua ya kwanza Kenya ambao ni jirani zetu. Wenyewe *GDP per capita* yao sasa hivi ni Dola 2,075. Kwa hiyo hata wao wakiyumba hawawezi kushuka mpaka Dola 1,025. Mwaka 2025 *GDP* ya Kenya itakuwa Dola 2,593. Lazima tushindane nao, wao wamefanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine niliouchukua ni Seychelles. Nimechukua Seychelles kwa sababu wanaojua historia ya nchi yetu miaka ya 1980, bila Serikali yetu au wanajeshi wetu kwenda Seychelles, hali ilikuwa mabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GDP* ya Seychelles, kwa kifupi, ndiyo ya kwanza kwa Bara zima la Afrika, lakini tuliwasaidia, tuliwapigania, wametuzidi. *GDP per capita* yao sasa hivi ni Dola 12,233. Mwaka 2025 *GDP per capita* yao itakuwa Dola 18,812. Ni kwamba Seychelles itakuwa ni nchi tajiri, itakuwa kwenye *higher income*. *Higher income* ni lazima uvuke *GDP per capita* iende zaidi ya Dola 18,000.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Muhogo, wale hatuwawezi kwa sababu *population* yao hata 300,000 hawafiki.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *GDP per capita* ni suala la hesabu. Ni kama machungwa, ni hesabu, ni *ratio*. Ni *Gross National Income divided by the population*. Kwa hiyo, lazima ulinganishe tu. Hiyo ni hesabu, ni *ratio*. *Ratio* ni *ratio*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, tutafikaje huko na tutabakije huko? Pendekezo langu la kwanza, kama mpango unavyosema, uzito wote tuweke kwenye kilimo. Kwa sababu, kwanza tuna tatizo la ajira, ambalo tutalijibu kupitia kwenye kilimo. Pili, tunahitaji malighafi kwa viwanda vya ndani na vya nje, tutapata kwenye kilimo. Sasa hapo kwenye kilimo tunaendaje? Cha kwanza kabisa, nilimsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, alijibu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Serikali, mahali pa kuanzia pa kwanza ni suala la mbegu. Hili suala la mbegu ni suala ambalo duniani sasa hivi biashara yake ni bilioni 45 dunia nzima. India inajitahidi katika hizo bilioni 45 inachukua mbili. Kwa hiyo, sisi mahitaji ya mbegu lazima tuyatatue na tutayatata kwa kuzalisha mbegu zetu na tutayatata kwa kuwekeza kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi, walioko kwenye sayansi na mambo ya uchumi ya dunia, tumeona uhusiano mzuri uliopo kati ya ukuaji wa uchumi na utafiti unaofanyika ndani ya nchi hiyo. Haiwezekani, haijawahi kutokea, labda iwe kwa miujiza na miujiza huwa ipo kwamba wewe huwekezi kwenye utafiti, ukaja kuitawala hii dunia, haiwezekani! China na Marekani wanapambana kwa ajili ya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, hilo ndiyo pendekezo langu la kwanza kwa upande wa kilimo.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Bado nadhani.

MBUNGE FULANI: Bado sana, endelea.

MWENYEKITI: Bado dakika tano za mwisho.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Ooh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hizo, nimechukua mazao ambayo lazima tuwekeze sana, kwa sababu yanaliwa sana duniani. Tunaweza tukalima kila kitu, lakini tulime mchele ambao zaidi ya asilimia 50 ya watu wote duniani ambao sasa hivi tupo bilioni 7.8 wanatumia mchele kama chakula kikuu (*staple food*). Cha pili ni ngano, nayo ni zaidi ya asilimia 50; cha tatu ni mahindi. Mahindi ni chakula na kwenye viwanda.

Cha nne, nimechagua muhogo kwa sababu una matumizi zaidi ya 100 na unatumika sana viwandani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa pendekezo langu kwa sekta ya kilimo, tuzalishe mazao ambayo wananchi wengi duniani wanayatumia ambayo ni mchele, ngano, mahindi na mihogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kilimo, kwa ajili ya muda, ninachopendekeza ni nishati. Naenda kwenye fedha nyingi, siyo ndogo ndogo. Nishati ni lazima tuzalishe umeme kutoka vyanzo vingi. Vyanzo vyetu sasa hivi ni maji na makaa ya mawe. Tumejenga *transmission lines* za 400KV za kupitisha umeme kwenda Kenya mpaka Ethiopia, kwenda Zambia mpaka soko la SADC huko. Zile *lines* zinaweza kupitisha *Megawati* 2,000 kwa mpigo, kwenda au kurudi. Kwa hiyo, eneo lingine ambalo litatupatia fedha nyingi...

(*Hapa Mhe. Hussein M. Bashe alikatiza katikati ya Mwenyekiti na mchangiaji kinyume na Kanuni za Bunge*)

SPIKA: Mheshimiwa Bashe, rudi ulikotoka, umemkatiza Profesa. Endelea Profesa.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, umeme huu tuutoe kwenye maji, tuutoe kwenye gesi na kwenye makaa ya mawe (*coal*), halafu na *renewable* (*solar, wind, geothermal* na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *coal* hatuna hata *megawatt* moja. tulianza mjadala, tukaiambia dunia kwamba sisi hatujachafua mazingira kwa sababu siyo tu *per capita, pollution* yetu kwa kila mtu ni 0.22 *tones per person per annum*, huwezi kulinganisha na China na Marekani ambayo ina zaidi ya tani 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo la pili la kutupatia fedha nyingi ni umeme uwe mwingi, bei itashuka nchini, viwanda vitazalisha kwa bei ya chini na vile vile tunataka tuuze umeme nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naligusia ni *LNG (Liquefied Natural Gas)*. Tuna gesi kule baharini karibu 57TCF. Ni lazima tuharakishe ili tuweze kupata hizo 15 *metric tones per annum* ambazo tumepanga kuzalisha pale Lindi. Sasa hii *LNG* itatusaidia sana kuleta fedha nyingi ndani ya nchi. Ukichukua nchi kama Qatar, nimechukua mfano. Qatar haina uchumi mkubwa wa kutegemea mazao, inategemea gesi tu. Yenyewe *GDP per capita* ya Qatar ni dola 52,000. Ni *among the top ten in the world, GDP per capita* ya Qatar na wana-*depend on gas*. Kwa nini sisi gesi yetu isiharakishe huu uchumi na hizi fedha za mipango yetu tunayoifanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipanga kuzalisha ule wa kuzalisha, yaani *two trains*, maeneo ya kuzalisha. Qatar wana *14 trains*, hatuwezi kushindana nao. Wenzetu Msumbiji sasa hivi wamejipanga watazalisha *train* moja 13 million *metric tones per annum* halafu na nyingine itaenda mpaka 43. Tatizo la Msumbiji wakitutangulia ni kwamba wataweka mikataba ya muda mrefu na nchi ambazo sisi tunataka kwenda kuuza gesi. Kwa hiyo, lazima tushindane na Msumbiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nimelileta, nadhani nina muda wangu; nimechukua kwenye fedha nyingi tu. Nilimsikia yule Mheshimiwa Mbunge wa Rukwa akiongea kuhusu gesi ya *helium*. Sasa hivi duniani, ilikuwa inazalishwa kwa wingi Marekani, kule Texas na Oklahoma, wakaingia nao vita ya kwanza, ya pili inaanza kupungua. Duniani mahitaji ya *helium* ni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Kwa hiyo,...

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba hii gesi ambayo tunayo nyingi sana, kwa makisio ya awali ya wale vijana wa *Oxford* ni kwamba tuna 2.8 billion cubic feet; na sasa hivi Soko la Dunia ni six billion. Kwa hiyo, tunaweza ku-*sustain* Soko la Dunia kwa miaka kati ya 20 mpaka 30, hatutakuwa na tatizo la kung'ang'ana na uzalishaji mdogo mdogo wa viazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sospeter Muhongo. Tunakushukuru kwa sababu umetuwekea msingi wa mjadala wetu na watakaofuata wataona kwamba sasa tunajadili namna ya kuboresha Mpango wetu na mwisho wa siku tuone vipaumbele ni vipi. Basi, pamoja na mambo mengine tutajadili *in that line*. Yeye kajikita zaidi kwenye mbegu, umeme, *LNG* na *Helium*. Akayapanga mazao yake kwenye mchele, ngano, mahindi halafu muhogo. Nina hakika Mheshimiwa Musukuma angeambiwa apange haya mazao, angepanga mahindi; ugali kwanza la mwidebe, halafu muhogo udaga... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Musukuma, endelea kuchangia. *(Kicheko)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia mpango huu. Kwanza naipongeza Wizara na Mheshimiwa Profesa Mpango kwa kazi kubwa kweli ambayo yeye na wataalam wake wameionyesha kwenye kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kuipongeza sana Serikali hasa sekta ya madini ambayo mimi ni Mjumbe wake, kwa kazi nzuri sana iliyofanya na imetuonesha hata kwenye taarifa kwamba kutokana na kupokea mawazo ya wadau, Serikali imeongeza kipato kikubwa sana kutokana na wadau wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais pale alipotupa nafasi sisi wa darasa la saba tukaishauri Serikali na akatusikiliza. Baada ya kutusikiliza leo Serikali inavuna mabilioni kutokana na mawazo tuliyoyatoa sisi wa darasa la saba ambao ni watendaji wakubwa kwenye Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe tu ushauri kwa upande wa Serikali. Nianze na suala la miradi. Tumeona Serikali katika kipindi kilichopita imekuwa na miradi mikubwa ya mabilioni ya pesa ambayo haina *impact* yoyote kwenye Taifa na Watanzania wale chapakazi hasa wale wa chini, hatuoni faida ya miradi mikubwa ambayo Serikali imewekeza mabilioni ya pesa. Nimejaribu kuwasikilisha wiki iliyopita, Waheshimiwa Wabunge wengi wanalia kwamba kwenye *TARURA* hakuna hela; na nikijaribu kuangalia mawazo ya wenzangu huko chini, naona tunafikiria labda kwenda kuongeza kwenye mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mifano miwili mitatu. Mimi nilipoanza Ubunge nilikuwa Kamati ya Ardhi na tulienda kukagua mradi mmoja Morocco kwenye nyumba za watu wenye hali ya chini; nyumba za maskini; yale majengo mazuri yaliyoko Morocco. Tuligombana sana, sijui ndiyo kilisababisha Mheshimiwa Spika, ukaniamisha kunipeleka Kamati ya Madini! Niliwaambia, ikitokea uchumi ukiyumba, humu tutalaza popo. Wapo Wajumbe tuliokuwa nao hawakunisikia. Leo sasa unaona jengo lile limeisha na hakuna chochote kinachoendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya, nataka kutoa mfano tu kwamba siyo mradi mmoja wa Morocco, tunayo miradi kwa mfano Soko la Morogoro, Machinga *Complex* na sasa tuna Soko la Ndugai. Wote ni mashahidi, yamefeli, ni mabilioni mangapi yametumika? Ni kwa sababu pengine wasomi wanashindwa kutafakari kwamba wanapojenga masoko, stendi kubwa za mabilioni, ile ni huduma. Sasa wanaviweka kama vitega uchumi; na watu wanaowawekea vitega uchumi ni masikini, hawa Mama Ntilie, hawawezi kwenda mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi kuingia humu ukumbini kwa sababu hili jengo nalo lilitumia hela nyingi za Watanzania, pengine na sisi tungekuwa tunachajiwa getini, tungeona uchungu kwa yale tunayoyapanga kwa wale wananchi kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba fedha hizi za mabilioni ambazo tunawekeza kwenye vitu ambavyo havizalishi, tungewekeza zaidi kwa watu wa chini. Kwa mfano, tungechukua haya mabilioni, kila Halmashauri ikaandika miradi kama pesa mnazo, tukaenda kuboresha barabara zetu kule vijijini, wakulima watalima vizuri na mazao yao yatasafirishwa kwa bei nafuu. Itakuwa na *impact* kwenu walaji, mtapata kwa bei ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka kushauri kuhusiana na suala la biashara mitaani. Tusioneane aibu wala tusifichane, kweli hali ni mbaya. Watu wanafunga maduka, watu wamekata mitaji, lakini sioni namna ambayo Serikali yetu na viongozi wetu na Mawaziri labla wanakuja na mawazo mbadala ya kuweza kuona namna gani ya kuwabeba hawa wafanyabiashara wanaofilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetokea kwenye tasnia ya biashara huko mtaani, nina uzoefu mkubwa. Ni kweli maduka yanafungwa, wala tusifichane. Kwa nini yanafungwa? Tuone namna ya kuzibadilisha sheria. Wafanyabiashara wale waliomo humu enzi za nyuma kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano, ilikuwa inawezekana kukamatwa ukapigwa faini ukalipa. Ilikuwa inawezekana kujadili. Serikali ya Awamu ya Tano hakuna mahali mtu anaweza aka-*temper* kulipa kodi. Ila sheria zinazotumika kulipisha kodi sasa hivi ni zile zile wakati bado unaruhusiwa kulipa viwili, vinane vinapita bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tuone namna Serikali kama tunaweza; na namshauri sana Mheshimiwa Rais, kwenye hiki kipengele naona kama Mawaziri wanamwogopa Mheshimiwa Rais. Sasa kwa sababu sisi Wabunge ni Wawakilishi wa wananchi wote kwenye

maeneo yetu tunayotoka, namwomba Mheshimiwa Rais awaite wafanyabiashara, awaite waagizaji, awaite wenye viwanda na wauzaji. Tukiendelea kufumbiana macho, watu wanafilisika. Ni lazima tuwaite, tuwasikilize, tuone namna na tujifunze kutoka hata kwenye Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipomfuata Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kukamata, nyang'anya, kamata, nyang'anya, tukamwambia Mheshimiwa Rais, utatumaliza hela. Tuite utusikilize. Akatuita, tukamweleza, akapangua kutoka kodi ya asilimia 50 kurudi asilimia saba peke yake. Kwa hiyo, nadhani hata kwa hawa wafanyabiashara wa viwanda, maduka na watu wengine, tukiwaita, tukawasikiliza tutaondoa lawama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukipita huko mtaani, watu wengi tu wanasema, Magufuli amebana. Serikali imebana hela. Imebana wapi? Ni kwa sababu hatujarekebisha kodi rafiki ambazo mtu atalipa bila kuumia na Serikali itakusanya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2016, Mheshimiwa Dkt. Mpango alivyokuja hapa alikisia kukusanya milioni 81 peke yake kwa wachimbaji wadogo, tulibishana sana hapa kama *Hansard* inaweza ikakumbusha. Nikamwambia hiyo ni kodi ya mtu mmoja, baada ya kutusikiliza hebu leo ona kutoka 4.6 pato la madini mpaka kwenda kwenye *five point*. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Rais awaite wafanyabiashara awasikilize, haya maneno ya kusema hali ni nzuri, tusione aibu watu wanafilisika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa namuangalia Mheshimiwa Rais kwenye siku ya sheria alitaja orodha ya benki ambazo zinawadai wafanyabiashara kwamba zimechukua hela na hawajarudisha na benki wameenda mahakamani. Ni kweli, watu wameenda Mahakamani kwa sababu? Sababu ni nyepesi. Kwa mfano, mimi nina mtaji wangu wa shilingi milioni 50, nimeaminiwa na benki shilingi milioni 500, nafanya biashara vizuri nalipa rejesho langu vizuri inafika mahali anaingia *TRA* anasema tunakudai shilingi

milioni 500, zinaenda zile hela za benki. Kesho yake mimi nakuja kuuziwa nyumba, nitakubalije? Ni bora nikimbilie benki na mimi nikapaki tu huko tuelewane. Kwa hiyo, ni vizuri haya mambo Serikali yetu iweze tukayapitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza juzi wajumbe wanazungumza sana kuhusu Bodi ya Mikopo, mimi nadhani Bodi ya Mikopo inafanya vizuri sana na Serikali inatoa hela nyingi ila nina ushauri mdogo tu. Serikali inaamini ubongo bila mkataba, mtu anakuwa tu na elimu yake amefaulu anaenda kuaminiwa mkopo mpaka anapata *degree*, karatasi. Kwa nini Serikali isije na wazo mbadala kwamba baada ya kumpa ile *degree*, kwa sababu sisi tunaohudumia watoto mpaka kupata *degree* kwa kweli kule vijijini tunakuwa tumeshamaliza na ng'ombe tumezeeka, Serikali ije na dirisha lingine kwamba mtu anapopata *degree* karatasi kuwe na dirisha la mikopo ya hela wakaanze biashara aweke dhamana ile *degree* kwenye lile dirisha. Akiweka kile cheti chake cha *degree at least* hata milioni 10 au 20 tupunguze hizi kelele za watu kukaa wanatembea na ma-*degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifungua simu za Wabunge wako kila mtu ana CV za watu kutoka Jimboni kwake 10, 20 au 30. Sasa kama mkifungua hili dirisha mkopeshe na mitaji kwa kutumia vyeti tutaweza kuondoa ule usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la kumuongeza Mheshimiwa Rais muda, mimi naliona tofauti kidogo. Nimejifunza kwenye awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne na ya tano ukijenga hoja hapa, nazidi tu kumuomba Rais afikirie hili kwamba kwa nini watu wanasema Rais aendelee? Nikiangalia kutoka huko tulikuwa tumeshapaki anzia treni, ndege tumekata skrepa, treni tulikuwa tumeshaanza kununua skrepa leo hivi vitu vyote vinaendelea. Tunaanzisha miradi mikubwa kwa ujasiri wa mtu mmoja na hakuna ubishi kwamba bila Magufuli mawazo yake yale tusingefika hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujifunze kwa wenzetu wa Zimbabwe. Mimi siyo msomi lakini kwa sababu ya biashara

nimezunguka kidogo. Wazimbabwe walipoamua kuwafukuza Wazungu na kujitegemea Wazungu waliwapimia tu wakasema itafika mahali hawa watakuja kutupigia magoti, wakawawekea vikwazo. Wakafanya miradi yao ilivyokamilika kuwafukuza Wazungu wakajenga mpaka na kiwanda cha fedha. Ilipofika muda zilipoisha karatasi za ku-*print* pesa wazungu wakawaambia hatuwezi kuwapa hizi *material* za karatasi kwa sababu mko kwenye vikwazo. Ndiyo Serikali ya Zimbabwe ikaanza kuwa inabadilisha tu Rais anatangaza noti ya milioni moja inakuwa ya milioni 10. Baadaye watu wakaanza kulipwa mshahara kwenye kiroba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe haya mambo ambayo Rais ameyafanya na tumeona mengine yanaangukia 2024, 2025, kwa ujasiri ule ule tunaweza kuona namna kama alivyosema Mzee Butiku juzi tukamuongeza muda kwani kitu gani? Mbona wenzetu wamefanya? Ina maana sisi Watanzania tunajua demokrasia zaidi ya Wachina ambao ni matrillionea na kila mtu ana teknolojia yake? Wamefika mahali wakasema tumuone kwa mawazo haya, tumuongeze muda hata miaka 20 mbele ili aweze kukamilisha yale ambayo alikuwa ameyapanga. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tu...

MWENYEKITI: Muda hauko upande wako. Nakushukuru sana kwa mchango wako.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri siku moja mkatembea Dodoma hapa mkaona *apartments* ambazo Mheshimiwa Musukuma anajenga. Ni kweli, darasa la saba wanafanya kazi. (*Kicheko*)

Ni kweli hizi *degree* inabidi Watanzania tuziangalie sana, wakati mwingine ni ugonjwa tu. Sasa ili wapate mikopo inabidi somo la ujasiriamali litafutiwe mahali katika *course* zote pawe na kasomo ka ujasiriamali hivi. Vinginevyo itakuwa shida, watapata hiyo mitaji halafu hawataweza kurudisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jerry Silaa nilikutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Aboud.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano na wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali, k hotuba ya Waziri ameonesha kazi kubwa iliyofanyika kwa miaka mitano. Tunaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma rasimu hii ya Mpango wa Miaka Mitano, naomba kuchangia kwenye Sura ya Tano; 5.4.10 ukurasa wa 102 kwenye miundombinu ya barabara. Kwenye miaka mitano iliyopita kazi kubwa sana imefanyika kwenye miundombinu ya barabara. Nchi nzima barabara zimejengwa, madaraja yamejengwa na sisi wa Dar es Salaam tumeona ujenzi mkubwa wa miundombinu kwenye Daraja la Mfugale, Ubungo *interchange* na *interchange* zingine zinaendelea kujengwa pale Chang'ombe na ujenzi unakaribia kuanza pale Morocco na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Rasimu hii ya Mpango inaonesha jinsi gani Serikali imejipanga kwa miaka mitano hii inayokuja kukamilisha ujenzi wa barabara za lami lakini vilevile kuondoa msongamano wa magari katika majiji. Mimi naamini Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwamba unapoongelea mafanikio haya makubwa ya

miudnombinu mikubwa ya barabara lazima uoanische na barabara za ndani ambazo ndiyo zinamhudumia mwananchi katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia barabara hizi za mijini na vijijini, unaizungumzia *TARURA*. Naomba sana kuishauri Serikali kwamba lazima kwenye mpango huu kuwe na mipango inayotekelezeka ya kuisaidia *TARURA* iweze kutatua changamoto ya miundombinu kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakazi wa Jimbo la Ukonga tunamshukuru Rais, ile foleni ya *TAZARA* pale haipo tena. Hata hivyo, leo wakazi wangu akiwemo Mheshimiwa Waitara, akishavuka *TAZARA* kutoka pale Banana kuitafuta Kivule ama Kitunda kuna kazi kubwa sana. Ukienda *TARURA* mfumo mbovu lakini na fedha hazitoshi. Leo Dkt. Ndumbaro na wakazi wenzake wa Majohe atavuka vizuri *TAZARA* lakini nyumbani hapafikiki. Simu zetu hizi ukiona simu yoyote inatoka maeneo hayo unaanza kuomba dua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi yako mambo mawili ambayo Serikali ikijipanga vizuri itafikia malengo haya yaliyowekwa kwenye Rasimu ya Mpango. La kwanza, ni muundo wa *TARURA*. Tulianza vizuri, tulikuwa na *Regional Coordinator* na na Meneja wa Wilaya. Kazi ya Meneja wa Wilaya ilikuwa ni kutekeleza miradi ya barabara kule kwenye Wilaya na Majimbo yetu. Hata hivyo, mfumo umebadilika, tumemgeuza yule *Regional Coordinator* amekuwa *Regional Manager* na yule *Manager* wa Wilaya sasa hata ile kazi aliyokuwa anafanya ya kulipa wakandarasi wanaofanya kazi kwenye maeneo yake imehamishiwa mkoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kumpata mkandarasi wa kufanya kazi Nachingwea anatafutwa Lindi Mjini, mazingira haya ni tofauti sana. Huwezi ukampata mtu kufanya kazi Ngara kwa kumtafutia pale Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri ameliona hili kwenye ziara zake, ameahidi kuanza

kulifanyia kazi na mimi naomba kuishauri Serikali. Ili Mpango huu uweze kutekelezeka lazima tuwe na muundo wa uhakika wa *TARURA*. Yule Meneja wa Wilaya awezeshwe, aweze kupata wakandarasi, fedha zifike, aweze kusimamia miradi yake na aepuke kuwa karani wa kutujibu sisi maswali yetu Waheshimiwa Wabunge ambayo hana utendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakii la pili, ni fedha. Ipo dhana na naendelea kuliomba Bunge lako na Serikali ijenge dhana ya kusikiliza michango ya Wabunge kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hawa wanayoyasema hapa siyo mawazo yao ni mawazo ya wananchi wanaoawaongoza. Ipo dhana kwamba ukiongeza tozo ya barabara kwa mfano, leo Bunge likashauri kuongeza tozo ya barabara za mjini na vijijini kwenye mafuta, iko dhana kwamba gharama ya usafirishaji itaongeza. Leo kwa miundombinu isiyopitika kwenye maeneo yote ya pembezoni ya mijini na vijijini ya nchi yetu gharama za usafirishaji ziko juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mwananchi wa kule Majojhe Bomba Mbili kuitafuta Mombasa analipa nauli Sh.700 mpaka Sh.1,000. Naamini barabara ya uhakika ingejengwa leo kungekuwa na daladala zinatoka kuanzia Bomba Mbili mpaka Kariakoo na gharama ya usafirishaji itashuka badala ya kuongezeka kwa kuongeza tozo kwenye mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anapokuja ku-*wind up* Mpango na wewe mwenyewe umesema kwamba Mpango huu ni Rasimu, basi mawazo haya tunayoyatoa yaweze kuchukuliwa kwa uzito na yahusishwe kwenye Mpango huu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ya *TASAC*, miradi ya *DMDP Phase II*, kule kwetu ni kizungumkuti, inasemekana imekwama kwenye maamuzi kwenye meza za watendaji wa Serikali lakini matatizo kule chini ni makubwa sana. Ni vyema tunavyotengeneza Mpango ukaongeza na kasi ya utendaji kwa watendaji wetu hasa kwenye miradi hii inayowagusa wananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika dhana hii hii ya kusikilizwa na leo wewe nikupongeze kwenye swali lile la Mheshimiwa Gambo asubuhi lazima Serikali ijifunze kusikiliza yale yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge. Ukiingia sasa hivi kwenye mitandao *comments* za wananchi wa Arusha wanaoathirika na utalii wanasikitishwa sana na majibu yale yaliyotolewa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kuiomba Serikali hii sikivu kwa sababu tunafahamu jinsi gani Rais wetu alivyokuwa msikivu, tunaona anavyotatua matatizo ya wananchi kule anakopita, tuombe na Mpango huu na wenyewe ujipange katika kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naskuhukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jerry Silaa kwa mchango wako. Pamoja na mambo mengine amesisitiza Meneja wa Wilaya naye aweze ku-*manage* mafungu yake. Wazo zuri sana. Ndiyo lile swali la asubuhi kwamba hela iko kwa *RPC* tukawa tunashangilia, nikawashangaa wenzangu wakati matukio yakitokea majimboni kwetu gari ya polisi haina mafuta wakati mwingine inabidi Mbunge ndiyo utoe hela, inabidi wananchi ndiyo watoe hela, mafungu yako mkoani. Sasa hoja hapa yashuke halafu sisi tunasema yabakie mkoani, kweli hiyo? Wakati wewe jimboni kule ndiyo unapata hizo dhahama. Mtu amejinyonga, hakuna gari ya polisi, watu wanakaa siku mbili hawajazika na kadhalika. Ni vizuri hii sera ya kufikiri kwamba wanaohusika huko wakawa na mafungu yao kule lakini wakasimamiwa kutoka Mkoani ni jambo linatusaidia kwenda mbele.

Sijui kama nilishamtaja anayefuata, Mheshimiwa Khadija Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Hawa Mchafu ajiandae. Mheshimiwa Khadija nimekuona.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi

Mungu, Muumba Ardhi na Mbingu hashindwi na walimwengu apangalo yeye huwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Rais wetu na wasaidizi wake. Hapo walipotufikisha wametufikisha mbali, Watanzania tunajionea wenyewe maendeleo yaliyofikiwa katika kuwasaidia wananchi kwenye huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Fedha na wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri walizotuletea za mipango na makadirio. Naunga mkono hoja zote zilizowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na sekta ya kilimo. Kilimo kimeelezwa kwenye Mpango wa Mwaka Mmoja na wa Miaka Mitano. Naunga mkono hatua mbalimbali zilizoelezwa kwenye hotuba zote za kuimarisha kilimo kama uti wa mgongo wa kumuinua mwananchi mmoja mmoja na kuinua nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kina sekta nyingi lakini nitagusia kilimo ambacho kitahifadhi mazingira yetu. Ardhi yetu tunahitaji sisi kama tulivyoikuta lakini pia na kuvirithisha na vizazi vijavyo. Nahamasisha kilimo kilimo hai na kilimo hifadhi. Kilimo hai na kilimo hifadhi kinalinda ardhi yetu ili iweze kutumika kwa miaka mingi lakini pia kinatoa mazao ambayo hayana kemikali ambapo kwa sasa ni mazao yenye bei sana katika soko la dunia na wananchi duniani wanayahitaji mazao ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha bustani ni kilimo ambacho sasa hivi kinaleta hamasa sana kwa vijana na wanawake kwa sababu kina soko kubwa nje ya nchi. Hata hivyo, lazima sasa tupange ardhi yetu, ardhi ya kilimo, ufugaji, viwanda, majengo na mengineyo. Kilimo hiki ukataji wa miti ni mkubwa, tunakata miti mikubwa ya kudumu tunalima bustani. Kwa hivyo, kilimo hiki kina fedha nyingi lakini pia

kizingatie hali ya mazingira na hali ya nchi yetu kulingana na mabadiliko ya tabia nchi yanayotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na waliosema kuhusu mbegu bora. Mbegu bora zinahitajika ili kwendana na mazingira ya nchi yetu, udongo wa nchi yetu na hali ya hewa. Kwa maana hiyo sasa ni vizuri kuwekeza kwenye utafiti. Utafiti unahitaji wataalam na elimu hii ni ya muda mrefu, nashauri Serikali, kuna wataalam wetu wa utafiti ambao wamestaafu lakini sasa wanatumikia nchi za jirani, watafutwe waungane na hawa waliopo ili waje kuendeleza soko hili la kuzalisha mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji ndiyo muarobaini kutokana na hali ya hewa na mazingira ya tabianchi. Kilimo cha umwagiliaji kinatupa usalama wa chakula lakini kitatoa mazao bora kwa ajili ya malighafi za viwandani. Nashauri Sekta ya Maji iimarishwe ili yapatikane maji ya kuhudumia mifugo, viwanda, ukulima na sisi wananchi tupate maji safi na salama. Juzi nilisema Mfuko wa Maji umefanya kazi nzuri sasa unahitaji kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzalishaji wa malighafi za viwandani, lakini pia wakulima wana changamoto kubwa baada ya kuzalisha mazao yao, hakuna usafiri wa kutoka kwenye maeneo yanayozalisha hivyo vyakula kuyafikia masoko ya mijini. Mfano maziwa ni bidhaa ambayo inaharibika kwa muda mfupi sana kwa hivyo barabara za vijijini zikiwa mbaya, wakulima wa maziwa wanapata hasara na Taifa letu pia linapata hasara ya kukosa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ujenzi wa maghala na vihenge, naipongeza Serikali imefika hatua kubwa na mipango inaonesha kuna maendeleo makubwa katika ujenzi wa vihenge. Pia katika kuhifadhi chakula na usalama wa chakula, naishauri Serikali mwananchi mmoja mmoja naye aweze kuhifadhi chakula chake kwa mwaka mmoja au miwili. Kwa maana hiyo, kuna viwanda vya wawekezaji hapa nchini tayari wanazalisha mifuko ya kilo 100 na 200 kwa maana ya

mwananchi aweze kuhifadhi mazao yake. Ni vyema viwanda vile vikapunguziwa kodi na tozo mbalimbali ili mwananchi aweze kumudu gharama za kununua ile mifuko aweze kujihifadhia mwenyewe chakula chake na watu wake huko nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nagusia kidogo Sekta ya Uvuvi. Uvuvi wa Bahari Kuu tunaipongeza Serikali kwa ununuzi wa meli za uvuvi, bandari za uvuvi na maghala ya kuhifadhia samaki. Kwa vile chombo hiki ni cha Muungano, nashauri Shirika la Uvuvi la *TAFICO*, kuna mpango wa kuliimarisha, naomba sana na Shirika la Uvuvi la Zanzibar (*ZAFICO*) mambo haya yaende sambamba ili kuwekeza zaidi katika uchumi wa bahari kuu. Katika Mipango ya Miaka Mitano, nashauri na bandari moja ya uvuvi kule Zanzibar nayo ijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hiyo ya uvuvi, napenda kuchangia kwenye ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Sekta hii ni sekta ambayo haitumii nguvu kubwa. Ni vyema sasa na wala haihitaji elimu kubwa, wale vijana wetu waliomaliza darasa la saba, waliomaliza masomo darasa la tano na la nne, wanaweza kufanya hii sekta ya viumbe kwenye maji. Nina ushahidi mtoto wa darasa la tatu anafuga mwenyewe samaki wa *gold fish*, anawalisha *biscuit* tu na anawauza kwa watalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana sekta hii inawezekana kwa vijana wetu wa darasa la saba na la tano kufanya sekta ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji, kwa sababu ni sekta ambayo haihitaji elimu kubwa, haihitaji utaalum mkubwa. Tukiwekeza hapa tutapunguza wale vijana ombaomba wanaozunguka mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile Mifuko yetu ya ujasiriamali ya vikundi vya vijana ni vyema sana zikaandaliwa program maalum za vijana hawa, baada ya kumaliza masomo ndio wakapewa ile mitaji sasa kwa sababu tayari wameshapata ujuzi, wameshapata uelewa na kazi watakuwa wanaipenda, kwa hivyo, watakuwa wanafanya

kitu ambacho wanakipenda, kwa hivyo, kutakuwa na ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nakuombea dua wewe uendelee kutuongoza vizuri. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais na timu yake aendelee kutuhudumia sisi wananchi tunamhitaji, tunampenda na tunampongeza sana kwa juhudi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Aboud. Msiomfahamu Khadija alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu miaka mingi kwa hiyo, ni kingunge katika chama.

Nimeshakutaja Mheshimiwa Ahmed Shabiby, utafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba yetu ya leo ya mipango. Katika kuchangia nitajikita kwenye vile vitu ambavyo vinaleta *impact* ya haraka. Mipango ya haraka ambayo pesa yake inapatikana kwa haraka ambayo italiingizia Taifa faida kwa haraka. Nitachangia vitu viwili, nitachangia utalii na kilimo, nikipata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika hotuba ya leo inaonekana kabisa wazi kwamba, sekta ya utalii ni ya pili kwa uchangiaji kwa Taifa kwa sababu, inachangia asilimia 17.5, lakini ukiangalia katika mpango wake wa miaka mitano katika hotuba unasema kwamba, itakua hadi kufika asilimia 28. Sasa ukiangalia katika sekta hii ambayo kuna nchi zinaishi kwa kutegemea utalii peke yake kwa mfano, nchi nyingi sana zinategemea utalii hata hapo ukichukua hiyo Seychelles waliyokuwa wanaitajataja hapo, ukiangalia hata Ufaransa asilimia nayo inategemea utalii kama watu hawafahamu, Misri, Thailand, Morocco. Sasa nchi kama Tanzania ambayo

uwekezaji wake katika utalii hauna gharama kwa sababu vitu vingi tayari ni vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika vivutio, Tanzania ni nchi ya pili ukitoa Brazil, lakini hakuna mkakati wowote wa kutangaza utalii kwenye hii nchi na hakuna mkakati wowote wa kuonesha kwamba, utalii unaweza ukachangia zaidi ya asilimia 80 ya mapato ya nchi hii.

MWENYEKITI: *Chief Whip*, wakati Mheshimiwa Shabiby anazungumzia jinsi ambavyo sekta ya utalii ni muhimu kiasi hicho, humu kwenye ukumbi hamna cha Waziri wa Utalii wala Naibu wake, wana yao tu. Endelea Mheshimiwa Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa ukiangalia nini tunakwama? Tunakwama sana kwenye *advertise*, kwenye utangazaji. Hatutangazi kabisa utalii kwenye hii nchi wala hakuna mpango wa kutangaza. Kwa hiyo, ushauri wangu kwenye hizi Balozi zetu lazima pawepo na wale *commercial attaches* lazima wawepo. Tunaita muambata wa kibiashara kwa sababu, ukiweka muambata wa kibiashara kwenye kila ubalozi utakuwa unatangaza utalii, unatangaza uwekezaji, unatangaza na biashara nyingine kwa hiyo, tunakuwa na watu wa diplomasia ya uchumi ndani ya zile balozi kwa hiyo, tunakuwa tunaangalia nchi. Kwa mfano, nchi kama America tunahitaji watalii, basi tunampeleka muambata yule ambaye yeye anakuwa ni mtaalamu wa kutangaza utalii. Tunaangalia nchi fulani tuna mawasiliano nayo labda kwa ajili ya kilimo, tunampeleka muambata wa kiuchumi ambaye anahusika na kilimo, kwa hiyo, tunakuwa tunafanya hivyo. Hiyo itasaidia kuutangaza utalii wetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia leo hii mbuga ya Serengeti ni mbuga bora duniani, lakini haifahamiki kama Masai Mara ya Kenya. Sasa hapo unaweza ukajjuliza ni kitu gani kwa sababu, watalii wengi wanaokwenda Kenya wanakuja kwa ajili ya kuangalia Masai Mara ndio baadaye waje Serengeti au waje Kilimanjaro. Hata Kilimanjaro inatangazika sana Kenya kuliko Tanzania kwa hiyo,

tunachezea na hapa ndio mahali ambapo pana pesa kabisa nyingi. Mimi huwa sitaki kutoa ile mipango ambayo itafanyika huko ya maneno maneno, hapana, huu ni mpango ambao uko wazi na hii ni *hot cake* kabisa, haina shida kwenye hii pesa ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia leo Brazil kwa nini imekuwa ya kwanza duniani, ni kwa ajili ya utalii wa bahari. Sisi huku tuna utalii wa asili, lakini leo bahari kama pale Kigamboni, bahari mali kabisa, *beach* zake ni safi, leo yamejaa magereji, yamejaa maviwanda, yaani hata mpango wa kutumia ardhi haueleweki. Mimi Mbunge niko muda mrefu, hata hivi kusimama basi, maana saa nyingine mnaongea tu halafu vitu havitekelezeki. Sasa Mheshimiwa Waziri lazima aangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu watu wanalalamika kuhusu habari ya utalii sijui asilimia 10 hiyo iliyoongezwa kwenye utalii. Lazima vitu vingine watu wawe wazalendo, kumleta mtalii mmoja haya makampuni ya binafsi yanachukua dola 5,000, kwa hiyo, wewe kuongezewa dola 10 tu unapiga kelele utalii Tanzania utakufa, utakufa kwa msingi gani? Hauwezi kufa utalii kwa ajili ya dola 10, haiwezekani kitu kama hicho. Cha msingi tu ni kuantanga utalii watalii waje wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine katika utalii, lazima tuwe na *regulations, private regulations*, katika kama zilivyokuwa sekta nyingine. Leo ukija huku kwenye sekta labda ya Mawasiliano kuna *TCRA*, ukienda labda huku Uchukuzi kuna hawa wengine hawa sijui *LATRA*, ukienda kwenye Nishati kuna *EWURA*. Huku nako lazima kutengenezwe *regulation* ya *private* ili iangalie na kudhibiti maslahi pamoja na kuchukua hao wadau nao kuangalia watafanyaje, ili utalii uendelee kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya kilimo; hii lazima watu mkubali, tunapanga vitu vingi sana, lakini bahati nzuri unanifahamu vizuri ni mkulima, mfugaji, mfanyabiashara, vyote nafanya. Nchi hii tusidanganywe na

mambo mengi sana, kama tutadharau kilimo, kilimo tumebadilisha *slogan* za kila aina; kilimo ni uhai, kilimo sijui ni uti wa mgongo, sijui nguvu kazi, sijui kilimo kwanza, sasa hivi kilimo cha biashara, lakini mafanikio hakuna. Hata Mheshimiwa Bashe wakati anajibu mpango huu, mpango huu, mpango huu, wakati hela hazipo na hautekelezeki. Hii ni hadithi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tajiri namba moja wa Tanzania kwanza ni mkulima anayelima kuanzia nusu eka mpaka eka 50. Hii yote mnazungumza tu hela zimebanwa, sijui hela mtaani hakuna, kwa nini hamshangai mwezi wa Januari, Februari na Machi wakati mkulima yuko shamba ndio hela hamna ninyi? Si mjiulize? Ukiingia mwezi wa Januari, Februari na Machi, hakuna anayepanda basi, hakuna anayeingia dukani, hakuna anayenunua chochote na huko mabenki nako pesa hakuna, hakuna kila sehemu, lakini kuna mkakati gani? Kuna mpango gani wa kumnyanyua huyu mtu? Hakuna mpango wowote wa kumnyanyua huyu mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza Habari ya *irrigation*. *Irrigation* ya Tanzania tunaangalia tu mito kwa nini hatuangalii na nchi kavu kama Dodoma na sehemu nyingine? Tunatafuta dola, lakini tunapoteza dola kila siku ya Mungu kununua ngano. Tunapoteza dola kila siku ya Mungu, hizo alizeti tunasema viwanda, alizeti inayolimwa Tanzania inatosha kwa miezi mitatu tu alizeti imeisha, kwa hiyo, viwanda vinasimama. Ngano, kwa miaka hiyo ya Awamu ya Kwanza, Basutu, wale wanaotoka Arusha, mashamba ya Basutu yalikuwa yanalisha nchi nzima ya Tanzania ngano, leo hata eka moja ya ngano hailimwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya Saudi Arabia hakuna mvua. Mvua inanyesha baada ya miaka mitano, inanyesha mvua mara moja, lakini wanalima ngano tani laki saba kwa mwaka. Mwaka jana kuja mwaka huu 2019/2020 wamelima tani laki saba. Hapa Tanzania kuna bahati ya mvua mpaka tunaichukia, eka mbili hakuna, halafu tunazungumza kitu

gani? Halafu tunachukua hiyo hiyo pesa tunayoita futa, dola, tunaenda kununua ngano ambayo tunaweza tukalima tukajilisha. Tunaenda kununua mafuta ya kula ambayo tunaweza kuleta hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya *irrigation* tusidanganyane wala tusipakane mafuta hapa, Wizara ya Fedha haitoi pesa kwenye Wizara ya Kilimo, wala tusitake kupambana, haitoi pesa kabisa. Hayo mambo ya *irrigation* ni maneno tu. Labda Wabunge wageni, kama hamjui, hizi hela zinazopangwa zote ukija kuangalia zimetoka robo au hata robo isifike. Sasa mipango ya Wizara itaenda vipi? Nawashangaa tunang'ang'ania tu *TARURA*, *TARURA*, kama kilimo hakuna, *TARURA* watabeaba nini huko kwenye mabarabara hayo? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda cha mwisho, nashauri. kodi ya mafuta inayotolewa...

MWENYEKITI: Wabunge wageni mnawaona Wabunge wenyeji wanavyochambua hoja? (Makofi/Kicheko)

Endelea Mheshimiwa malizia.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa kitu kimoja, hii habari ya *TARURA*; watu wanazungumza tunatoa mazao yetu, yepi? Kama sio kupita sisi Wabunge kwenye barabara, wale wazee wameshazoea wanataka hela tu. Mwananchi akiwa na hela hata ukimpitisha shimoni hapa mradi kichwa kionekane yeye anaona barabara si ziko kama lami tu. Kinachotakiwa hapa ni kuwajengea mazingira wao kupata pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri, kwenye barabara hizi tunachangia shilingi 263 kutoka kwenye mafuta, kila lita moja na kwenye umeme tunachangia shilingi 50 kila lita; nashauri, mimi nina vituo vya mafuta na mafuta yanapanda na kushuka, kwa nini pale tusiongeze shilingi 37 iwe shilingi 300 iende kwenye kilimo ili iweze kuchukua hili eneo? Kwa sababu, kama kuna mtu mwingine na mimi

mwenyewe nina mabasi na malori silalamiki kupandishwa mafuta, sasa nione mtu alalamike humu. Ipandishwe shilingi 37 iende kwenye kilimo, tunachangia tu *EWURA*, sijui nani *TARURA*, *TARURA* wenyewe hawa ni wezi tu mimi nawashangaa mnapiga kelele, barabara wanapata hela hawatengenezi lolote. Huku kuwatoa sasa hivi hawahusiki kwa Madiwani, wamekuwa Mungu mtu, nashangaa Wabunge hamzungumzi hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana *TARURA* sasa hivi Madiwani ndio wana mikakati ya barabara zile. Diwani ndio anayesema barabara ya kimkakati ni barabara fulani kutoka pale kwenda pale, lakini leo *TARURA* wamekuwa wao Mameneja wa Wilaya, Mameneja wa Mikoa wamekuwa kama Mungu mtu kwa sababu, hawawajibiki kwa Madiwani. Wabaki kwenye *management*, lakini lazima mipango yao irudi kulekule kwa Madiwani. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shabiby. Tuchangie mpango jamani ili tuoneshe njia tusaidie Mawaziri wetu tuweze kwenda mbele kwa kuzungumza shida halisi za wananchi. Hawa akina *TARURA*, sijui *RUWASA*, nasikia baadhi ya hawa akina *RUWASA* nani hawa, mshahara wa Meneja wa Wilaya unamzidi Waziri. Sijui ni kweli kiasi gani, lakini inasemekana kwamba wanalipwa kwelikweli, kwa kazi ipi? Haya. (*Makofi/Kicheko*)

Nilikutaja Mheshimiwa Grace Tendega. Utafuatiwa na Mheshimiwa Masauni.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao ni wa kuanzia mwaka 2021/2022 na 2025/2026. Nianze tu kwa kusema kupanga ni kuchagua, unavyopanga mpango matarajio ni kwamba, mpango ule angalau utatekelezeka kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanga katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, wanasema wametenga karibu trilioni

118 za miradi, lakini nikisema niseme jinsi fedha zinavyotolewa katika mipango ambayo imekuwepo toka Mpango wa Kwanza, Mpango wa Pili na sasa tunakwenda Mpango wa Tatu; nichukulie tu mfano sekta ya viwanda, kwa fedha za maendeleo ambazo zilitolewa kwa mwaka 2016/2017 ilikuwa ni asilimia 44; mwaka 2017/2018 ilikuwa asilimia 9.5; na mwaka 2018/2019 ilikuwa asilimia 6.5 tu. Sasa hivi ukijumlisha kwa miaka hiyo unakuta kwamba, utekelezaji wake ulikuwa ni asilimia 20 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunavyokuwa tunapanga hii mipango wananchi wanakuwa na mategemeo makubwa sana ya kuhakikisha kwamba, mipango tuliyoupana itatupeleka katika uchumi ambao tumesema tunataka kufikia, uchumi wa kati, lakini nashukuru Mheshimiwa Muhongo amelezea vizuri jinsi ambavyo tunaweza tukafikia katika uchumi huo wa kati kama tukifuata mikakati na jinsi ambavyo tutaishauri Serikali iweze kufikia katika huo uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda ambayo kwa miaka minne, Awamu ya Nne mwaka 2015 tulifikia kiasi cha dola 1.3 bilioni, lakini kwa Awamu ya Tano tulishuka, mwaka 2018/2019 ilikuwa ni dola milioni 894, mwaka 2019/2020 dola 805.2 milioni. Sasa unaangalia thamani ya mauzo ya nje ya viwanda, hii *value of exports* tumeshuka, sasa kama tumeshuka, je, nini ambacho kinakwamisha tusifike kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotukwamisha ukiangalia masuala mengi hatuna mazingira muafaka ya uwekezaji. Mazingira ya uwekezaji yamekuwa ni ya kusumbua wawekezaji, watu wanafilisiwa, watu wamehamisha biashara Mheshimiwa Musukuma amezungumza, utitiri wa kodi, sasa hivi vyote vinaikosha Serikali mapato.

Kwa hiyo, Serikali lazima iangalie namna ambavyo inaweza ikarekebisha tozo mbalimbali zikawasaidie wawekezaji na uchumi uweze kupanda na tuweze kunyanyua kipato hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hakuna mkakati mahususi kwa vijana wetu. Nasema kwa vijana kwa sababu, unapowekeza kuanzia kwa vijana mpaka watafika mbele watatengeneza uwanda mpana sana wa maendeleo. Sasa *private sector* haijapewa mkakati mkubwa, tumeiweka pembeni hatuitili mkazo, vijana hawaandaliwi kuja kuwa wawekezaji. Kwa hiyo, lazima Serikali iwe na mkakati wa kuhakikisha vijana wanaandaliwa kuja kuwa wawekezaji katika nchi hii. Tunasema vijana ni Taifa la leo, wawekewe mikakati mahususi ya kuhakikisha kwamba, watakuwa wawekezaji wazuri katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine lazima tuwezeshe uchumi wa wananchi kuwa na mtaji. Waziri wa Viwanda aliyetangulia, Mheshimiwa Mwijage, alikuwa anatuambia hata ukiwa na vyerehani vitatu au vinne ni kiwanda, hata ukiwa na *blender* ni kiwanda, lakini lazima tutengeneze uwezo wa kuwawezesha watu kuwa na mitaji. Hii itafanya watu kuwa wanawekeza kwenye viwanda, Watanzania hata watu wa nje wanaweza wakawa na mitaji ya kuweza kuwekeza katika nchi yetu. Sasa Serikali iangalie hawa Mawaziri ambao wanakuja wakitamka maneno ya namna hiyo na kuwafanya Watanzania washangae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, enzi za Mwalimu ilikuwa ukitamka kiwanda unajua kuna kiwanda cha *TANCUTA/masi*, kuna *MWATEX*, kuna Kiwanda cha Magurudumu, vilikuwa vinaeleweka, lakini leo tunatajiwa kwamba, kuna viwanda elfu nane na kitu ambacho Mheshimiwa Waziri ametamka hapa, lakini ukiangalia vingi viko kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kKivitendo kwenda ukaviona hivyo viwanda ni changamoto. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri anaporudi kujibu hapa atueleze kinagaubaga uwekezaji huo umewekezwa wapi? Pamoja na kwamba, wametaja baadhi ya viwanda vinne, vitano, ambavyo viko pale kwamba 201 hivyo ni viwanda vikubwa, lakini sijui kuna viwanda elfu nane na kitu ambavyo hivyo havieleweki viko wapi? Naomba ufafanuzi uwepo wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie jinsi ambavyo tutaoanisha kilimo na viwanda. Kilimo tumekitupa kabisa katika, hatujawekeza. Mwaka, kama sikosei 2018/2019, ni asilimia mbili tu ya fedha za maendeleo ndio ilitolewa kwenye kilimo. Kwa hiyo, nashauri tuwekeze katika kilimo kwa sababu, kilimo ni ajira na vijana wengi na asilimia zaidi ya 67 wanaweza wakapata ajira kupitia kilimo, akinababa, wanawake, vijana, wanaweza wakapata ajira kupitia kilimo. Kwa hiyo, Serikali lazima iangalie katika utoaji wa fedha katika bajeti ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunafanya mipango, tunaisoma kwenye maandishi, utekelezaji Wizara ya Fedha toeni fedha katika utekelezaji katika sekta hii kwa sababu, fedha hazitoki. Tutaona, tutakwenda tutaangalia katika bajeti, fedha ambayo ilitengwa 2020/2021 utakuja kukuta kwamba, asilimia kubwa kabisa haijatolewa. Kwa hiyo, tuombe Serikali itoe fedha kwenye sekta ya kilimo ili hawa watu waweze kufanya kilimo chenye tija na waweze kutumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi katika miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kitasaidia sana katika kuongeza pato na mpango ukaweza kufanikiwa, lakini sisi hatuna miundombinu inayoridhisha katika kilimo cha umwagiliaji, sisi tunategemea mvua ambayo Mwenyezi Mungu anatupa. Kwa hiyo, tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji kwa nafasi kubwa, ili tuweze kukidhi hayo yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la ukuaji wa pato la Taifa. Pato la Taifa wanasema linakua, lakini hali-reflect hali halisi. Wanasema pato limekuwa, lakini hali halisi tunaiona, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa, ukiangalia Maisha ya Mtanzania, hali ni ngumu, watu wanaweza wakasema kwamba, ooh, sijui kuna kubana matumizi, kuna hiki, kuna kile, lakini hili pato la Taifa ambalo tunasema limekua kiuchumi, tunaomba wachumi wenzetu watueleweshe vizuri, wale wakulima wa kule kijijini wanavyosikia pato limekua hawaelewi kwamba, limekuaje?

maisha yanazidi kuwa magumu, vitu bei zinapanda na masuala mengine kama hayo. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo...

MWENYEKITI: Sentensi ya mwisho, malizia.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hali ya uchumi ngumu duniani kote Mheshimiwa Grace, sio Tanzania tu. *(Kicheko)*

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza shughuli zake kwa muda huu.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuruni sana, tumeanza vizuri mawasilisho ya Serikali kuhusu Mipango na pia mjadala mmeanza vizuri, tutaendelea nao jioni na tutaendelea nao wiki nzima, tuendeleo kujiandaa vizuri. Tusome mapendekezo kama yalivyo, lakini pia tuje na ushauri mzuri katika kujadili mpango huu, ili tujenge msingi, maana utekelezaji wa Mpango huu ambao ndio wa kwanza kwa Bunge hili utasaidia sana kuweka msingi mzuri kwa miaka mitano inayokuja, namna gani tuweze kwenda. Kwa hiyo, mwendeleo kujipanga vizuri na sisi tutajitahidi hapa mezani kuwapa nafasi kadiri ya hali itakavyokuwa.

Nina tangazo moja tu kwamba, Wabunge wa CCM mkitoka hapa mnatakiwa hapo Ukumbi wa Msekwa kwa muda mfupi tu.

Baada ya maneno haya, basi naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni na mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Charles Mwijage, akifuatiwa na Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Masauni pia ajiandae.

(Saa 7.07 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge liliudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022

SPIKA: Katibu tena.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Kamati ya Mipango, Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango mbalimbali kama tulivyoanza asubuhi. Kwa kweli nikikutaja ukiwa haupo mpaka tuje tukurudie tena itakuwa imechukua muda. Kwa hiyo, ili kuokoa muda tunaendelea na dakika

10, 10 zetu, Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso. Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano na Mpango wa Mwaka Mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango na Serikali kwa kuja na mpango huu maana yake sasa tumefanikiwa kuikamilisha mipango yetu mitatu. Mpango wa kwanza, mpango wa pili ambao tunaamaliza sasa na tunakwenda kwenye mpango wa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napoanza kuchangia narejea kwenye maandiko, lengo kuu la Mpango wa Tatu ni kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya 2025 yaani kuwa na Watanzania wenye kipato (*income per capita*) Dola 3,000, kuwa na jamii ya Watanzania iliyoelimika na yenye uchu wa kujifunza, kuwa na uchumi shindani wenye uwezo wa kuagiza na kuuza nje, utawala bora lakini eneo ambalo sisi tunalimudu la umoja, mshikamano na amani. Nina imani hapa tunafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla hatujaenda kwenye mapendekezo yangu nipitie kwenye dhima tunayomaliza na dhima tunayokwenda. Uzuri wa kitabu hutangazwa na kichwa cha kitabu (*the title*). Kwa waandishi wazuri kama Mheshimiwa Dkt. Philipo Mpango unaweza kusoma jina lake la kitabu ukajua uzuri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya mpango wa pili wa miaka mitano ambao tunamalizia, ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Ni vitu viwili; kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu lakini kujenga uchumi wa viwanda, ni zaidi ya kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu alikuwa anashangaa muhubiri wa zamani aliyekuwa anahimiza watu kutumia cherehani kumbe ni kujenga uchumi wa viwanda siyo kujenga kiwanda, ni kujenga utamaduni (*the culture*).

Rafiki yangu marehemu Shah wa A to Z alianza na cherehani kimoja wakati anakufa alikuwa ana kiwanda cha A to Z na alikuwa mlipaji mkubwa wa kodi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha kubwa ni ujenzi wa uchumi wa viwanda unaweza kuanza kidogo kidogo halafu unakua. Watanzania ndicho tunapaswa kufanya kwamba ujenge utamaduni wa kitu kusudi mwisho wa siku uweze kufika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima mpya ni kujenga uchumi shindani (*the competitive economy*) kwamba katika mawanda yote tuwe na *competitive economy*. Nakubaliana na jina la kitabu, nakuja kwenye mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma mipango yote mitatu, huu mpango umeandikwa tulidhamiria kuchangamsha *productive sectors* (sekta za uzalishaji). Mpango tuliomaliza ilikuwa kutengeneza miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi, tumeishaitengeneza, sasa ni kuchangamsha shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeandikwa ifikapo 2025 hatutaki uchumi wa kati, tunataka uchumi wa kati uliojumuishi. Ili uweze kupata uchumi wa kati uliojumuishi wale watu wanaohusika lazima uwajumuishe. Unawatoa wapi? Ni kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyie mnaoandika mpango mmesema hii ni rasimu lazima rasimu hii ije na miradi kielelezi (*flagship projects*) kwenye sekta zitakazotujumuisha. Tunaweza kuvumbua madini na kuyazindua, gesi, *helium*, *mention whatever*, tukawa na *GDP* na *income per capita* ya Dola 15,000 haina maana yoyote chenye maana ni uchumi jumuishi. Uchumi jumuishi ni kuwachukua Watanzania hawa katika shughuli zao wanazofanya ukazizindua kwa nguvu wakaweza kuzipeleka kwenye shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda mfano mmoja wa Singida, *block farming*, Singida wanachukua watu kwenye

ekari 6,000 wanakwambia kulima hapa *minimum* eka 5 ukiweza eka 20 hauna *caterpillar* wanakuletea. Wanakuwezesha unalima halafu kwenye kuvuna ndipo wanakukata. Tunataka uwekezaji *flagship project* kwenye miradi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika mipango ya Serikali wanazungumza vihenge, wanazungumza hifadhi. Hoja siyo kuwa na vihenge, tunachotaka kusikia ni uwezo wa taifa wa kuhifadhi bidhaa au chakula kwa kipindi gani. Tuambiwe kwamba tunaweza kuhifadhi mchele wa kulisha nchi hii miaka mitatu, miaka minne ikinyesha mvua likitoka jua hizo ndizo hesabu hoja siyo vihenge. Unaweza kuwa una kihenge ukaita watu 10 wakakila wakakimaliza siku moja. Kwa hiyo, tunataka malengo makubwa mtueleze kwa muda gani. Tunapokwenda kwenye hizi *productive sectors* kama alivyosema marehemu Ruge, Mungu amrehemu tunaanzia sokoni, mchele una soko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napoipongeza Serikali kwa dhima iliyopita kuna jambo napaswa nilizungumze. Kuna jambo moja la kuangalia na niko tayari kukosolewa, tumeweza kukusanya mapato kwa sababu ya *compliance*, namna gani watu wali-*comply* siyo mjadala wa leo, tumepata trilioni 2, niliwahi kusema tunaweza kupata hata 3 hata 4. *Compliance* ilipatikanaje siyo mjadala tunapaswa tupate mapato makubwa kutokana na ukuaji lakini ukuaji haupo, sekta binafsi inapaswa ikue haikui. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *compliance* ndiyo imetufikisha hapa, walifanywaje watu kulipa kodi mimi sijui, nisiingie kwenye mjadala huo lakini tunapaswa tukue. Hapa ndipo inapokuja hoja ya kujenga sekta binafsi ya Tanzania. Ili tuweze kufika yale malengo sekta binafsi ya Tanzania inapaswa ijengwe. Wasikudanganye popote duniani sekta binafsi hujengwa na haiendi kwa miaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili unaweza kujenga sekta binafsi, mimi mwenyewe mikononi mwangu nimetengeneza mabilionea naweza nikawazungumza hapa

na wengine kaka zao wako humu kwamba Mwijage ndiyo alimtengeneza kaka na msishangae hata Monduli Sajenti ndiyo hutengeneza Brigedia. Kwa hiyo, lazima tutengeneze sekta binafsi, tuwawezeshe. Watu wanachelea kwamba watapoteza pesa, usipochafuka utajifunzaje? Wape wapoteze pesa watoke. Kwa hiyo, kuna haja hiyo ya kuweza kujenga sekta binafsi ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliseme hili tunapointia kwenye Mpango wa Tatu maana yake ni nini? Dira ya Taifa 2025 inakwisha kesho. Kwa hiyo, kuna jukumu la kuhisha Dira mpya ya Taifa na hapa tujiangalie, kanuni iliyotupa ushindi leo kesho inaweza isifae. Tunaweza kuwa tunajivuna na rasilimali ambazo kesho zitakuwa ni *obsolete*. Tunazungumza chuma ikaja dunia isiyohitaji chuma, unazungumza *petrol* yanakuja magari ya *hydrogen* na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima leo katika Mpango huu wa Miaka Mitano tutege kipindi tuzungumze Dira mpya ya Taifa, tuhusishe watu wengi. Hii ni lazima muiweke kwenye mpango kwa sababu tunapanga kesho *ijayo, the fourth industrial revolution* inazungumza mambo yanatisha watu wanaanza kulima bila kutegemea udongo, watu wanaendesha viwanda vinavyotumia watu wachache lazima tujipange tunajua tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napomalizia katika mpango wa mwaka mmoja Serikali wanasema watakwenda kumaliza matatizo ya ardhi Kagera kwa kutoa hekari 7,000 kwa JKT SUMA na hekari 22,000 kwa vijiji vya Misenyi. Kagera haigawanyiki, Kagera ni moja. Huwezi kumaliza tatizo la Misenyi bila kumaliza tatizo la Muleba, Karagwe na Bukoba Vijijini. Huu mpango kama unamaliza Misenyi afadhali uachwe, mnapoifuata Kagera muifuate Kagera nzima. Ukimaliza tatizo la Misenyi litahamia Bukoba utakuwa hujatatua tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoweza kumaliza mgogoro wa ardhi Kagera siyo pesa ni ushirikishwaji wa

wananchi. Sisi Wabunge ndiyo viongozi wa wananchi mtushirikishe, mnahitaji siku 15 mgogoro umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano na Mpango wa Mwaka Mmoja tuendelee kuuchakata. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Msisitizo wako ni sekta binafsi. Mheshimiwa Moshi Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Masauni.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafsi nami nichangie Mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika eneo moja ambalo litatusaidia sana Waheshimiwa Wabunge tujue nini cha kufanya. Asilimia kubwa ya Wabunge wanalalamikia sana miundombinu na *TARURA*. Yalikuwepo mawazo kufikia hatua ya kutaka kufanya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwaelimisha ili wajue. La kwanza Mfuko wa Barabara umeundwa kwa sheria ambayo ilipitishwa na Bunge. Malengo yake yalikuwa kuhakikisha barabara zilizojengwa na *TANROADS* zinakuwa imara na zinapitika katika kipindi chote. Fedha za Mfuko wa Barabara si nyingi, ni karibia bilioni 900 kwa mwaka. Asimilia 70 ya fedha hizo zinaenda *TANROADS* kwa ajili ya *maintenance* barabara zetu, 30% ndizo ambazo zinaenda kuhudumia barabara za vijijini na mijini. Sasa hapa ndipo ambapo mnaweza mkaona kwamba tuna eneo ambalo Serikali inatakiwa ilifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara ambao una 100%, 70% zinachukuliwa na *TANROADS* na ..

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, anayechangia ndiye Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Miundombinu. Kwa hiyo, tumsikilize vizuri mawazo yake kuhusu hii hoja ambayo

Wabunge tumekuwa tukiisemea sana ya TANROADS na TARURA. Endelea Mheshimiwa. (*Makofi*)

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizo 30% hazina uwezo wa kutengeneza kitu chochote. Kwa mwaka 2015/2016 Mfuko wa Barabara; *TANROADS* walipata shilingi bilioni 541 na *TARURA* zilienda shilingi bilioni 257. Mwaka 2016/2017 *TANROADS* zilienda shilingi bilioni 519 na *TARURA* zilienda shilingi bilioni 247. Mwaka 2018 *TANROADS* zilienda shilingi bilioni 573 na *TARURA* zilienda shilingi bilioni 246. Mwaka 2020 *TANROADS* zimeenda shilingi bilioni 524 na *TARURA* zimeenda shilingi 224. Mwaka 2021 *TANROADS* zitaenda shilingi bilioni 572 na *TARURA* zitaenda shilingi bilioni 245. Barabara za *TARURA* zina zaidi ya kilometa 130,000 kitu ambacho haziwezi kutengenezwa kwa hizi fedha zinazotengwa. Ni miujiza ambayo itatokea kama tutaweza kutatua tatizo la *TARURA*. *TANROADS* wanaweza kwa sababu Serikali Kuu wanatoa bajeti ya kujenga barabara na hata hizi zinazotengwa kwa 70% hazitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri Waheshimiwa Wabunge, tunapokuwa tunajenga hoja ili barabara zetu ziweze kutengenezwa tuna maeneo ambayo tunaweza tukaishauri Serikali. La kwanza Serikali itenge fedha iwape TAMISEMI wawe na bajeti kwa ajili ya kujenga barabara zetu za vijijini. La pili linahitaji maamuzi sisi wenyewe kama Wabunge. Mimi naangalia chanzo kipya ambacho tunaweza tukakiangalia kikaja kutatua tatizo la ujenzi wa barabara za mijini na vijijini kupitia *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele ambacho nataka niwashawishi Wabunge wenzangu kama tutafika mahali tukakubaliana, tukaishauri Serikali na Serikali ikachukua mawazo yetu, tuna eneo la mawasiliano. Kwenye sekta ya mawasiliano kwa siku tuna uwezo wa kutumia simu milioni 30, hizo zinafanya kazi ndani ya nchi yetu, tuna idadi ya simu karibia milioni 50. Kwa hiyo, milioni 30 zina uwezekano wa kupata chanzo kipya cha fedha na huko ni eneo ambalo ni *luxury* tu asilimia kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza tutenge shilingi kumi kila mtumiaji wa simu ajue kwamba leo ninapopiga simu nachangia shilingi kumi kwa ajili ya mfuko wa barabara, zitakazokuja kujenga barabara za miji na vijijini. Milioni 30 mara kumi utapata milioni 300 mara saa moja, mara mwezi, mara mwaka, tuna uwezo wa kupata trilioni 1.296 ambazo zitakuja kutoa tatizo la barabara, hapo tunakuwa na chanzo ambacho ni kizuri na ambacho hakitakuwa na tatizo kwa wananchi wote na watu watakuwa wanajua kwamba mimi kama mtumiaji wa simu ninayetumia siku ya leo nimechangia barabara za miji na vijijini, tatizo hili litakuwa limeondoka kabisa. Naomba eneo tulifanyie kazi na wenzetu wa Kamati ya Bajeti waendee wakajaribu kuangalia haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye eneo hilo hilo la mawasiliano, sisi tunafanya miamala ya simu kwa siku kwa mwezi tunafanya miamala yenye thamani ya shilingi milioni 300, kila mwezi ambayo iko kwenye mzunguko na Serikali wanapata fedha kupitia mzunguko huo huo karibu kwa mwezi mmoja kunakuwa mzunguko wa fedha wa trilioni 18 zinazozunguka kwenye sekta ya mawasiliano.

Kwa hiyo, hata huko nako tukiangalia kwamba pana uwezekano naamini tunaweza tukafikia karibu trilioni moja na nusu tukapata fedha hizi zikaja kujenga mazingira ambayo yatawasaidia Watanzania, hata hiki kilimo tunachokisema kama hatuna barabara zinazounganisha huko vijijini ni sawa na hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo ambalo nililiona ni la muhimu sana, na ile dhana ambayo mnafikiri Waheshimiwa Wabunge kwamba tuzigawanye zile fedha tunakosea. Tusije tukarogwa kuja kupotosha kabisa kuuhamisha ule Mfuko wa *TANROAD*, tukihamisha matokeo yake barabara nyingi zilizojengwa na Serikali zitakufa, tukajifunze Zambia, Zambia walifanya kosa kama hili walijenga barabara hawakutenga fedha za *maintenance* matokeo yake barabara zote asilimia kubwa zilikuwa mashimo mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini ipo barabara ambayo ni ya mfano ilijengwa kwa mfumo huo, haikutengewa fedha za *maintenance*, barabara ya kutoka Arusha, Minjingu iliisha ndani ya kipindi kifupi sana. Naomba hili tulifanyie kazi na naomba Serikali ipokee mawazo ili yaweze kusaidia kutatua tatizo la barabara za miji na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ndilo nililochagua kuchangia kwenye mpango ili liweze kutusaidia na wananchi wote wajue na Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba mfuko tunaouchangia ni mfuko ambao fedha zake sio nyingi sana na tukiumega una athari kubwa sana ambazo zitaleta kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso. Nilishakutaja Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni na atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu na Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

MHE. ENG. HAMAD MASAUNI YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwanza kuipongeza Serikali kwa ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano iliyopita ambao tumeona mwenendo wa viashiria vyote vya uchumi vikiimarika licha ya nchi yetu ama dunia kwa ujumla kukumbwa na janga la *Covid 19*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu mafanikio haya yamechangiwa zaidi na uongozi imara, uongozi thabiti na wenye maono katika nchi yetu. Mara nyingi uongozi thabiti na uongozi imara hupimwa pale Taifa linapoingia katika misukosuko ama Taifa linapohitajika kutoa maamuzi magumu na mazito kwenye maslahi ya nchi na watu wake hapo ndio unaweza kujua kama nchi hii ina uongozi thabiti ama laa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bahati njema Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, kiongozi wetu mkuu

amejipambanua vya kutosha katika eneo hilo, wala sio nilichokipanga kukizungumza hapa. Leo nimepanga kuzungumza mchango wangu kuhusiana na mpango. Nitaomba angalau nitumie hata dakika moja nizungumze jambo moja la msingi sana na hasa kwa sisi ambao tunatokea Zanzibar. Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli wakati akiwa vilevile ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi amesimamia vema maandalizi ya ilani ambayo maandalizi hayo katika Ibara 136(e) kwenye maeneo mahususi ya Zanzibar yameweza kutoa mwelekeo mpya wa uchumi wa *blue* kama ni sekta ya kipaumbele kwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa sasa hivi wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi ameanza vizuri sana katika siku si zaidi ya mia moja tumeshuhudia utiaji saine wa mikataba mikubwa ya ujenzi wa bandari za uvuvi, bandari za mafuta na gesi, bandari za mizigo, kiwanda cha kuchakata samaki, Chuo Kikuu cha Uvuvi, chelezo na kadhalika haya ni mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kabisa miradi hii itakapokuwa imekamilika kwa wakati, basi itaiondosha Zanzibar na kupiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo na changamoto ya ajira kwa vijana ikiwemo vijana wa Jimbo langu la Kikwajuni itakuwa limepata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, maono yake haya hayakuwa yameanzia juu juu, mtakumbuka mara nyingi zinapokuja shughuli za uchumi wa bluu miaka ya nyuma alikuwa aki-*delegate* kwa Rais wa Zanzibar aliyekuwa wakati huo Dkt. Shein, lakini kana kwamba hiyo haitoshi, ameamua kugawa meli nusu kwa nusu bila kujali ukubwa wa kijiografia wala kidemografia kwa Taifa hili kati ya Zanzibar na Bara hii inadhihirisha ni mapenzi makubwa ambayo anayo kwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge katika hili wameunga mkono naamini hii inadhihirisha umma kwamba muungano wetu huu

si muungano wa vitu ni Muungano wa kidugu wa damu.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika mpango, langu ni moja kwamba juu ya mafanikio yote ambayo tumeyazungumza ni ukweli usiofichika kwamba tuna changamoto ya idadi ya maskini wengi katika nchi hii. Wataalam wanasema kwamba wananchi wa Tanzania ambao wanaishi chini ya Dola 1.9 ni zaidi ya nusu. Ni kweli kasi ya umaskini imepungua kwa mujibu wa takwimu za miaka kumi mpaka 2018, wanasema kasi ya umaskini imeshuka kutoka asilimia 34.4 kuja asilimia 26.4. Hata hivyo, takwimu hizo hizo za wakati huo huo zinaonesha kwamba idadi ya umaskini imeongezeka zaidi ya milioni moja, kutoka maskini milioni 14 kuja 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna jambo la kufanya ambapo tunaenda nao, kwanza lazima tujue tatizo ni nini? Tatizo ni moja kubwa la msingi kwamba sekta hizi ambazo zinaajiri watu wengi, kwa zaidi asilimia 66.6 ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi ukuaji wake ni mdogo kulinganisha na sekta ambazo haziajiri watu wengi kama vile ujenzi, huduma, madini na kadhalika. Kwa hiyo kuna haja ya msingi ya kuhakikisha kwamba sasa kipaumbele chetu tunawekeza katika sekta hizi ambazo zinaajiri watu wengi zaidi na kuzifungamanisha sekta hizi na viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kauli mbiu ya mpango wetu wa mwaka ujao unazungumzia kwamba ukuaji wa kujenga uchumi wa viwanda na kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Sina shaka kwenye maendeleo ya watu tumefanya kazi nzuri, tunapozungumzia kupungua kwa umaskini ni kwa sababu ya kazi nzuri ambayo imefanya kwenye kuwekeza katika sekta ya elimu, katika sekta ya maji, sekta ya umeme vijijini na maeneo mengi, ina maana umaskini umepungua kasi yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitajika sasa hivi tuwekeze katika kuona jinsi gani tunaibua fursa za kiuchumi kwa watu ambao wanashiriki katika sekta hizi na njia peke

ya kufanya hivyo ni kuona kwamba sasa tunaifungamanisha na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nataka tufanye marekebisho katika hii kauli mbiu, badala ya kusema kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu mimi nasema iwe na kupunguza idadi ya maskini huku mwisho imalizie hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, bahati mbaya au bahati nzuri jimbo langu mimi sisi tunalima asmuni tu, kwa hiyo naomba nitoe mapendekezo zaidi nikijikita katika uvuvi. Jambo la kwanza na kubwa kuliko yote ili viwanda vya uvuvi viweze kusimama lazima wawepo samaki wa kutosha na samaki wa kutosha hatuwezi kuwapata kama hatuna utaratibu mzuri, aidha, wa kupitia *public* ama *private sectors*. Kwa hiyo, lazima ili hoja ya Mheshimiwa Rais aliyozungumza ya kununua meli katika Bunge hili kuanzia bajeti ya mwaka huu tuhakikishe kwamba Serikali tunaishauri inaongeza bajeti ya kuweza kununua angalau meli mbili kila mwaka za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wewe ni *champion* wa hili jambo, ulifanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba tunasimamia kupitisha Sheria mpya ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Hoja ya uvuvi ya bahari kuu haiepukiki na hoja hii ilipofikia imefikia pazuri, nimpongeze Waziri wa Mifugo na timu yake wameanza kazi vizuri. Sasa hivi kanuni lazima aziharakishe, lazima ahakikishe kwamba wanashirikiana na mwenzake Waziri wa Zanzibar kuharakisha kanuni. Kanuni hizi zitakapokamilika ndipo changamoto nyingi ambazo zilikuwa zikikwaza sekta ya uvuvi na viwanda vitakapokuwa vikipata ufumbuzi ikiwemo suala la tozo na suala la leseni, utaratibu wa *exemption* na mambo mengine mengi, utaratibu wa kujengea uwezo vijana wetu ili waweze kushiriki katika sekta hii ni na mambo mengi ambayo tuliyajadili vizuri mwaka uliopita kwenye mabadiliko la sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika Mpango huu limezungumzwa suala la ujenzi wa Bandari ya Mbegani, kwa mtazamo wangu kwanza bandari moja haitoshi. Nakumbuka Mheshimiwa Rais wa hapa wakati anazindua Bunge alishangazwa sana kuona kwamba ukanda mzima wa bahari hindi kuanzia Lindi, Mtwara, Mafia, Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Pemba, Ugunja, hakuna hata kiwanda kimoja cha kuchakata samaki. Hii inasababishwa na nini? Kwa sababu tutakapokuwa tumeimarisha miundombinu mizuri, miundombinu ya viwanda, miundombinu ya bandari na tukaweza kuwajengea uwezo wananchi wakashiriki vizuri katika uchumi huu wa bahari kuu, itasaidia sana kuweza kuchochea sekta hii na sekta ya uvuvi itaimarika na hatimaye tutaweza kupambana na changamoto ya kupunguza umaskini katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilidharimia kuchangia katika eneo hilo la uvuvi, nakushuru sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, nimeshakutaja Mheshimiwa Hawa Mchafu na atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hyayuma ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyekiti Mungu aliyenijalia kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiusoma Mpango wa Maendeleo, ukichukua Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi na ukiangalia hotuba za Mheshimiwa Rais, nyaraka zote hizi zinajielekeza katika kukuza uchumi wa nchi yetu, kupunguza umaskini na kuondoa ukosefu wa ajira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana sote hapa Serikali ya Awamu ya Tano imejizatiti katika kukuza uchumi

wa nchi yetu na hili linajidhihirisha pale Serikali ya Awamu ya Tano ilipoamua kwa makusudi kuanzisha miradi ama kujenga miradi ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule ambao unaenda kutupa *megawatt* 2,115 nini tafsiri yake? Tafsiri yake ni kwamba viwanda vilivyopo na viwanda vitakavyojengwa vinaenda kupata umeme wa uhakika, vinaenda kupata ambao hauna kusuasua katika suala zima la kuchakata, kusindika, kuzalisha bidhaa na kupeleka sokoni, jambo ambalo linaenda kuleta mzunguko wa fedha. Bidhaa zinazozalishwa ni kwa ajili ya soko la ndani na zile zinazozalishwa kwa ajili ya kupeleka nje *exportation*, jambo ambalo litatuletea *forex*, ni kitu ama ni chachu inayochochea ama inayochagiza uchumi wa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ujenzi wa reli iendayo kasi, ujenzi wa miundombinu ya barabara na ununuzi wa ndege mpya 11 vyote hivi kwa pamoja vinachagiza, vinachochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuangalia Mpango, nitapenda kujielekeza jicho langu litaenda katika Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara ya Mifugo. Nikianza na Wizara ya pacha, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji, ndani ya Mkoa wetu wa Pwani, lipo eneo linajulikana kama Kata ya Kwala, ama linajulikana Kwala. Kwala ni *potentials* sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, ninapoizungumza Kwala ndio kule ambapo kuna *biggest dry port*, tuna bandari kavu kule, lakini pia tukiizungumzia Kwala, kuna *sub-station* kubwa ya umeme inayotoka *Stigler's* kuelekea Chalinze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia i ukiizungumzia Kwala umepita pale Mto Ruvu, tunapoizungumzia Kwala kuna reli ya *TAZARA* pale, tunapoizungumzia Kata ya Kwala kuna *central railway line* ama *SGR* na *measuring yard*. Tutakubaliana halipo eneo katika Tanzania hii linalofana na Kata ya Kwala ndani ya Mkoa wa Pwani, lina vitu vyote, lina

vichocheo vyote ambavyo mwekezaji yeyote akifika ndani ya nchi yetu leo hatashindwa kuwekeza pale kwa sababu lina vitu vyote ambavyo vinatakiwa ama niseme mwekezaji anavihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuwaomba Waziri mwenye dhamana ya viwanda na biashara na Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji, kuhakikisha wanatenga eneo katika Kata ya Kwala kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. EPZA niwaombe sana tuache kuhangaika na maeneo ambayo yanahitaji fidia kwa wananchi, tunapozungumzia Kata ya Kwala pale wala hamuhitaji fidia, lile eneo lipo chini ya Serikali ambayo iko chini ya Wizara ya Mifugo, kwa hiyo Wizara ya Mifugo, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara ni watoto wa baba mmoja, wakae chini wazungumze waone namna bora ya kutenga eneo kwa ajili ya viwanda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana tena sana Mawaziri niliowataja waangalie namna gani wanahakikisha wanalitangaza eneo la Kwala kwa sababu lina kila kitu ambacho leo mwekezaji akija anapata kwa mara moja, maji yapo, umeme upo, barabara ipo, kila kitu kipo, kwa hiyo, nataka niwaombe sana tuliangalie eneo hili kwa sababu linaenda kuleta uchumi wa haraka sana, matokeo ya uchumi tutayaona haraka sana litachochea ongezeko la uchumi na kupunguza umaskini kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri, Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji, Jimbo lake ni Ubungo ambapo kimsingi akienda jimboni lazima atakatisha Mkoa wa Pwani na Waziri mwenye dhamana ya Viwanda na Biashara, Jimbo lake Masasi kimsingi akienda jimboni lazima atakatisha Mkoa wa Pwani. Kwa hiyo, niwaombe sana wakati wanaelekea jimboni wakishe pale kwenye ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani awapatie hiki kitu Pwani *Regional Investment Guideline*, ambayo imeeleza kwa undani, thamani na ubora na jinsi gani Kwala itakavyoenda ku-boost uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Mifugo ambayo kimsingi nimesema eneo kubwa la Kwala liko chini yao, nidhahiri Wizara ya mifugo wamehodhi eneo kubwa pale. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa maelekezo kwamba na sisi kama Mkoa wa Pwani tumeshaandika barua kuomba ekari 4,000 kwa ajili ya kuweka maeneo wezeshi kwa kupokea wawekezaji na kupokea viwanda. Tunahitaji hilo eneo la ekari 4000 kwa ajili ya ujenzi wa hoteli, benki pamoja na maeneo ya huduma za kijamii. Lengo na tija hapa kwamba *once* viwanda vinapokuja au wawekezaji wanapokuja wakute kila kitu kiko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine upo katika Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kama ambavyo nimetangulia kusema kwamba Mradi huu unakwenda ku-*boost* uchumi wa nchi yetu na nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uthubutu, umahiri na ujasiri, kimsingi hapa tuliwekewa vikwazo vingi kwamba kuna *environment impact assessment* na vikwazo vinavyofanana na hivyo kuhusiana na ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini leo hii Mheshimiwa Rais wetu amefanikisha, hivi tunavyozungumza *overall* ya Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa upande wa nishati wameshafika asilimia 30. Nampongeza sana Waziri Dkt. Kalemani, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa lipo jambo ambalo tunataka kuzungumza kama Taifa, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unaenda sambamba na miradi mingine mingine katika Wizara zingine. Nitazungumzia mfano mradi wa kupump maji, Wizara ya Maji hatujasikia chochote mpaka dakika hii katika mradi ule wamefikia wapi na wamefikia hatua gani. Pia Wizara yenye dhamana na kilimo tunazungumzia suala zima la kilimo cha umwagiliaji kwamba ndiyo maana nasema Wizara ya Maji kwa kupitia mradi ule wakiya-*pump* yale maji inamaana yataenda kuwanufaisha watu wa Kibiti, Rufiji, Mkuranga, Kisarawe na majirani zetu Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunapenda tusikie *status*, mpango ukoje kwa Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Kilimo, tunasema kilimo cha umwagiliaji. Imezungumzwa na Wabunge wengi humu ndani kwamba viwanda vinahitaji malighafi sasa kama watu wako tayari kwa ajili ya kilimo kikubwa cha umwagiliaji na mradi wa Mwalimu Nyerere unaenda sambamba na masuala mazima ya kilimo cha umwagiliaji, nini kauli ya Serikali mmefikia wapi katika ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yenye dhamana na Ujenzi na Uchukuzi, mradi ule unaenda sambamba na ujenzi wa barabara ya Kibiti - Mloka yenye kilometa 97. Vilevile mradi ule unaenda sambamba na barabara ya Kisarawe - Vikuruti ambayo ina kilometa 167 (*The Great Nyerere Road*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yenye zamana na Maliasili na Utalii, Wizara zote ambazo kimsingi kwa namna moja ama nyingine ziko katika Mradi wa Ujenzi wa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere tungependa kusikia kauli na mipango kwa sababu mradi ule wa nishati utakapokamilika uende sambamba na hii miradi mingine. Tumesema itakuwa kazi bure kama tutakuwa na viwanda, tutazalisha tutachakata, halafu tutakosa miundombinu ama barabara ya kubeba bidhaa hizo na kuzipeleka sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni shukurani, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna alivyotusaidia katika Kisiwa chetu cha Mafia kuhakikisha tunapata gati pamoja na kivuko maana ilikuwa adha kwa wafanyabiashara na kwa watu ambao wanachangia uchumi maeneo ya Mafia. Kwa sasa wamepata usafiri wa uhakika, kwa hiyo, wana nafasi nzuri ya kuchangia uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nipenda kutoa shukrani zangu kwa Chama cha Mapinduzi kwa kunipendekeza kuwa Mbunge wa Viti Maalumu kwenye Bunge lako la Kumi na Mbili pamoja na kuwashukuru wanaweke wa Mkoa wa Pwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa mchango wako. Tunaendelea na tunazidi kuona michango ilivyo mizuri, *fruitful* ambayo naamini kabisa inaujenga mpango wetu kuzidi kuwa mzuri zaidi. *Of course* kama Wabunge tunapaswa kuwa tunafikiri zaidi na zaidi. Wakati mwingine najiulizaga maswali ya kawaida tu lakini yanasumbua kichwa. Mara nyingi huwa namfuatilia Mheshimiwa Musukuma pamoja na mambo yake ya kisukumasukuma lakini mnajua uchumi wa nchi hii umeshikwa na darasa la saba? Ni kweli kabisa nikisema darasa la saba maana yake darasa la saba kwenda chini. (Makofi)

Hawa darasa la saba ndiyo wanaolima tumbaku, pamba, korosho. Ndiyo wanaofuga wasomi wangapi wanafuga au wanalima? Sasa hivi kila mtoto anayefaulu kila mahali, kata zote nchi nzima anakwenda sekondari na kila anayemaliza *form four* akili yake ni kwamba mimi nimeondokana na kilimo na ufugaji haendi kuchuga wala shambani kulima. Nyie mnasema tu tuzalishe mazao, lima hekari 1,000 za mahindi, fanya kila kazi, nani atavuna hizo hekari 1000 za mahindi? Kuna *form four* hata mmoja atakuja kukusaidia kuvuna pale? *We have a problem.*

Nchi inakwenda mahali ambapo huu uchumi wa kati kuna kundi kubwa la watu kwanza wavivu sana. Ni kweli, ni maeneo machache tu, kwa nini kila mama anataka *house girl* atoke Iringa asitoke Dodoma. Kwa nini mabinti wa Kigogo hawawi ma-*house girl* bali wa Kihehe, Iringa ni *very hard working*, wanachapa kazi sana. (Makofi)

Sasa ukiangalia hivi vitu unaweza kusema viwanda, huku kwenye kuzalisha yupo nani? Elimu yetu inawafanya hawa wapende hivi vitu vya kuzalisha au tunataka kudaka hapa juu? Ukitaka kudaka hapa juu mbona utabaki unaning'inia? Kwa hiyo, sasa tufanye nini hata mimi sijui lakini ni kweli kabisa kwamba tunatengeneza vijana wa kucheza

pool, ku-*chat* na simu, nafikiria Mheshimiwa Kakoso ulichosema tuongeze kodi huko labda itapunguza sijui. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwenye mpango hapa ni mahali tunapotakiwa tufikiri zaidi tuone nchi yetu tunaitowaje hapa ilipo, kabisa maana sisi ndiyo washauri wa kuu wa Serikali. Nchi kama zetu hizi Mheshimiwa Rais amejitahidi sana, anafanya kazi sana lakini wanaofanya kazi kwa kiwango chake yeye ni wachache mno, huo ndiyo ukweli. Tunawezaje kuifanya nchi ikawa *compartmentalize*, kila mtu akawa na kipande chake kazi na pakawa na *measure* za kuhakikisha anafanya kazi hiyo na hasa walioajiriwa Serikali ndiyo kabisa. (Makofi)

Utumishi, hivi tufanye namna gani tuhakikishe kila mtu kweli anafanya kazi, kwamba kweli mabwana shamba wa nchi hii wanafanya *extension work* na hawapokei mshahara wa bure. Kweli Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa wa vijijini wanafanya kazi gani? Ninyi Wabunge mliwahi kuwaona Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wanafanya kazi gani? Wanapokea mishahara tu na watumishi wengine wengi. (Makofi)

Inauma, unaangalia unaona sijui ufanyeje, ile *passion* ya kufanya kazi haipo. Hata timu yetu ya Taifa ikienda kucheza huko wachezaji hawajitumi yaani Watanzania hawafanyi kazi, hawajitumi. Huoni wakilitafuta goli kama wenzao wanavyofanya. Sasa tuna tatizo gani? Inabidi mahali fulani tubadilishe *attitude* ili vijana wetu hawa wachangamke kufanya kazi na wapende kazi. (Makofi)

Tunaendelea na Mheshimiwa Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Hhayuma.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyenijalia afya njema hata siku ya leo ikampendeza niwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru Mheshimiwa Rais lakini eneo kubwa nimpongeze, kwa kiwango kikubwa sana amefanya uwekezaji kwenye mtaji kama taifa. Mheshimiwa Rais anavyoelekeza jitihada kubwa katika ujenzi wa reli ya *SGR* anafanya *capital investment* (uwekezaji wa mtaji), anavyoimarisha bandari anafanya *capital investment*, anavyonunua ndege pamoja na jitihada za ujenzi wa Bwawa la Umeme la Nyerere anafanya uwekezaji katika mtaji. Maana yake nini? Maana yake Mheshimiwa Rais anatuandalia taifa ambalo miaka hamsini ijayo sisi akina Kunambi vijana wa leo na vijana wa kesho tutanufaika na mtaji huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba nimesoma mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Nianze kwa kusema mpango ni zao la malengo, unavyotengeneza mpango lazima uanze na lengo ambalo litakupa mpango, mpango utakupa mkakati, mkakati unakupa mbinu, mbinu zinakupa mafanikio. Unavyokuwa na mpango lazima ujiandae na mikakati na mbinu za kutekeleza mpango ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kidogo kwenye sekta ya kilimo na kaka yangu Mheshimiwa Bashe ni msikivu sana na naomba katika eneo hili anisaidie kidogo. Ukisoma ukurasa wa 88 mpaka 89 unaeleza habari ya sekta ya kilimo. Sote tunafahamu asilimia 65 ya Watanzania tunapata kipato kutokana na kilimo. Kama hiyo haitoshi kilimo kinachangia takribani 27% kwenye pato la Taifa na kati ya asilimia 27, asilimia 24 ni mauzo ya nje ya nchi na haya yameelezwa kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tuna kazi kubwa kwenye sekta ya kilimo, lazima tukubali. Kilimo chetu tunafanya *subsistence agriculture*, ni kilimo kwa ajili ya kula, *not for surplus is for consumption* kitu ambacho bado tuna safari ndefu sana. Nchi kama Tanzania yenye ardhi kubwa yenye rutuba lakini bado hatujaitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kwenda *training ya quality structure system* ya mwezi mmoja nchini Japan, nilishangaa sana. Nilikutana na *Vice President* wa JICA alinielea maneno haya kwamba Japan kwa mwaka mzima wananunua chakula kutoka nje ya nchi ikiwemo Afrika lakini aliitaja Zimbabwe, *why not Tanzania?* Kama kuna nchi imebarikiwa ukiondoa Kongo inafuata South Africa na Tanzania ni nchi ya tatu kwenye rasilimali za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itoshe kusema pamoja na kwamba tuna changamoto ya *funding* kwenye sekta ya kilimo, lakini tatizo siyo *funding* inawezekana tukafanya mageuzi makubwa sana kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Changamoto kwa Watanzania kuu ni tatu na siyo tu kwa *level* fulani, Watanzania wote tuna changamoto kuu tatu. Ya kwanza ni *mindset*. Marcus Garvey alisema neno moja, ukiwaza juu ya jambo lolote umeshindwa. Ukianza kwa kuwaza tu, mmh, nitaweza kweli umeanza kushindwa mapema na hutashida. Ni *mindset* kwa maana ya *positive thinking*. Ndiyo *challenge* tuliyonayo kwamba inawezekana, *yes it can be done*, kwa Mtanzania hiyo ni changamoto, unaanza kuwa na hofu kabla hujaanza safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili ni uzalendo, tulio wengi hatuipendi nchi yetu. Ndiyo maana utaona hata kwenye Utumishi wa Umma watu hawawajibiki. Ile *OPRAS* ningetamani iende kwa nafasi zote hata kwenye teuzi za Mheshimiwa Rais, kila mtu awe na *OPRAS*. Kama mtu anateuliwa apewe miezi sita hamna matokeo aondolewe tu. Unakuta kama ni Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa anafika anakuta kiti kilekile na analazimika kukaa kiti kilekile mpaka anaondoka hata kubadilisha kiti hawezi, hata kubadilisha mkao wa kiti hawezi, wengi tuna changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *commitment*, utayari juu ya jambo fulani. Itoshe kusema *I am not speaking from without, I am speaking from within*, nazungumza mambo ambayo nayafahamu. Naomba niseme hapa bayana lengo ni kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo kwenye suala zima la umwanguiliaji bado tuna changamoto.

MWENYEKITI: Bado la tatu, umetutajia mawili.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni *commitment* (utayari). Tuna changamoto ya uzalendo, pili *mindset* kwa maana fikra chanya, tatu ni *commitment*, haya mambo matatu ndiyo changamoto ya Mtanzania siyo fedha, hatuna shida ya fedha hii nchi ni tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya kilimo tunatakiwa kufanya mageuzi makubwa sana. Kaka yangu Mheshimiwa Bashe pale Mlimba, Kata yangu ya Mgeta ina shamba ya hekta 5,000 mpaka leo zimetokelezwa. Serikali imewekeza kuna miundombinu ya umwanguiliaji ndani ya hekta 3,000 na hekta 2,000 ndiyo bado na huu mradi hadi Baba wa Taifa miaka ya 1985 alipewa msaada na Serikali ya Korea lengo ni kuifanya Tanzania ipate uwezo wa kujikimu kwenye chakula. Ule mradi wamekwenda wajanja wajanja fulani mpaka leo umetelekezwa, Serikali imewekeza hekta 3,000 zina miundombinu ya maji ya kumwanguilia hekta 2,000 ndiyo bado, hiyo ni fedha ipo pale, tungeenda kule tungefanikiwa. Kaka yangu Mheshimiwa Bashe naomba nimpeleke pale Mgeta, Jimbo la Mlimba akaone jinsi gani Serikali inapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni sekta ya ardhi, tuna changamoto ya kodi lakini ardhi ya Tanzania inaweza kutupa fedha nyingi sana. Bado sekta ya ardhi haijafanya kazi. Naomba niseme bayana na Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri naomba mnisikilize. Nchi hii inaweza kupimwa, tuna halmashauri 185 lakini leo hii Wizara ya Ardhi hata kupima halmashauri 50 hatuwezi, kuna haja ya kuendelea kuwepo hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mfano bora, Dodoma hii tunayoona leo, ndiyo maana nimesema naeleza nachokifahamu, Dodoma hii miaka mitatu iliyopita ilikuwa haijapimwa. Mimi ni mfano, Jiji la Dodoma tumepima viwanja

2,000 bila kupata fedha benki wala ya Serikali Kuu. Tukipima nchi hii kwenye halmashauri zote kazi ndogo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze jinsi gani wanaweza kupima nchi nzima, Naibu Waziri ananisikiliza. Umesajili kampuni za vijana wa Kitanzania ambao wamesoma, wakajajiri, ukizipeleka zile kampuni zaidi ya 180, unazo Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye ofisi yako, zikapime kwenye halmashauri zote, ardhi ikipimwa ni mtaji tunaongeza wigo wa kodi. Nitasema kweli daima, kuna pesa tunaiacha kwenye ardhi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ndiyo maana nchi jirani, si mnajua tuna jirani nchi moja tu, tunazo nchi nyingi lakini moja ndiyo jirani zaidi, yule pale Kaskazini, ndiyo maana bajeti yao ni *twice comparing with ours* kwa sababu ardhi ya Kenya *all most* yote imepimwa ukiacha lile jangwa. Kwa hiyo, wanalipia *every year* ardhi yetu haijapimwa, nakuunga mkono. (*Makofi*)

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Anachoweza kufanya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ni jambo moja tu, kuna vijana waliosoma *land management* na amewasajili, anazo kampuni zaidi ya 180, leo hii ana-*discourage* kampuni zisipime nasikitika sana. Namshauri aruhusu kampuni za vijana hawa wakapime kwenye halmashauri zote nchini. Yeye kazi yake wale vijana wakipima ardhi ile mwananchi atapata hati miliki, atakopesheka, uchumi wake utakua, kama ni shamba atakopa mkopo benki atalima. Vilevile wigo wa kodi unaongezeka yaani *tax base* ya nchi inaongezeka. Hizi kodi tunazokusanya ni ndogo sana sekta ya ardhi peke yake inatupa utajiri wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kusema, leo nimesema maneno haya Mheshimiwa Naibu Waziri ikimpendeza kuna ule mfumo wa *ILMIS* awekeze pale, atafuta fedha awekeza kwenye mfumo, hizi kampuni binafsi ziende kwenye halmashauri zikapime. Waziri hana haja ya kupeleka fedha pale, hakuna haja ya hela, nimepima Dodoma viwanja 2,000 bila hela ya Serikali Kuu na kila mtu amepata ardhi hapa Dodoma viwanja bure inawezekana.

WABUNGE FULANI: Tunanunua.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Ndiyo unanunua lakini nimepima Dodoma karibia asilimia zaidi ya 50, kama kuna mbishi asimame hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kusema kama kweli tunataka kumsaidia Mheshimiwa Rais Wizara ya Ardhi ijitathimini. Kwa kiwango kikubwa tunataka nchi hii iwe tajiri. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kunambi. Baadhi mnaweza msiione *point* yake lakini ni ukweli halisi. Nchi hii ikipimwa, mashamba yote yakapimwa ile kodi ya ardhi tutakayopata nchi nzima ina *double* hii bajeti wala hatutakuwa na mawazo sijui tuongeze kwenye simu au *petrol*. Pia masuala yote ya migogoro ya ardhi, ooh, hifadhi sijui na nani, kila mtu akipimiwa anapata *beacon* zake sawasawa, ana hati yake, tutakuwa na maswali hayo hapa? Hatutakuwa nayo na ukishapimiwa utalipa kodi. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Samweli Hhayuma, utafuatiwa na Mheshimiwa Minza Mjika.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Mpango wa Tatu wa Taifa.

Niseme tu kwenye maelekezo yako umeni-*preempt*, nilitaka niongelee eneo la elimu. Wadau wengi wamezungumzia suala la mitaala yetu ya elimu kwamba tuna sababu ya kuangalia kama kweli elimu ambayo tunaenda nayo inaendana na mazingira yetu halisia. Tumesema sana lakini ukiangalia kwenye vyo vyetu tafiti nyingi zinafanyika lakini haziendi kutatua changamoto za wananchi. Maana yake wakati mwingine juhudi kubwa zinafanyika kwenye taasisi zetu za elimu lakini yale yanayopikwa kule hayajafiki kwa walaji ambao ni wananchi katika kutatua changamoto zao kwenye upande wa kilimo, mifugo na masuala mengine ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe ufike sasa wakati elimu ile tunayoifundisha isiwe inaowotoa wanafunzi au watu wetu kwenye maisha yao yale ya kawaida, bali iende kuimarisha maisha ya watu yale ya kawaida. Twende tukawasaidie wafugaji wafuge kisasa, hatimaye wapate tija. Siyo kama mtoto akienda shule...

MWENYEKITI: Upande huu kuna kelele sana, naomba tumsikilize Mheshimiwa.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Sio tukipeleka watoto wetu shule, tunawatenganisha na zile shughuli za asili ambazo tumekuwa tukizifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati nasoma shule ya msingi tulikuwa na Afisa wa Kilimo, alikuwa anafundisha kwa vitendo kwa wanafunzi na kwa wanakijiji, naye alikuwa anashika jembe la mkono, alikuwa anashika plau la kuvuta na ng'ombe na katika mazingira yaleyale ambayo watu wapo tuangalie elimu yetu kama inatuelekeza upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kwenye Vyu vyetu vya VETA mambo tunayofundisha ni yaleyale ya kila siku; je, tunaangalia mabadiliko ya maisha ya sasa? Je, tuna-*address* yale mambo ya msingi ambayo yatatuletea tija? Ukiangalia nchi yetu ina mifugo wengi, tunalima sana, lakini hapo tija inakosekana kwa sababu hatupeleki sayansi kwenye maeneo husika ili tuzalishe kwa tija ili hatimaye tunavyoongea Tanzania ya viwanda tubadilike kutoka kwenye kilimo, tuzalishe tupate mazao ya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinatumia ardhi, ardhi haiongezeki, Watanzania tunaongezeka. Baada ya muda kama elimu haiwezi kutusaidia waangalie ni namna gani baada ya muda kwa sababu ardhi tuliyonayo haiongezeki lakini sisi tunaongezeka. Kama haiwezi kututoa kwenye eneo hilo kuhakikisha kwamba elimu yetu inatatua changamoto za msingi na mabadiliko ya kila wakati jinsi tunavyoongezeka na ardhi haiongezeki tukatatua hiyo changamoto ya msingi

kwamba baadaye tutakuwa hatuna ardhi ya kutosha, hatuna maeneo ya kufuga mifugo, hatuna maeneo ya kulima. Je, elimu yetu itatutoaje kwenye changamoto hiyo? Lazima tujielekeze huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la ufugaji, hasa eneo la usindikaji wa bidhaa zinazotokana na mifugo. Tuna mifugo mingi sana lakini ukiangalia malori barabarani ukiona yamebeba mifugo, mingi tunasafirisha nchi za jirani. Tunasafirisha nyama, ngozi na mazao mengine. Hatuwezi kupata tija bila kuliangalia hilo eneo kwa makini. Ni lazima tujiwekeze kwenye kuboresha mifugo yetu. Tujiwekeze kwenye kuhakikisha kwamba tunakuwa na machinjio kwenye maeneo yale ambayo kuna mifugo wengi. Hatimaye tu-*process* vizuri tukatafute masoko nje badala ya kusafirisha mifugo ambayo iko hai. Hiyo inatupotezea na tunapoteza fedha nyingi kwenye eneo hilo. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo suala la miundombinu; hii imeongelewa sana. Hakuna namna tunaweza kupata maendeleo bila kuboresha eneo la miundombinu. Kazi kubwa imefanyika lakini bado tunayo kazi kubwa ya kuifanya. Lazima tutoke hapa tukiwa na jawabu. Kwa sababu ukiwa umelima, una mifugo, bila kuwa na uhakika wa kusafirisha na huduma nyingine za kijamii zinakuwa ni changamoto kubwa. Maeneo mengi barabara kwa sasa hazipitiki kwa sababu ya mvua. Lile suala la *TARURA* kutokuwa na bajeti ya kutosha, hilo eneo bila kuli-*address* hatuwezi kutoka, lazima tuje na jawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametolewa mapendekezo mengi. Tuache kwenda kama kawaida, lazima tuje na ubunifu kuhakikisha kwamba kwenye eneo hili tunapata fedha za kutosha na siyo kuchukua kwenye upande wa *TANROADS*. Nao wana majukumu makubwa ambayo ni ya msingi, hivyo, tuje na njia mbadala ya kupata fedha ilituboreshe *TARURA* ipate fedha za kutosha ili hatimaye watu wapate huduma za usafiri ulio...

MWENYEKITI: Sasa hapa tulipo Mheshimiwa *Engineer* ni mahali ambapo utuambie sasa tuzipataje hizo fedha? Yaani utoe mapendekezo.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, lazima tuwekeze kwenye maeneo yetu mkakati. Yameongelewa, eneo la upimaji wa ardhi ambalo nalo nataka niongelee ardhi peke yake, ni *sleeping giant* ambaye hatujavuna chochote kutoka huko. Ukiangalia kwenye eneo hilo hilo la upande wa ardhi, biashara za upangishaji wa nyumba hazijasimamiwa vizuri. Maeneo hayo kuna mapato ambayo yangeweza kupatikana kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kutosha. Tuangalie namna ya kuhakikisha kila tulichonacho tunaweza kukitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipima ardhi yote kila mtu akalipa kodi tukahakikisha kwamba biashara zote zinazofanyika za ardhi; za kuuza ardhi, za kupangisha nyumba na nyumba zote zikalipa kodi ile stahiki, tukisimamia maeneo hayo tunapata mapato ya kutosha.

Tuangalie namna ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha ili tuwekeze kwenye miundombinu ili hatimaye tuweze kufanya shughuli za uzalishaji kwa urahisi. Miundombinu inayopitika kwa urahisi ndiyo itakayotutoa kwenye mkwamo tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi maeneo mengi wananchi wanakwama kwenda hospitali, wananchi wanakwama kufanya shughuli za kimaendeleo kwa sababu barabara zimekatika na hii kila wakati inakula uchumi wa nchi, lazima tuje na jawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee kidogo eneo la umeme; kazi kubwa imefanyika, vimebaki vijiji vichache. Hata hivyo, ukiangalia kuna baadhi ya maeneo umeme umepita juu, kiasi kwamba wananchi wale wakishushiwa

gharama sidhani kama ni kubwa sana, itatusaidia katika kuchochea uchumi kwa kujenga viwanda vidogo na vya kati ili wananchi waweze kufanya shughuli za maendeleo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Samweli Hhayuma kwa mchango wako. Nilishakutaja Mheshimiwa Minza Mjika, utafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

Mheshimiwa Minza hayupo? Mheshimiwa Cecil Mwambe, naye hayupo. Mheshimiwa Daimu Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa siku hii ya leo kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mwaka Mmoja. Kwanza napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kurudi tena kwa awamu ya pili, lakini nawashukuru wapiga kura wangu ambao hawakufanya ajizi, wameona yale niliyoyafanya wakaamua kunichagua tena. Pia nitakuwa ni mchoyo wa fadhila bila kukishukuru Chama Cha Mapinduzi. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango nitachangia mambo mawili, jambo la kwanza ni suala la elimu. Kwanza niipongeze Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ikiongozwa na Rais wetu, jemedari, Mheshimiwa Dkt. Pombe Joseph Magufuli, kwa kazi kubwa aliyofanya kwenye Sekta ya Elimu. Naamini wengi tumeona mafanikio yaliyotokana na Sekta ya Elimu, tumetoka kwenye kuongeza shule za sekondari, kuongeza wanafunzi katika shule za msingi, vyuo pamoja na majengo na ukarabati wa miundombinu katika shule za sekondari na vyuo vikuu vilivyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili la elimu bure napenda tuone namna mpango unavyoweza kusaidia

shule za kata. Naamini wengi tuliotoka kwenye majimbo ya vijijini wanafunzi wengi wanasoma kwenye shule za kata. Ongezeko la wanafunzi kwenye shule za msingi limesababisha shule za kata ziwe na watoto wengi. Sasa miundombinu iliyopo kwenye shule hizi si rafiki sana ukilinganisha na shule zile ambazo zinahudumiwa na Wizara ya Elimu kama shule zile 89 ambazo zinafanyiwa ukarabati. Ndiyo maana hata ufaulu wake umekuwa wa kiasi kidogo sana ingawa zinajitahidi na watoto walio wengi kutoka vijijini wanasoma kwenye shule hizi. Naomba mpango ungeweka badala ya sasa kuendelea kukarabati naamini shule katika miaka mitano zimekarabatiwa zile kongwe, basi Serikali iangalie shule hizi za kata kuweza kuziongezea miundombinu ili zilingane na shule nyingine ambazo ziko katika mazingira mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia shule hizi nyingi wanasoma watoto wa maskini ambao wamejitahidi kujenga mabweni lakini watoto wanakwenda na vyakula shuleni. Naomba Serikali kupitia Mpango wa Miaka Mitano ijayo ijitahidi kuongeza ruzuku kwenye shule za kata ili watoto wanaosoma kwenye maeneo yale ambao wanatoka katika mazingira magumu kwenye kata zetu waweze angalau na wao kupata chakula kwenye shule hizi za kata ili kuwafanya watoto hawa waweze kufaulu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini watoto hawa kwa mazingira tunayoyaona wanafaulu katika mazingira magumu sana na ndiyo maana utakuta *private school*/wanafaulu vizuri zaidi kwa sababu wako kwenye mazingira mazuri, wanalala mahali pazuri, Walimu wengi wa sayansi, Walimu wa masomo mengine wako wengi na maabara za kutosha. Naomba mpango uangalie namna ya kuimarisha shule zetu za sekondari za kata ili miundombinu ya maabara, madarasa, mabweni, hata chakula Serikali iweze kutoa ruzuku kwenye shule hizi za kata waweze watoto wetu kusoma katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda nichangie sana suala la barabara. Ukizungumzia barabara ukweli

tunaishukuru Serikali, *Mtwara Corridor*, barabara kutoka Mtwara sasa imefika mpaka Nyasa. Tunaishukuru sana Serikali kwa kitendo hiki cha kutujali watu wa kusini kuhakikisha barabara hizi zimekamili na sasa unapiga lami kutoka Mtwara mpaka unafika Ziwa Nyasa na baadaye unapanda meli kwenda Malawi unakwenda Mbeya, unakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizi, tunaomba tukumbukwe *Mtwara Corridor* kwa maana ya Reli ya Kusini. Reli ya Kusini ndiyo *solution* itakayosaidia kuleta maendeleo Mtwara, Lindi na Mkoa wa Ruvuma. Leo Ruvuma kunapatikana makaa ya mawe Ngaka, yote yanasafirishwa kwa njia ya barabara. Utengenezaji au ukarabati wa Bandari ya Mtwara utakuwa na maana kama Reli ya Kusini itajengwa mpaka kufika Mbambabay ambako makaa ya mawe kutoka Ngaka yatatembea kwa njia ya treni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango kazi ambao unajengwa pale Mchuchuma na Liganga hauna maana kama hatutaweza kujenga Reli ya Kusini ili kusaidia uchukuaji wa mawe pamoja na chuma kutoka kwenye machimbo kwenda Bandarini Mtwara ambako bandari yake sasa inakuzwa kwa kiasi kikubwa ili kuhakikisha kwamba inahudumia huku mikoa ya kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara hii ya kutoka Mtwara mpaka Nyasa, kwa kweli kwa upande wa Kusini kupitia Mkoa wa Ruvuma hakuna barabara ya lami kwenda Msumbiji. Tunaomba barabara ya Songea kwenda Ngaka iwe ya lami na barabara hii ya Songea – Mokuru – Mkenda ijengwe kwa lami kwa sababu ndiyo njia pekee itakayosaidia kukuza biashara kutoka Msumbiji kuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara moja ya kutoka Mtwara Pachani – Nalasi mpaka Tunduru Mjini, tumeona iko kwenye ilani, tunaomba Serikali ndani ya miaka mitano hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuokoa mikoa hii ya kusini, hasa Wilaya ya Namtumbo pamoja na Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna barabara moja ambayo ninadhani nayo iingizwe kwenye ilani na iingizwe kwenye mpango ili isaidie watu wa Msumbiji kwa sababu watu wa Tunduru mambo yao mengi yanakwenda na watu wa Msumbiji kwa sababu tunafahamiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Tunduru Azimio mpaka Lukumbule mpaka Makande ambayo inamilikiwa na *TANROADS* nayo ingeweza kuingizwa kwenye mpango kuhakikisha kwamba barabara ile inajengwa kwa kiwango cha lami ili kuwahudumia wananchi wa Tarafa ya Lukumbule na wa Jimbo la Tunduru Kusini kwa ujumla kwa ajili ya kwenda Msumbiji kupeleka mali na kuchukua mali kutoka Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia ili niweze kutoa mawazo yangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Mpakate. Mheshimiwa Neema Mgaya, atafuatiwa na Boniventura Kiswaga.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mada hii. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunirudisha tena ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia niwashukuru wapigakura wangu, akinamama wa Mkoa wa Njombe kwa kunichagua kwa kura nyingi za kishindo na kuweza kurudi tena ndani ya Bunge hili. Vilevile nikishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuteua jina langu na kuniwezesha kuwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya ndani ya miaka mitano kuweza kutekeleza miradi mikubwa mbalimbali ndani ya nchi yetu, ukiwemo Mradi wa *Stiegler's*, ukiwemo Mradi wa *Standard Gauge*. Miradi hii itakwenda kuufanya uchumi wetu wa Tanzania kuwa uchumi mkubwa lakini vilevile uchumi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira yetu ya Tanzania ni dira ya uchumi wa viwanda ambao utakuwa shindanishi lakini vilevile jumuishi kwa maisha bora ya Watanzania. Nimeona Wizara wana mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba wanatumia malighafi mbalimbali zilizopo ndani ya Tanzania yetu ili kuweza kujenga uchumi imara na endelevu. Malighafi hizo zikiwa ni pamoja na malighafi ya uvuvi, malighafi zinazotokana na mazao, malighafi zinazotokana na madini na malighafi ambazo zinatokana na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kujielekeza kwenye malighafi ambazo zinatokana na madini. Kule kwetu Ludewa, Mkoa wa Njombe sisi tuna Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Kwenye mradi ule kuna takribani madini ya chuma pamoja na mengine tani milioni 128. Kama Serikali itaamua sasa kutekeleza mradi ule, tutakuwa na chuma kingi ambacho kitasaidia kama malighafi katika viwanda vya kutengeneza nondo, mabati, vifaa vinavyotumika kwenye madaraja na vifaa ambavyo vinatumika kwenye reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma, kama Serikali itaamua kuanza kuutekeleza tutakwenda kuokoa takribani bilioni 640 kwa mwaka ndani ya miaka 30 ya uhai wa mgodi huu wa Liganga na Mchuchuma, sambamba na kuweza kuzalisha ajira 35,000. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa muda wa miaka mingi tumekuwa tukiupigania, tumekuwa tukisimama, Wabunge mbalimbali wamekuwa wakisimama ndani ya Mkoa wa Njombe na Mikoa jirani kuiomba Serikali ianze kutekeleza Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma. Kwa sababu kama nia yetu ni kukuza uchumi wa Tanzania, mradi huu kama utatekelezwa utakwenda kuchangia Pato la Taifa *(GDP)* asilimia tatu mpaka nne. Naomba Serikali itusikilize ili iweze kutekeleza mradi huu wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie malighafi ambazo zinatokana na mazao kama ya mbao. Mikoa ya

Njombe, Songwe, Mbeya, Iringa, Rukwa, Katavi na Tanga ni wakulima wazuri sana wa mazao ya mbao. Naiomba sasa Serikali ihamasishe wawekezaji wa viwanda vya karatasi ili sisi Watanzania sasa twende kutumia karatasi zetu za hapa hapa Tanzania na kuhamasisha kufunguliwa kwa viwanda hivi vya karatasi. Hii itatusaidia pia kukuza ajira kwa watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashangaa sana kama ikiwa mpaka sasa hivi Serikali na watu wengine tunaendelea kuagiza *furniture* kutoka nje ya nchi wakati tuna Mageeza, JKT na wananchi ambao wana viwanda vya kutengeneza *furniture*, wanatengeneza *furniture* nzuri na zenye ubora kuzidi zile zinazolingizwa kutoka nje ya Tanzania ambazo nyingi ni mavumbi ya mbao, siyo mbao halisi kama zile *furniture* zinazotengenezwa hapa nchini kwetu Tanzania. Naiomba Serikali, i-*discourage* uingizaji wa *furniture* kwa kuweka kodi kubwa katika bidhaa hii na kupunguza gharama za kodi katika *raw materials* kama msasa na zile *accessories* ambazo zinatumika kunakshia *furniture* ili kuchochea uanzishwaji wa viwanda vingi vya *furniture* ndani ya Tanzania yetu na kuweza kukuza uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa nimejipunja sana kama sitazungumzia malighafi ya zao la parachichi ambalo liko ndani ya Mkoa wangu wa Njombe. Halikadhalika Songwe, Iringa, Katavi na mikoa mingine ya Tanzania wanalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali imefanya jitihada kubwa sana ya kuweza kuwasaidia wakulima wetu wa parachichi kuweza kusafirisha parachichi nje na kuuza ikiwa ghafi. Naona ni wakati sasa Serikali ijikite katika kuhakikisha kwamba inahamasisha viwanda vinavyotengeneza *cosmetics* inayotumia malighafi ya parachichi kama *conditioner* ya nywele au *lotion*, majani ya parachichi unaweza ukatengeneza asali au dawa. Serikali ihamasishe viwanda hivi vya kutengeneza *cosmetics* ambayo inatokana na malighafi ya parachichi, viwekezwe kwa wingi nchini wakati huo tukiendelea kuhamasisha wakulima

kuendelea kulima parachichi kwa wingi. Kwa kufanya hivyo, itasaidia pia kuongeza ajira kwa viwanda hivi ambavyo vitaenda kufunguliwa ndani ya mikoa yetu hii ya kulima parachichi na kuweza kukuza uchumi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuzungumzia malighafi inayotokana na wanyama. Naipongeza Serikali kwa jitihada mbalimbali inazochukua kuhakikisha wameweza kuhamasisha na ku-*convince* viwanda mbalimbali vinavyotumia ngozi kutengeneza mikoba, viatu na mikanda. Naomba tusishie *leve*/hiyo ya kutengeneza tu viatu, mikanda na mikoba, hebu tuige kwa wenzetu wa Ethiopia. Wao ndio wanao-*supply* ngozi katika Kampuni ya *Mercedes Benz* kwenda kutengeneza zile *seat cover* zake. Naomba Serikali ifikirie katika mlengo huo, hii yote ni katika kuweza kukuza pato la Taifa letu na uchumi wetu na kuufanya uweze kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Kilimo. Juzi hapa Mheshimiwa Hussein Bashe alizungumza namna bora ya kuboresha mbegu ili tuweze kupata malighafi nyingi kwa kuwa na mbegu bora katika masuala mazima ya kilimo. Haitoshi, inabidi Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Viwanda, baada ya kuwa Wizara ya Kilimo inaweka mikakati mizuri ya kuboresha mbegu zetu ili kuweza kupata malighafi bora na kuongeza mavuno, inabidi Wizara ya Viwanda ikae makini katika kuhakikisha kwamba malighafi hizo zinazotokana na kilimo zinatumika hapa hapa Tanzania katika kuchochea viwanda, kwa kuhamasisha viwanda vingi kufunguliwa ndani ya nchi yetu na kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya. Mheshimiwa Bonaventura Kiswaga, hayupo.

MBUNGE FULANI: Yupu.

MWENYEKITI: Ahsante. Baada yako nitamwita Mheshimiwa Salome Makamba achafue hali ya hewa kidogo. Mheshimiwa Kiswaga. *(Kicheko)*

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Mpango wa Mwaka Mmoja na Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo amewasilisha mafanikio ambayo yamefikwa kwa miaka mitano iliyopita na matarajio ya miaka mitano ijayo. Inatupa faraja kwamba nchi hii tutasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere huko nyuma alitangaza Kilimo cha Kufa na Kupona, wengine sasa wamekuja na *slogan* nyingi. Kusema ukweli wananchi wengi walioko vijijini wanahusika na kilimo, lakini kilimo chetu hiki ni cha kutegemea mvua wakati Mungu ametupa ardhi yenye maji chini. Ni vizuri Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo zikaja na mpango wa kila eneo kuliko na shamba tuchimbe visima virefu, tusafishe maji, tusukume, tutengeneze miundombinu ya umwagiliaji ili wakulima wetu waweze kulima kwa awamu karibu tatu kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri sana wakulima kulima miezi minne wanapumzika miezi nane, kibiashara haikubaliki. Mfanyabiashara halisi hupenda kufanya biashara kila siku bila kupumzika. Tumpeleke mkulima wetu afanye biashara, kwa sababu kilimo ni biashara, ndipo tutafikia kipato cha juu kwa kila mwananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ni mawazo ambayo yanapaswa yaanze sasa. Kwa sababu tumezungumza sana miaka mingi, Bunge hili litaisha, Bunge lijalo litaisha na mengine. Ni vizuri mipango hii ikaanza kutekelezwa kwenye uongozi wako, tukaacha *legacy* kwenye kilimo cha wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote ili Mpango wa Maendeleo ufanikiwe, ni lazima wananchi na viongozi wake wawe tayari. Kwa nchi yetu ya Tanzania viongozi wako tayari na wananchi wako tayari kwa sababu wakati wote wanawajibika kikamilifu, kwa hiyo, ni mambo tu ambayo tunatakiwa tufanye. Tulipokuwa tunaandaa mazao matano ya kimkakati, ni vizuri tukaandaa na viwanda vya kimkakati ili kuhakikisha kwamba tunakuza uchumi wa kilimo na kukuza ajira kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la pamba. Kulikuwa na Mpango wa *C2C (Cotton to Clothes)*. Mpango huu hauwezi kufanikiwa kama Serikali haitaamua yenyewe kuwezesha sekta binafsi kama dunia ilivyoweza kuwezesha sekta binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, unapotaka kutengeneza kiwanda cha majora, yaani vitambaa vya aina mbalimbali kama kitambaa cha suti, kitenge, kanga, *jeans*, *t-shirt* au shati, unahitaji uwekezaji usiopungua Dola milioni 100, kwa sekta binafsi haiwezekani. Dola milioni 100 tunazungumzia shilingi bilioni 230, benki zinaweza ku-*collapse*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea ziliwezesha sekta binafsi. Ukienda Bangladesh, pamba yetu ya Tanzania inaliwa na kiwanda kimoja tu. Kweli tunavyo viwanda vidogo vidogo hivyo vya nyuzi, vitambaa, haviwezi kumaliza *raw material* tuliyonayo hapa. Kwa hiyo, ili tukuze uchumi ni lazima Serikali iweke *guarantee* kwa sekta binafsi ziweze kukopesheka duniani ili tuweze kuwekeza na tutoe majora ya aina mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoa majora, kwanza tutakuwa na uhakika wa bei halisi ya pamba. Kwa sababu mnyonyoro wa thamani tutaujenga vizuri ili kuhakikisha kwamba mkulima huyu ananufaika. Ndipo tutakapokwenda sasa kwenye viwanda vya nguo ambavyo vilikuwa vinazungumzwa hapa na wenzangu, kwamba mtu mwenye cherehani tano au nne, hivyo ni viwanda. Ukienda Vietnam, kila familia ina kiwanda nyumbani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tubadilishe mawazo yetu, NEMC ije na mawazo chanya. Kwa sababu hapa kwetu ukitaka kuweka kiwanda kwenye nyumba yako unaambiwa unaharibu mazingira. Ukienda China unakuta familia moja, chumba kimoja inatengeneza mabegi; familia moja chumba kimoja inatengeneza simu; ndipo sasa utaweza kwenda kwenye viwanda vikubwa. Huwezi kuanzia juu ukaja chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yetu iweke *guarantee* kwa wale walio tayari, kama sivyo, Serikali tu-*sacrifice*, shilingi bilioni 230 ni nini, tuipe Jeshi lijenge kiwanda kikubwa, wafungwa waendeshe kiwanda, watoto wa JKT waendeshe kiwanda, tutafikia uchumi ambao tunautarajia. Kama hatutafanya hivyo, tutakuwa tunazungumza pamba ambayo haitusaidii sana, tunaagiza nguo kutoka nje na pamba tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali, lazima iamue, tunajenga madaraja na barabara...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga nilitaka kukukumbusha tu kwamba sasa huo ndiyo uchangiaji wa Mpango. Ile habari ya barabara ya kutoka mahali fulani kwenda kwenye kijiji changu, hiyo subirini wakati wa bajeti. Sasa hivi tueleze Mpango, ili mpango huu ukatuletee hela Serikalini, Serikali iwe na fedha halafu sasa ndiyo tutaongea habari ya barabara yako ya kata moja hadi nyingine. Kama unavyotueleza kwamba tukiwekeza kwenye pamba tunaweza tukatoka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Kiswaga, endelea. *(Makofi)*

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunajenga barabara, madaraja, stendi na masoko kadhaa, kwa nini Serikali isiamue kutoa shilingi bilioni 230 ikakabidhi hata Jeshi kama sekta binafsi haiaminiki, hapo sisi tutakuwa soko la Afrika kwa vitambaa na tutamaliza matatizo mengi. Wale wakija kununua vitambaa, watalala hoteli, kuna kodi ya Serikali; watakunywa bia, kuna kodi ya

Serikali; watatumia *taxi*, watatumia mafuta, kuna kodi ya Serikali; wenye *taxi* watanunua tairi, kuna kodi ya Serikali. Kwa hiyo, tusiangalie tu jambo moja tukashindwa kuangalia kwa upana wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wowote wa Maendeleo duniani huhitaji kuongeza ajira, kukusanya kodi na kuweka mifumo mizuri ya kuhakikisha mpango ule unatekelezeka. Kuna wakati taasisi zetu wakati mwingine zinaweka mipango ambayo haitekelezeki na kandamizi. Mfano, wenye mabasi; kuna kitu kinaitwa *LATRA*, wameingizwa kukata tiketi kwa mfumo, ambapo kimsingi wanalazimishwa kuweka fedha kwenye mashine. Kama una magari 40 lazima asubuhi uweke milioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wafanyabiashara wetu wa mabasi wana uwezo, kwanza basi wanakopeshwa, halafu unapoweka huo utaratibu, maana yake kuna 2% wanakatwa hawa wafanyabiashara. Hiyo pia, hakuna mkataba wowote ambao unawafanya wafanyabiashara hawa wawe na imani kwamba fedha hizi zikikatwa kwa mtandao zitarudi au zitaenda Benki?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ni kengele ya pili.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Ni hoja muhimu lakini muda wako umekwisha.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wapewe *EFD machine* wafanye kama ambavyo wafanyabiashara wengine wanafanya bila kupitia utaratibu huo. Hapa tutaongeza ajira, Mama Ntilie watapika chakula, wapiga debe nao watafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. Tutachangia kwenye Mipango mingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga, huja-*declare interest*, una mabasi mangapi? *(Kicheko)*

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina basi ila kwenye pamba.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye anauza mafuta kwenye mabasi.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ningeshangaa, maana Wasukuma ninyi hamna mabasi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Salome atafuatiwa na Mheshimiwa Eric Shigongo.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na wa Mwaka Mmoja. Wamezungumza wengi lakini mimi napenda nianze kwa kutafuta tumekwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nasoma Mpango huu wa Tatu wa Serikali ilibidi nirudi nyuma niangalie Mpango wa Pili na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo. Ukiangalia Mpango wa Pili wa Maendeleo ambao ndiyo tunaumaliza, Serikali kwenye eneo la ukuaji wa uchumi, ilikuwa imepanga kukuza ukuaji wa uchumi mpaka asilimia 10 ifikapo mwaka 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoanza tu ule Mpango mwaka 2016 tulianza na 7%. Tulipoanza tu Awamu hii ya Tano 2016 tukaporomoka kutoka 7% mpaka asilimia 6.8. Tukajipanga vizuri, mwaka uliofuata mwaka 2017/2018 tukarudi asilimia 7%. Hivi ninavyozungumza, tangu Awamu ya Tatu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kiwango cha ukuaji wa uchumi kimebaki 7%. Tafsihi yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba ukuaji wa uchumi katika nchi yetu ya Tanzania umesimama tangu mwaka 2001. Kwa maana hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye Mpango wa Kwanza, Mpango wa Pili tumeshindwa kufikia angalau *target* ambayo tumejiwekea wenyewe ya asilimia 10 ya ukuaji wa uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *target* hii iko kwenye Mpango, yaani Serikali wamejipangia wenyewe. Ni sawa na mtu unaenda kuposa ukaambiwa jipangie mahari; ukasema nitatoa Sh.50,000/=. Haya basi lipa, halafu unasema sina. Hapo sasa ndipo tunapoanza kukwama kwenye Mpango wa kuwasaidia wananchi kuwatoa kwenye umasikini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye pato la kila mmoja. Kwenye Mpango wa Pili ambao ndiyo tunaumaliza, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ilisema itahakikisha Mtanzania anaongeza pato lake mpaka Dola 1,500 kwa mwaka ifikapo mwaka 2021. Wakati huo inaingia Awamu ya Tano, kipato cha mmoja mmoja kwa Mtanzania ilikuwa ni kama dola 1,043 na kasi zote, makofi yote na ngonjera zote tunazozipiga, tumejivuta wee, kutoka Dola 1,043, tumefika Dola 1,080; tumeongeza Dola 37 kwa mwaka. Yaani shilingi tuseme kama 6,000/= hivi kwa mwezi kwa kila Mtanzania yaani hizi kelele zote tunazosisikia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kwa miaka mitano tumeweza kuongeza Dola 37 tu kwenye pato la Mtanzania mmoja mmoja, tafsiri yake, ili tufike kwenye *target* ya Dola 1,500 kwa kila Mtanzania, tunahitaji miaka 60. Hiyo ndiyo tafsiri. Kwa sababu miaka mitano tumeongeza Dola 37, tukiongeza miaka mitano mingine tutafika Dola 74 au tutashuka, hatuwezi kujua. Kwa sababu ikiisha hii kumi, hatujui atakayekuja atakuwa na kasi gani? (*Kicheko*)

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome kuna Taarifa upokee. Nilishawaambia hali ya hewa itachafuka hapa. Naona dalili za mawingu. (*Kicheko*)

Ni Mheshimiwa nani? Ni Mheshimiwa Kingu, karibu.

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe dada yangu Salome Taarifa kwamba, ukuaji wa uchumi na suala zima la *per capita income* lazima lijengewe *base* ambazo zikisha-*mature* zitakwenda kuleta *spill over impact* kwa *individual citizen*. Uwekezaji unaofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi katika kuwekeza katika Sekta ambazo zitafanya *transformation* kwa mfano Sekta ya Umeme, Miundombinu pamoja na Miundombinu ya Kilimo hicho wanachokisema cha mwaka mmoja kukua kwa hizo dola anazoitaja ni upotoshaji. Nataka nimhakikishie Tanzania na uchumi wake utakwenda kubadilika kulingana na mipango Madhubuti ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Salome unaelimishwa kwamba hiyo hesabu yako inaweza ikawa hivyo kwa ile lugha ya wenzetu *if everything remains constant*. Sasa nani kakwambia tunakokwenda ni *constant*? Kwa uwekezaji anaousema kutakuwa na *faster growth*. Unapokea Taarifa hiyo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Kingu atulie. Tujadili haya mambo, Mheshimiwa Rais ana mategemeo makubwa sana na Bunge hili, tujadili haya mambo tumekwama wapi halafu nitashauri tunatokaje tulipo. Ndiyo maana nikasema kama tumeongeza dola 37 kwa pato la mtu mmoja kwa miaka mitano. Itatuchukua miaka 60 ili tufikie malengo ya pato la mtu mmoja liweze kufika dola 1500. Hapo sasa, *if all factors remain constant*, hapo ndiyo tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili jambo hili linasemwa uchumi wa kati, watu wanasema hela hatuna mfukoni na ni *very confusing* na nashauri tu Wabunge tupewe semina ya uchumi wa kati unavyotakiwa ku-*reflect* pesa zilizoko mifukoni mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kiwango cha umaskini nchini, Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi hasa Serikali ya Awamu ya Tano wakati inaingia madarakani iliahidi kupunguza kiwango cha umaskini kwa asilimia 11.5, kwamba watatutoa kwenye kiwango cha umaskini kutoka asilimia 28.2 mpaka asilimia 16.7. Sasa mpaka tunamaliza mpango huu wametutoa asilimia 28 mpaka asilimia 26 na pointi, sawa na asilimia 1.8. Sasa nina lengo kubwa sana la kuisaidia hii Serikali na mimi bado ni kijana. Kwa mwendo huu tunaokwenda nao kuna mawili; ama hatuwapi nafasi wachumi wetu kutushauri vizuri tuweze kuwa na mpango unaoendana na uhalisia au tunamwogopa Mheshimiwa Rais kumweleza ukweli, tunaamua kumpamba kwa maneno mazuri lakini kiukweli hali ya kiuchumi ni mbaya. Kuna hayo mawili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kusema tumekuja kwenye uchumi wa kati, wananchi hawalielewi kwa sababu hali ya umaskini katika nchi hii ni kubwa. Ni zaidi ya asilimia 26.2, kwa hiyo ukisema tumeenda kwenye uchumi wa kati wakati watu bado ni maskini lazima watu wachanganyikiwe. Matokeo yake, tunavyo-*promote* kwamba tuko kwenye uchumi wa kati, tunajitoa kwenye *level* ya nchi inayostahili misaada...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome ngoja upewe Taarifa kidogo. Jitambulishe.

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kingu.

MWENYEKITI: Aaa, bado Mheshimiwa Kingu unaongea tena.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa dada yangu Salome.

(Hapa baadhi ya Wabunge walzungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Naomba mtulie *this is democracy*. Naomba kumpa dada yangu Salome Taarifa kwamba nchi kuingia kwenye uchumi wa kati kuna *stage*. Naomba dada yangu Salome atulie asome *principles* za ukuaji wa uchumi na masuala mazima ya *global economy*. *Stage* za nchi kuingia katika uchumi wa kati haimaanishi kwamba tumeshafika katika *barya juu ya per capita income of individual* na hicho ndicho Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inajenga misingi sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeingia katika uchumi wa kati, tuko katika *class* ya chini, ndiyo sasa hivi tunajenga mipango hapa kutaka kuijenga nchi na kupeleka kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome pokea.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Taarifa siipokei na kwa sababu ya muda, naomba niendeleo na Mheshimiwa Kingu naomba utulie kidogo, acha hayo mambo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali tuliyonayo ya kiuchumi mifukoni watu hawana kitu ndiyo inayosababisha watu wasielewe maana ya nchi kuingia katika uchumi wa kati na kwa maana hiyo hata Serikali yenyewe imechanganyikiwa kwenye hilo. Tumeingia kwenye uchumi wa kati tunajisifu. Nchi ikishaingia kwenye uchumi wa kati inaingia kwenye *class* ya nchi ambazo kuna baadhi ya mambo lazima tukose, tutakosa misaada mbalimbali, misamaha mbalimbali ya kikodi, *scholarship* za wanafunzi. Tunajikuta kwa sababu ya kukosa, kwa sababu tuko kwenye uchumi wa kati...

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Kimei. Mheshimiwa Salome subiri Mheshimiwa Kimei...

T A A R I F A

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naomba niseme hivi,

fedha iliyo mfukoni haihesabu kama wewe ni tajiri au sio tajiri. Kitu kinachohesabika ni kuna fedha unayopata wewe kama kipato chako, mshahara au umeuza mazao yao inaingia mfukoni kwako unalipa na kodi na kadhalika. Kinachojalisha sana ni zile huduma unazopata kutoka Serikali za bure. Huduma za bure kama elimu, watoto wanasoma bure. Hiyo shilingi ambayo ulikuwa ulipie mtoto wako anaenda shule si umeweka mfukoni? Unaibakiza mfukoni kwako. Ukipata matibabu ambayo yana ruzuku si hela inabaki mfukoni ya ziada? Ukipanda gari ambalo ulikuwa ulipe shilingi 1,000 ukalipa shilingi 500 kwa sababu barabara ni nzuri si hela inarudi mfukoni, si utajiri unaongezeka? Utajiri hautokani na ile hela ambayo lazima uwe nayo. Tuangalie pia kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imetupa huduma gani za ziada ambazo hazilipiwi na ambazo zinarudisha fedha zetu mfukoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe angalizo moja. Fedha ambayo tunapewa inaenda moja kwa moja kwenye huduma hizi inasaidia zaidi kwa sababu kuna wengine walikuwa wanapata hela wanakunywa tu. Hata hawapeleki watoto shule, wanaacha shule. Sasa watoto wale wanaenda kwa hiyo inakuwa kwa *welfare of the society* ni kwamba hiyo inakuwa ina-*contribute* sana. Tusiangalie tu hela ya mfukoni, hela ya mfukoni haina maana! Hela ya mfukoni *is not so much important*. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kimei. *Actually*, ndiyo maana alisema kwamba Wabunge tunahitaji semina. (Makofi)

Mheshimiwa Salome malizia.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze tu kwenye hilo neno lako ulilolisema, kwanza Taarifa siipokei na awe makini sana kwa sababu ni Mbunge wa Jimbo, unaposema tusiangalie tu hela ya mfukoni tunaongelea habari ya hali ya wananchi kuweza kufanya manunuzi ya bidhaa. *Per capita income* watu hawana hela. Serikali inajinasibu iko kwenye uchumi wa kati kuna watu

wako Muamalili kule Chibe hawawezi ku-*afford* kununua kilo moja ya unga, yeye alikuwa Mkurugenzi wa CRDB, tunaongelea wananchi maskini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Sasa naomba nimlinda ili amalizie na sababu yake ni kwamba ni katika walio wachache na wao kutwa nzima ya leo wanachangia wawili tu. Kwa hiyo tuvumilie kidogo tusikilize mawazo ya upande wa pili. (Makofi)

Kwa hiyo, Salome nakupa dakika tano ili umalize sasa. (Makofi)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nishauri yafuatayo: Wameleta mapendekezo ya Mpango. Warudi nyuma kuanzia mapendekezo ya Mpango wa Kwanza na wa Pili kwa sababu tumekwambia hapo. Warudi nyuma wakaangalie tulikosea wapi, kwa nini tuli-*project* kufika asilimia 10 na tumekwama kwenye saba tangu 2001 katika hali ya uchumi. Warudi hapo. Hiyo ni mosi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni lazima turudi kwenye mfumo shirikishi wa kiuchumi. Hatuwezi kuishi kwenye Serikali ya matamko, hatuwezi kuishi kwenye Serikali ya miongozo. Ni lazima wananchi, Sekta Binafsi na Serikali tushirikiane kwenye kukuza uchumi na nitatoa mifano miwili. Mfano kwa kwanza ni kuhusiana na hivi vitambulisho vya wajasiriamali. Yalitoka matamko hapa, *presidential proclamation* kwamba vitambulisho view shilingi 20,000 vikakusanywe. Jambo hilo halikueleweka. Tukienda kwenye *hansard* Wabunge waliomba ufafanuzi lakini kwa vile ilikuwa *your wish is my command*, lilikwenda, limekwama! Sasa wamelirudisha mwongozo kwenye Wizara. Mwongozo kwenye Wizara unasema Halmashauri zikatekeleze, wakatekeleze kwa

mfumo upi? Ule ule wa Mgambo kupiga mama zetu ili wachangie 20,000? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unayo *power* ya kuagiza sheria hii iletwe Bungeni ishirikishe wadau, ifanyiwe *scrutinzation* ili iweze kuendana na mfumo halisi wa maisha ya Watanzania. Mfumo huo huo uko kwenye kodi za mabango na majengo. Walitoa kwenye Halmashauri, Halmashauri zika-*paralyse*. Sasa hivi wamewarudishia lakini kimsingi hawajarudisha, ni vile hawana *manpower* ya kukusanya zile pesa wamepeleka *local government* zikusanywe, zinaingia kwenye mfumo wa *control number* zinaenda Hazina kurudi kwenye Halmashauri ni mtihani. Kwa hiyo lazima tuwasikilize wananchi, lazima Serikali isikilizwe na wananchi ni Bunge. Kabla hawajaenda kwenye hatua hiyo sisi wawakilishi wa wananchi ni lazima tushiriki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, mapendekezo yangu. Iko haja ya kutengeneza Kamati Maalum ya Bunge itakayofuatilia ahadi za Serikali na Viongozi Wakuu wa Nchi hii. Leo Waziri kanijibu hapa, bahati nzuri ulikuwa kwenye Kiti namuuliza ni lazima tupunguze ajali za barabarani, ni lini utaleta marekebisho ya sheria ananiambia sheria iko njiani amefunga makaratasi ameondoka! Sijui njiani ni Kibaigwa, sijui ni Manyoni, hakuna *commitment!* Watu tuko *serious, we are using brain*, watu wanafanya siasa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili Bunge lako ni Bunge makini, Mawaziri wageni mjue tunahitaji, na Kanuni zinasema lazima swali la Mbunge lijibiwe kikamilifu. Tutengeneze Kamati Maalum ya kufuatilia ahadi za Serikali na Viongozi Wakuu. Sasa hivi kila Waziri hapa anasema tutaongozana kwenda Jimboni kwako wanaenda kufanya nini, hatujui. Wakienda wanafanikisha hatujui. Tunataka tufahamu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho na sio kwa umuhimu, Mheshimiwa Mpango mwenyewe amesema kwamba ili tufanikiwe Mpango huu lazima tuwe na utawala bora lazima tuwe na amani, lazima tuwe na utulivu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome na Mawaziri wanatakiwa wafuatane nao ni Mawaziri wanawake tu. *(Makofi/Kicheko)*

Malizia hoja yako dakika tano zinaisha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema lazima tuwe na utawala bora, tuwe na amani, tuwe na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayako sawa! Ni kwamba yametulia tumetoka kwenye uchaguzi. Yaliyotokea kwenye uchaguzi mnayajua, hatuwezi kuka kimya. Tutengeneze Tume ya Umoja ya Maridhiano ya Kitaifa. Tukatibu vidonda vya wananchi. Mimi nimefanya kazi ya mahusiano ya jamii. Miradi yoyote itakayokwenda kutekelezwa na Serikali kwa wananchi wenye vinyongo lazima ikwame! Twendeni tukatibu magonjwa. Kuna watu 50 hapa wamepita bila kupingwa kwenye Majimbo, wapo humu! Miradi mikubwa imeelekezwa kwenye majimbo yao unategemea utekelezwaji wa miradi ile utakwendaje? Lazima tutoe vinyongo, watu waseme tuyamalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe unajua... kumtangaza Bwana mdogo pale ilibidi waniweke jela, nina kinyongo.... *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Spika, muda wako umeshaisha, muda wako umekwisha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Muda wako umeisha Mheshimiwa Salome. *(Kicheko)*

Nilijua tu hawezi kumaliza bila kumchokoza mtu hapa. Usiwe na wasiwasi watu wanapumua kidogo, maana kipigo alichopata kilikuwa kikubwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Eric Shigongo na atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kusimama tena ndani ya Bunge hili Tukufu kutoa mchango wangu ndani kwa Taifa langu. Naomba tu niishukuru sana familia yangu, wapiga kura wangu kwa kazi kubwa waliyofanya kunileta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa matumaini. Najua nasikilizwa hap ana watu hapa ndani, lakini najua nasikilizwa na Watanzania sehemu mbalimbali ya nchi yetu. Naomba tu niseme hivi, nina matumaini makubwa kwa nchi yangu leo kuliko ilivyokuwa jana. *My hope for this country is greater today than it was yesterday.* Nataka niwaambie Watanzania wanaonisikiliza kwamba tunakokwenda ni kuzuri sana.

Sasa nina bahati ya kuwa hapa ndani leo, tangu nimeingia nasikiliza watu wanaongea, nasikiliza napata muda wa kujifunza. Namshukuru Mungu niko hapa ndani nashiriki, zamani nilikuwa nawaangalia mnaongea nikiwa nje. Najifunza kitu kimoja kikubwa sana. Ukiwa hapa ndani kuna wakati uweke *fence* kwenye akili yako, ujiwekee *fence*, useme hiki hakiwezi kuingia kwenye kichwa changu, hiki kinaweza kikaingia maana kuna mtu anaongea kitu halafu najjuliza hivi huyu hajui yanayoendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inakua, tena inakua kwa kasi! Nani hajui tulipotoka? Nani hajui?

TAARIFA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge Eric Shigongo anayeongea kwamba katika Bunge hili sisi tuko kwa niaba ya wananchi tunatoa mawazo yetu na ya wananchi, kwa hiyo pana uhuru wa mawazo yote tunayoongea ni sahihi mahali hapa. Mwisho wa siku tunakuja na kitu kimoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shigongo hajamtaja mtu, endelea tu.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo sijaipokea kwa sababu sijamtaja mtu yeyote. Nataka niwaeleze Watanzania na niwaeleze watu wote walioko hapa ndani kwamba mnapoamua kujenga uchumi kuna *transition period*. Kuna kipindi cha mpito lazima mpite. Hata ukisoma historia ya China wakati wa Mao Tse Tung kulikuwa na kipindi kigumu sana walikipitia wale watu hatimae wakafika walipo leo. Yawezekana tunapita lakini tumeshaanza kupita kwenye *transition* hivi sasa mambo yanaenda kuwa safi. Nataka kuwaambia Watanzania wanaonisikiliza kwamba ya kwamba wawe na matumaini, wawe na imani na kiongozi wetu mkuu, wawe na Imani na Bunge hili ya kwamba tunakokwenda ni kuzuri na kazi inafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nichangie Mpango wa Mwaka mmoja na wa Miaka Mitano. Nasema hivi; nitachangia eneo la *digital economy*, uchumi wa kidijitali. Eneo la viwanda na nikipata nafasi nitachangia eneo la mitaala yetu ya elimu kwa ajili ya watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia nizungumze mambo matatu tu ya muhimu kwamba *we are a blessed country*. Tanzania kama Tanzania ni nchi iliyobarikiwa sana. Kuna mtu alisema kwamba Mungu wakati anaumba dunia inawezekana siku ya saba alikuwa yuko Tanzania, maliasili zote aliziacha hapa wakati anakung'uta kung'uta mavazi yake ili arejee alikung'uta kila kitu akaacha hapa. Kaacha gesi, makaa ya mawe, almasi, dhahabu na kadhalika. Wakati anaondoka wanasema akadondosha *handkerchief* yake pale Arusha kadondosha *Tanzanite* pale haipo sehemu nyingine duniani. *This is a blessed country*, tukusanyikeni hapa tuzungumze namna ya kutumia utajiri wetu kupeleka Taifa letu mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kulizungumzia ni uchumi wa kati. Hatujafika kwenye uchumi wa kati

accidentally, hatujafika kwa bahati mbaya. Kuna mambo tuliyafanya yametufikisha hapo. Mambo hayo tuliyoyafanya tunayajua, basi tukayafanye mara mbili zaidi tulivyokuwa tukifanya zamani. Tutapanda kutoka uchumi wa kati wa chini kwenda uchumi wa kati wa juu, hili linawezekana. Hilo ni jambo la pili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu linahusu kufanya kazi kwa juhudi kubwa. Haukuwepo Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa nikawakumbusha Wabunge juu ya *checklist manifesto*, kuandaa mpango kama huu uliokuja halafu mnakuwa mna-*tick* kimoja kimoja mnachokifanya baadaye kwenye siku ya pili au mwaka wa pili mnahama na yale ambayo hamkuyatimiza huko nyuma. Lazima tuwe na *checklist manifesto* ya namna ya kutekeleza mambo yote tunayoyapanga kwenye mpango huu na tuanze moja baada ya lingine na tupange vipaumbele vyetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika huwa inateseka na tatizo kubwa sana la kupanga *priorities*. Sisi tukatae, sisi tuwe watu tunapanga *priorities* zetu sawasawa, tunaanzia hapa kwa sababu ni muhimu, tunakuja hapa, tunakwenda hapa, tunakwenda pale. Watu tufanye kazi, Rais wetu anafanya kazi sana. Tuna Rais mchapa kazi, Rais *visionary*, lazima tumuunge mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais huyu hana maneno mengi na hazungumzi sana. Mfano, juzi alikuwa Mwanza akasema huko Dar-Es-Salaam nikija nikute shule imejengwa; imejengwa haijajengwa?

WABUNGE FULANI: Imejengwa.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo ndiye Rais tuliye naye tufananye nae Watanzania wote tufanye kazi kwa nguvu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kusoma vitabu. Kaka yangu Waziri wa Sheria aliwahi kuniambia

msemo mmoja niurudie hapa, akasema ili ufanikiwe lazima uwe na kitu kinaitwa Bibliophilia, yaani usome sana vitabu. Sijasoma sana lakini napenda kusoma sana vitabu. Nimesoma kitabu cha Jack Welch, Jack Welch *is a number one general manager in the history of the world*. Huyu ndio aliyetoa *General Electric* kwenye kufilisika mpaka kuwa *number one company in America*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jack Welch alisema ili uongoze watu lazima ufanye mambo mawili. La kwanza uwaongoze kwa *compassion*, kwa kuwasukuma au uwaongoze kwa *persuasion*, kwa kuwasihi na kuwabembeleza wafanye kazi. Hapa Tanzania na Afrika Jack Walsh angekuja kufanya kazi hapa angefilisika. Kwa sababu hapa Tanzania ukitaka kuwapeleka watu kwa kuwabembeleza kazi haziendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina kampuni binafsi; nilijaribu *persuasion* ikanishinda nikaamua kutumia *compassion* kwamba anayetaka kusukumwa anasukumwa anafanya kazi anayetaka kubembelezwa anabembelezwa anafanya kazi. Hapa Afrika mambo yote mawili yafanye kazi. Rais wetu anataka kazi. Ukipewa jukumu lifanye kwa nguvu zote ndiyo tunaweza kutoka hapa tulipo kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye *digital economy*. China wamegundua kwamba, *manufacturing* imeanza ku-*decline*, imeanza kushuka, ndiyo maana wakaamua sasa tuwekeze kwenye *digital economy*, uchumi wa kidigitali, ndio maana wanakimbia kwenye mambo ya 5G tunayaona. Sasa hivi duniani hapa China inaongoza katika mambo ya *digital*, kwa nini alifanya hivyo? Wanataka ku-*cover* lile *gap* ambalo litatokea *manufacturing* itakapo-*fail*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hakuna ubaya kwa sisi kujikita kwenye kutengeneza viwanda, ni sawa kabisa, lakini hebu tuelekezeni na akili yetu upande wa pili kwenye *digital economy*. Kwa nini tunaacha nchi jirani hapa zinajivuna

kama zenyewe ndiyo *Silicon Valley* ya *East Africa*? Tuna vijana wana akili hapa Tanzania sijawahi kuona. Wanagundua vitu vingi, lakini hawana mtaji hawa watoto, wanatoka *UDOM* hapo; wamejifunza mambo makubwa kabisa ya kuleta *solution* kwa changamoto tulizonazo lakini hawana *capital* na hawawezi wakaenda benki leo na *idea* akapewa mkopo, haiwezekani, benki zetu sio rafiki wa masikini. Sasa kama tunaweza kukopesha fedha kwa kijiji milioni 50, kama tunaweza kupeleka pesa kwenye halmashauri kuna shida gani hawa vijana wetu wakapewa *guarantee* ndogo tu kwa benki kwamba, *you have the best idea*, sisi tutaku-*sponsor* wewe utengeneze *application* yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest*, mimi nina *run media company*. Pale kwetu tuna *online radio*, tulihangaika sana tulipopata kazi ya kuweka redio kwenye mabasi ya mwendokasi pale Dar-Es-Salaam, tulikosa *technology*. Tukapata South African *partner* halafu akajitoa, tukabaki tumekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huwezi ukaamini waliotupa *solution* hiyo ni vijana wamemaliza *UDOM* hapa? Vijana wale wametengeneza king'amuzi cha kwao ambacho kinanasa matangazo kutoka ofisini kwetu mpaka kwenye mabasi yote ya mwendokasi. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. ERICK J. SHIGONGO: Watanzania *let us trust our children*, tuwaamini na tuwawezeshe watoto wetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana ni kengele ya pili.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Eric Shigongo. (*Makofi*)

Safari moja nilialikwa na Spika wa Israel. Katika mwaliko ule nikapa nafasi ya kupitishwapitishwa mahali kidogo. Nikakuta kuna vijana zile-*brains*za *form six*na kwenda mbele lakini A tupu ambao ni katika mambo ya *IT* na kadhalika. Wakaniambia sisi Isarael sasa hivi *product* yetu kubwa siyo kilimo, siyo nini, wakaniambia *we are selling brain*, hii ndiyo inatupatia mapato makubwa sana. Sasa hiyo *brain* waliyokuwa wanazungumzia ndiyo hii anayozungumza Mheshimiwa Shigongo. Ndiyo biashara kubwa sasa hivi duniani, *brain*. (*Makofi*)

Tunaendelea Waheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Condester, atafuatiwa na Mheshimiwa Ernest Nollo.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa, niendeleo kukupongeza wewe kwamba katika kipindi chote ambacho mimi nimekuwa nikikufuatilia kuanzia ukiwa Naibu Spika na mpaka sasa hivi umekuwa Spika, kiukweli nafurahishwa na namna ambavyo unaendesha Bunge hili. Mimi niseme kwamba ni miongoni mwa Maspika bora kabisa Afrika ambao wanapaswa kuigwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Rais na niendeleo kusema kwamba hata yeye amekuwa ni *record breaker*. Ni miongoni mwa Marais ambao wameingia kwenye historia, hakuna Taifa lolote kwa sasa ambalo unapotaja jina la Dkt. John Pombe Magufuli hawamjui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuchangia Mpango wa Miaka Mitano na Mpango wa Mwaka Mmoja kwenye eneo la biashara na niendeleo kuongelea kwenye eneo la mipaka. Mimi natamani kuishauri Serikali, kama ambavyo ulisema hapo kwamba sisi Wabunge wawakilishi wa wananchi ndiyo watu wa kwanza kabisa na sahihi wa kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado haijautendea haki mpaka wa lango la *SADC*. Napoiongelea nchi ya Kenya

ina mipaka zaidi ya minne, kuna mpaka wa Sirari, Namanga, Holili, Tarakea na ule ambapo ukipita Tanga unaenda Mombasa, bado yote ile ni Kenya. Nchi moja tu ina mipaka karibu mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali kwa kusema kwamba, *there is no way* Zambia itakuja kupata bahari. Dunia imeumbwa na itaondoka Tanzania ndiyo yenye bahari. Kwa vyovyote vile nchi zote ambazo ziko Kusini mwa Afrika zinategemea bandari ya Tanzania kutoa vitu vyao kutoka kwenye nchi za Ulaya na bado wanatarajia kupita Zambia kwa ajili ya kupeleka kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo, naweza nikasema kwenye lile geti moja tu la pale Tunduma ni mpaka ndani ya mpaka. Unaonekana tunapakana na Zambia, lakini nyuma tumebeba nchi nyingi. Je, Serikali haioni sababu ya kupanua mpaka ule ili tuendelee kunufaika nao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea sehemu zile za Tunduma. Kumekuwa na wimbi kubwa sana la ndugu zetu kutoka vijijini, hata kwenye Kijiji changu ambacho mimi natoka, wapo wafanyabisahara pale wanasukuma baiskeli tu kwa ajili ya kupokea mizigo, lakini unapokuwa Tunduma hakuna biashara yoyote kubwa ya nyumba za kupanga kwa sababu hata Mtanzania wa kawaida ambaye hajui kusoma na kuandika kwa biashara ndogo ambayo anaifanya pale kwenye mpaka ana uwezo wa kujenga na kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaendelea kulalamika kwamba hakuna ajira. Je, hatuoni sababu ya kuboresha mipaka na sehemu nyingine hata wale wa darasa la saba mipaka itakapotanuliwa watakuja kupokea mizigo ya wageni, watajipatia riziki kwa sababu Mungu hakutuumba watu wote tukafanana ndiyo maana kuna Rais, Waziri, mwalimu wa shule ya msingi na kuna msukuma mkokoteni. Kwa hiyo, tutumie fursa tulizonazo kwa ajili ya kutatua matatizo. Bora kidogo cha halali kuliko kikubwa cha haramu, hata Maandiko Matakatifu yanasema, aliyenacho huongezewa asiyekuwanacho hunyang'anywa hata kile alichokuwanacho, lakini sisi tunavyo hatuvitumii sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano ule ambao nilitaka kutoa nilipoishia, ni kwa namna gani biashara za magendo zinavyotoka zile nchi za Kusini mwa Afrika na hata nchi za Afrika ya Kati mfano Kongo. Kwa mfano, nikiongelea vipodozi, vipodozi vya kutoka Kongo vimekatanzwa kuingia hapa nchini Tanzania inachukuliwa ni magendo, lakini ukipita huko Dar-Es-Salaam na sehemu nyingine, bado unakuta *carolite* zinanzwa, zinapitaje kama pale *patrol* inafanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Jimbo la Momba. Unapokuwa pale *Livingstone*, Zambia, mtu anapotoka na bidhaa Namibia, Zimbabwe au Botswana, anapoingia Lusaka unafika mji mmoja unaitwa Mpika, pale kuna njia mbili njiapanda. *Whether* uamue kwenda Ndola ambapo uende *border* ya Kasumbalesa kule mtu achukue vile vipodozi. Anapokuwa pale Mpika ana uwezo wa kuamua kupita barabara ya Tunduma atokee pale lilipo lango la *SADC* au aamue kupita mahali kunaitwa Kasama kutokea *Mbara Road* anaingia upande wa Jimbo la Momba ambapo kutokea inapoanzia Tanzania kuingia *tarmac* ya Zambia ni kilometa moja tu na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliyesimama hapa ni *living testimony*, natoka kwenye kata ya mpakani, kipindi chote nikiwa nasoma *Mbeya Day*, inapofika kuanzia mwezi wa kumi na mbili, wa kwanza, barabara hazipitiki tunapaswa kwenda kupita Zambia ili tuweze kufika Tunduma, mazao na mifugo mingi inatoroshwa kwa kutumia njia hiyo kwa sababu iko wazi, hakuna utaratibu wowote pale. Serikali kama mnasikiliza ushauri tunaona ipo sababu, iko nia na manufaa ambayo tutayapata pale ambapo tutaongeza geti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kuongezea, kuna soko kubwa la kimataifa ambalo limejengwa ndani ya Jimbo la Momba kwenye Kata moja inaitwa Ndalambo, Kakozi. Ni soko la kimataifa zaidi ya shilingi bilioni 8 Serikali imeweka pale. Kwanza, Serikali yenyewe iliona kwamba ni soko la kimataifa la mazao na mifugo lijengwe kwenye mpaka. Sasa kama limejengwa kwenye mpaka soko hili litachochewa na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutataka tena kutoa mazao ambayo yanatoka Rukwa, Jimbo la Momba yaende yakapite Tunduma? Hizi halmashauri nyingine zinakuwaje? Zinawezaje kujitegemea kama haziwezi kusimama, mazao yote yanatoka yanaenda Tunduma na hili soko? Pia lilipo soko ndipo ilipo barabara ambayo inapita kwenda kwa baba yangu Mheshimiwa Kandege kwenda kwenye bandari ya Kalemii. Kwa nini kusiwe kuna sababu ya kupata geti? Tunaiomba na kuishauri Serikali tupate geti mahali hapo ili tuweze kuzuia biashara zote haramu na za magendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea, kumetokea migogoro mingi sana ya ardhi, kutokana na kwamba tuko mpakani *Congolese* na *Zambians* wengi wanawatumia Watanzania hawa kwa ajili ya kuja kumiliki ardhi kwa sababu ni kwenye mpaka. Tunaiomba sana Wizara yenye dhamana husika jambo hili muliangelie kwa karibu sana. Tunaomba Wizara ya Ardhi ifuatilie hati zote ambapo watu wanaonekana wanapata hati ndani ya Halmashauri ya Momba na muda mwingine ni wafanyabiashara hawa wanavaa uhusika wa Tanzania lakini wanawalinda hawa watu ni wahamiaji. Sheria ya Ardhi ya Tanzania inamkataza mtu yeyote asiyekuwa Mtanzania kumiliki ardhi. Kama anataka kumiliki kama mwekezaji ziko sheria ambazo zina mwongozo mtu huyo ni kwa namna gani anaweza kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea hapohapo kwenye suala la ardhi. Sisi watu wa Halmashauri ya Momba na halmashauri nyingine ambao wanapitia changamoto kama hii, hatutamani kuona tunafika kwenye matatizo ambayo ndugu zetu wa Kiteto na Morogoro wanayo. Limetokea wimbi kubwa la wawekezaji ndani ya Jimbo la Momba kutokana na ule mwamko wa lile soko kuwepo na ule mpaka, kuja kumiliki ardhi kinyume na taratibu. Kaka yangu Mheshimiwa Kunambi alisema pale, tunaomba ardhi ambayo inaonekana iko sehemu ambayo ni muhimu, kwa mfano sehemu kama hizi za mipaka, kwa kuwa wananchi wa maeneo haya wengi wao wanakuwa ni watu wa kipato kidogo, Serikali iingilie kati iyapime yale maeneo. Itusaidie

kuyapima siku zijazo yatatusaidia kwa sababu tunajua tu lazima mpaka utafunguka, biashara nyingi zitafanyika na ardhi itapanda thamani mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji hawa cha kwanza wanamiliki ardhi kinyume na taratibu. Mtu anamiliki ardhi eka 800, lakini amepata hati ambayo amepewa na Kijiji au mtu anamiliki ardhi zaidi ya eka 100, kutoka eka 50 mpaka eka 100 alipaswa angalau apewe na halmashauri, lakini anasema ana hati ya Kijiji. Wanamiliki ardhi kinyume na taratibu lakini hawaziendelezi ardhi hizi pia hawalipi kodi ya ardhi. Wao ndiyo watu wa kwanza kuchukua sheria mkononi na kuanza kuwaweka watu ndani. Wao wameshavunja sheria tatu, lakini wanawaweka watu ndani.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Ernest Nolla, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nafurahi kupata nafasi hii niweze kuchangia kuhusu Mpango huu uliowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu zaidi nataka nijikite kwenye suala zima la kilimo. Wachangiaji wengi wameonesha namna gani tunaweza kuendelea kwenye suala zima la kilimo. Ni dhahiri kwamba, nchi za Afrika tumekuwa tuna-*export* zaidi madini kwa maana ya *extractive* lakini tumekuwa hatufanyi vizuri katika ku-*export* mazao ya kilimo. Kwa hiyo, nataka nirudie na kusema kilimo tunahitaji

wawekezaji lakini vilevile tunahitaji Serikali iwekeze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nataka nijikite zaidi kwa Mkoa wa Dodoma. Mkoa wa Dodoma unachukuliwa ni mkoa ambao hauwezi kustawisha mazao na kilimo kiko chini lakini tujiulize ni kiasi gani cha maji kinachopotea katika mkoa huu. Nianzie tu karibu pale Kibaigwa, lile bonde linavyotoa maji kwenda kule. Nenda Mpwapwa ile milima na mabonde yale, nenda hadi Mto Ruaha pale, anza kushuka njoo huku Dodoma, ingia Chalinze hapa uende hadi Bahi kule na *swamps* zote zile, lakini maji haya miaka nenda rudi yamekuwa yanapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kwenda *Egypt*. Ukifika *Egypt* huwezi ukadhani kama uko kwenye jangwa. *Egypt* baadhi ya watu hawajawahi kuiona mvua maana mara nyingi inanyesha mara moja tena ni vinyunyuu kwa mwaka na kama umelala huioni tena, lakini ni nchi ambayo *it is very green* kuanzia Cairo mpaka Alexandria, nchi yote imestawishwa kwa umwagiliaji. Naichukulia Dodoma iko sawasawa na *Egypt* na Israeli. Tena nazilinganisha tu basi lakini sisi hatuwezi kulinganishwa na Israel na *Egypt*, sisi tuko *better off*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu za mwaka 2017, *export value* ya *Egypt* katika mazao ya kilimo ilikuwa ni Dola bilioni 2.2. Ukija Tanzania *export* ya mazao ya kilimo ilikuwa ni Dola 8,000,030 na hiyo siyo kwenye *hotculture products* ni mazao ya pamba, chai na kahawa. Kwa hiyo, nachotaka kusema ni kwamba tuna nafasi kubwa ya sisi kuweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Dodoma hapa tuna zao la zabibu lakini hatujalitendea haki. Nchi ya Israel imeweza ku-*export* ule mchuzi kwa thamani ya Dola milioni 240 kwa mwaka lakini zabibu ya Dodoma ndiyo zabibu ambayo unaweza kui-*train* izee muda wowote unavyotaka. Zabibu ya Dodoma wanasema ni nzuri katika dunia nzima kwa maana ya sukari lakini na namna ya ku-*train* kwamba iweze

kuzaa. Unaenda hivyo hivyo Egypt, wenzetu wako mbali kwenye kuuza mchuzi wa zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hoja yangu kwanini nataka kusema kwamba Serikali iwekeze kwenye kilimo. Tunahangaika kuchimba maji ya chini, tunatafuta maji *underground* huko kwenye miamba maji ambayo hatuyaoni ndiyo tunahangaika nayo, lakini maji yanayopita kila mwaka hapa mwaka huu yatapotea na mwakani yatapotea, hivi hatuwezi kweli tuka-*tap* maji haya yakutosha na tukaweza kulima kwa uhakika muda wote. Naamini kabisa Mkoa wa Dodoma huu unaweza hata ukalisha kwa kiasi kikubwa kulisha hata nchi yetu kwa maana ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ardhi nzuri, ina rutuba lakini tunaenda hadi lini kwa utaratibu huu, maji yanapotea muda wote na nataka niseme wenzetu wamejikita zaidi kwenye *hotculture* ambayo kwanza hutakiwi kutumia maji mengi, ni maji yanaenda kwa utaratibu,acha hii *massive* kama tunavyomwagilia katika mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, nataka niishauri Serikali kwamba hebu tutoke kwenye kutafuta maji chini ya ardhi, tutumie maji haya ambayo tunayo kwenye mito. Wakati tuko Egypt nilikuwa kwenye *delegation*, mkuu wetu wa msafara aliulizwa kwanini Tanzania mna maji lakini bado hamfanyi vizuri kwenye kilimo. Tulienda kwenye shamba la ng'ombe 35,000 jangwani Egypt, kwanza yule mwenye shamba alihojiwa akaulizwa na Waziri wetu kwamba

MWENYEKITI: Ng'ombe 35,000?

MHE. ERNEST K. NOLLO: Ndio ng'ombe 35,000.

MWENYEKITI: Kongwa *Ranch* ng'ombe hawafiki 10,000, endelea tu Mheshimiwa.

MHE. ERNEST K. NOLLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo shamba lile linalima nyasi kwa umwagiliaji jangwani na sera ya Egypt ni kwamba unaweza ukapata maji kwenye

Mto Nile, lakini mtu wa Egypt anasema unatakiwa uchimbe kama hujayapata hujachimba. Kwahiyo mtu wa Egypt ataenda chini *miles* na *mile* lazima ayapate maji. Hii *spirit* na maji tuliyonayo hata Mwenyezi Mungu nataka niseme anatushangaa na atatushangaa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka miujiza gani na maji haya tuliyonayo, ile pale nimetoa mfano pale Kibaigwa, kuna kipindi utadhani ni bahari, lakini maji yale yanapotea. Njoo kwetu Bahi sasa tuna-*swamp* ambayo imejaa maji kwelikweli, lakini hatuwazi kulima nyasi kwa kumwagilia, tupate maziwa yakutosha muda wote, hatuwazi maji yenyewe yatutosheleze, hatuwazi maji kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tungefanya hata anasa kama Kazakhstan, walichofanyawaliamia mji mpya ule wa Almaty, wakasema sasa tutengeneze kabahari, wakatengeneza bahari, maana waliona watu wengi wakiwa wana-*relax* kama ilivyo Dar es Salaam wanaona bahari, ikaja kujengwa bahari, ni matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uwekezaji kama wa umeme na reli ni gharama kubwa sana, lakini na hili nalo tulifanye, hivi kweli Serikali kwa maana tumetoa sasa ma-*exavetor* mwezi mzima wanachimba, hatuwezi kupata bwawa kubwa ambalo tutaweza kumwagilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo wenzangu wengi wamesema kwa habari ya mafuta, *edible oil*. Tumeongea sana, hivi ukatoa viwanda viwili tu pale Singida viwe vya bilioni 700, bilioni 500 tunamaliza kabisa habari ya *edible oil* kwenye nchi hii. Tuache habari ya kwamba tukuze michikichi baadaye tuanze kupata mafuta, lakini alizeti tukiamua miaka miwili hii tunamaliza habari yaku-*import edible oil*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini kwa kweli nataka niseme Serikali jambo hili la uwekezaji kwenye kilimo tulichukulie *serious*, kwa maana ya kwamba hatuwezi

kuwekeza kushindana kama alivyosema muwasilishaji alisema tunataka tuwe na ushindani wa kibiashara, lakini nashindana na nani katika sekta ipi? Sisi mashindano yetu yawe kwenye kilimo, tulikuwa na wenzenu akina Malaysia, akina Hongkong na akina Singapore, wale walikuwa ni wenzetu, lakini sasa wameshatoka kwenye uzalishaji wa kilimo wako kwenye teknolojia lakini sasa sisi tuko na wenzetu washindani kwenye sekta ya kilimo bado tuna *lag behind*, kwahiyi tunashindana vipi? Nataka niseme kwenye mambo elekezi *serious* kwa maana ya kwamba sisi tuko kwenye *stage* ya uzalishaji kwenye teknolojia hatupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio kile ulichokuwa unasema kwamba ku-*export brain*, ile ni *service industry* ambayo sasa dunia ya wajanja na wameshafikia hapo tunawapataje akina Heron Max, tunawapataje hawa jamaa wa *facebook*, kile ndiyo kitu cha msingi sasa, unatengeneza kitu kidogo lakini unatoa *billions of money*, sasa huko sisi hatujafika, lakini mambo mengine haya kwa mfano ya uwekezaji wa watu wetu, tunaweza tukafanya na tukaweza kupiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi kwa mchango wako. Nilishakutaja Dkt. Kimei na utafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa muda huu uliniopa nizungumze. Ninayo mengi kidogo, kwahiyi nitaenda moja kwa moja kwenye mjadala huu. Pia nikupongeze wewe kwa namna ambavyo unatuongoza, kusema kweli inatupa hamasa kubwa sana kuwa Bungeni hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja Mpango ambao umewasilishwa hasa kwasababu nafikiria kwamba mpango huu una uhalisia kwa kiasi kikubwa. Uhalisia kwamba *assumptions* zilizotumika kwa mfano ya kusema kwamba

tunaweza tukaongeza pato la Taifa mwaka ujao kwa 6.3%, wangeweza wakasema 7%, lakini wamesema 6.3%, naamini ni *achievable* kwasababu ya misingi ambayo tumeijenga. Naamini kwamba kuna mambo mengi ambayo yanaweza yakatuteteresha kwasababu hatujajua dunia ina kwenda wapi kwasababu ya wingu ambalo bado lipo kuhusiana na *corona* kwenye nchi za nje, lakini naamini endapo hali itabadilika kidogo tunaweza tukafikia hiyo 6.3% kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana pia wastani wa 8% utafikiwa mwishoni mwaawamu, lakini inawezekana pia hata 7%, ni nzuri sana kwasababu wale wanaojua kanuni ya ukuaji *cumulative*(limbikizo la ukuaji) wanaita ni *the low of cumulative growth*. Kama unaongeza pato lako kwa asilimia 6.0 kwa mwaka unaweza uka-*triple* hiyo kwa miaka siyo zaidi ya miaka 10. Kwahiyo naamini kwamba tunaweza tukafikia hiyo nanihi yetu ambayo ni pato la uchumi wa kati, kiwango cha juu. Kwahiyo naamini tupo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nakosa tu kwenye huu Mpango, nilikuwa natamani sana nione mipango ambayo imekaa fungamanishi kama kwa mfano ulivyokuwa mpango wa *SAGCOT* ambao unaeleza vitu vingi ambavyo vinasaidianaili kuhakikisha kwamba ile *corridor* inatoa kitu. Sasa kuna mipango kama huo wa *SAGGOT* ambao naamini kwamba bado uko unatekelezwa. Nilikuwa nataka tuone kama *logistics map* au *logistics plan* za kufanya Tanzania hususan Dar es Salaam kuwa ni *logistic hub* ya nchi hizi ambazo zinapakana na sisi, lakini sijauona vizuri. Ndiyo tunajenga vizuri *infrastructure* ile ya kutufungulia mipaka na kupeleka vitu kwenye mipaka na tuweze kupata *a lot of value additions*, lakini bado naona haijafungamanishwa sawasawa, ili kuona zile *corridor* tulizonazo zote zitatusaidia namna gani kuongeza kipato chetu bila kutegemea sana vitu vingine ambavyo ni *more primary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba wengi wanasema kilimo, kusema ukweli ni kizuri, lakini nataka kuwatahadharisha kwamba Mheshimiwa yuko sahihi

anaposema kilimo hakilipi kama hatuna viwanda. Bado watakaoweka bei kama tutawauzia *primary product* watakuwa bado ni walaji wa kule nje, ni walaji wa Ulaya na wanapooona kwamba tunataka kufanikiwa watazidi kutubana, watasema bei ziko hivi bei zitaanza kutuvuruga, kwahiyo njia tu pekee ya kuweza kuhakikisha kwamba beiya mazao yetu inaimarika ni kuhakikisha kwamba tuna-*process*, tunauza kitu ambacho kinaweza kihakikishwa, kikafika kwenye masoko tofauti tofauti kwa bei ambayo siyo ile inakuwa *dictated by the consumers*. Kama *consumers* ata-*dictate* bado utapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyosema kilimo lazima tunapokizungumzia tuseme tutafanyaje tukiunganishe na viwanda ili kiweze ku-*process*. Niseme kwamba tumezungumza mambo mengi kuhusiana naukuaji nakadhalika, lakini ni lazima tuzungumzie *strength*. Watu wanapotengeneza *plan* yoyote unaangalia *strength* zako ni nini na ni sawa tukasema ni uongozi bora, amani, utulivu, mshikamano na vitu vyote hivyo na siasa safi, lakini kitu ambacho hatujakiona ni ile *strength* tuliyojenga kwa kutuliza uchumi wetu ukawa tulivu ambao mfumuko wa bei upo chini, wenye *exchange rate* ambayo ni nzuri nakadhalika ambayo inatufungulia milango ya kuweza kuisaidia Serikali yetu kuweza kukopa kwa bei nafuu kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa MWENYEKITI, tunapoangalia mipango hii mara nyingi tunajua tunatumia *cash budget*, sasa tukianza kuzungumza mpango kwa kuanzia kwenye matumizi kwa kuorodhesha vitu gani tunataka vifanywe, kwanza niseme naomba Mungu ajaalie kwamba pamoja na mafanikio tuliopata kwenye miundombinu, kule Vunjo wamesahau. Naomba wasisahau zile barabara zetu kule Vunjo, lakini kama tutaorodhesha kila mtu aorodheshe vitu, the *shopping distance is huge*, TARURA inataka pesa, TANROADs inataka pesa, halafu bado wengine wanasema Serikali ijenge viwanda, hili hapana, Serikali haiwezi kujenga viwanda, zaidi Serikali iwezeshe kwenye viwanda vya kimkakati ambavyo tunatakiwa Serikali kama tunavijua kwenye maelekezo ya hotuba za Rais. Hiyo ya kuwezesha viwanda vya kimkakati

hata kama ikiingia ubia lakini kuhamasisha, sera ziwe safi, *blue print* iwepo, mambo yawe sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli hatuwezi kusema Serikali ikajenge viwanda vya alizeti nakadhalika hatutaweza hiyo, tuwezeshe watu na ndiyo kazi yetu kwenye zile kamati ambazo zinahusika. Kwahiyo nataka kusema hiyo tuwe makini, kwasababu hatuwezi kuorodhesha. Nimejifunza kitu cha msingi sana na nimefurahia sana Wabunge fulani wameanza kusema kwanini tusipate fedha namna hii. Kwasababu cha kwanza ni mapato, je, yanatoka wapi? Kuna Mheshimiwa Shabiby alisema pengine mapato tuongeze tozo kwenye matumizi ya mafuta na tena akatoa pia mawazo ya namna hii, yale ndiyo mambo tunataka tujue kwasababu ukishapata zile fedha ukimpa Rais wetu anazitumia vizuri, anajua kuzisimamia kwa ufanisi, zitazaa vyovyote tunavyotaka, lakini tuangalie na nashukuru wale wanaozungumzia kwamba tuzibe mianya ya pesa kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *tax effort* yetu *we mention* kwenye hizi *documentis* 13%, 12.9% ndiyo *revenue effort* tuliyoifanya mpaka mwaka jana na tunaendelea kusema mwaka unaokuja 13.3% ndiyo *tax effort*, nchi nyingine hata hapo Kenya 23% ya *GDP*, uwiano kati ya mapato ya Serikali na *GDP*, pato la Taifa ni 20%, sisi tunasema 13% ni ndogo sana, ina maana kwamba njia tunazotumia kutoza kodi na njia tunazokusanya mapato yetu ni finyu. Aidha, vile vyombo vyetu vinavyoshughulika na ukusanyaji wa mapato vijijunde upya *vi-think out of the box, what is happening? Effort* yoyote Mheshimiwa Rais aliyofanya kupata hela kwenye madini na nini lakini bado eti *revenue effort* 13% of *GDP is nothing*, tunataka tupate 20% *which means* tunapata 28 trilioni, tunge-*finance* vitu gani? *TARURA* ingepata pesa mpaka tushindwe kuzungumza, lakini ninavyoona ni kwamba kuna kitu kiko hafifu hapo katikati kwenye ukusanyaji, sijui zinaenda wapi hizo hela. Kwanini iwe 13% au sisi tuna *overstate GDP* yetu pengine *I do not know*, lakini kama kweli takwimu ziko sahihi 13% ni ndogo toka tukiwa kule sisi miaka ya 1996, kwahiyo tunazungumza kwamba *effort* yetu lazima ifikie 20%, sasa mpaka leo hii 13%, tuna matatizo lazima tuanzie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tuna-*demand* barabara na vitu vingine, je, mapato yanatoka wapi? Kwasababu hutapata kule kwenye Wizara ya Viwanda wanapata 6%, kilimo wanapata 6% *of approved budget, it will never work*. Kwasababu hiyo tuna *over state* hizi *revenue* ndiyo sababu tunapanga vitu ambavyo ni hewa, havi tatekelezeka, *where is the money? The money is the cash budget*, sasa niseme hivi kwanini nimeanza kusema kwamba tuna *strength* moja ya kukopesha. *Revenue* ya Serikali ya matumizi inatokana na vitu viwili *tax revenue* yaani mambo ya kodi na tozo; pili, mikopo. Sasa mikopo inaweza ikatokana kwenye mabanki ya ndani na *pension funds* nakadhalika yaani vianzio vya ndani, lakini pia zinaweza zikatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nje na tunaambiwa kwamba nanii yetu iko chini sana, yaani uhimilivu wetu wa ukopaji bado tunaweza tuka-*afford* hata mara tano, sasa kwanini tusikope zaidi, tunaogopa nini kukopa kwasababu tunajenga rasilimali, tunajenga mtaji, nchi hii ina *balance sheet* yake, *liabilities and assets*. Watu wanaposema sijui deni hili siyo himilivu, deni walikuwa wanapiga ile *gross* hawaondoi ile rasilimali tuliyotengeneza, *assets* kwahiyo lazima uchukue *asset - liabilities* unapata *net liability* au *net asset*.

Sasa sisi ukiangalia kwa mfano vitu ambavyo vimejengwa Awamu hii ya Tano thamani yake na deni letu, ni kama hatuna deni yaani ukiangalia kwa uhimilivu watu wa Taifa letu, uhimilivu wa *balance sheet* ya kwetu, *network* yetu ni nzuri kwasababu tumekopa tumeweka kule, hata kama tungekuwa tumekopa mara ngap, i tutaingiza kwenye *asset* inazaa vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie...

MWENYEKITI: Tayari ni kengele ya pili.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Sasa nina mengi sana, lakini...

MBUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Dakika 10 ni kidogo sana ndiyo shida yake. Mheshimiwa Riziki Lulida, mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyenijaalia afya njema nikaweza kuchangia katika hoja iliyokuwepo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli kwa huruma na upendo mkubwa aliouonyesha na kuweza kunichagua kuwa Mbunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Nasema Mwenyezi Mungu ambariki na sina la kusema zaidi ya kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu aweze kumtetea na aweze kumlinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa maombi yao na Watanzania kwa ujumla, nasema ahsante. Mwisho, nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa upendo walionionyesha na hata mimi kunipa moyo na kuniongoza na kunifikisha hapanilipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja ambayo ni ya muda mrefu, lakini Mheshimiwa Rais baada ya kunichagua nimeona nije na hoja yangu. Naomba Wabunge wenzangu mniunge mkono na muitambue kama hoja hii ni kwa maslahi mapana ya nchi yangu. Mwaka 1905 mpaka 1906 katika eneo la Tendeguru, Wilaya ya Lindi Vijijini, Mkoani Lindi walichukua mabaki ya mjusi kupeleka Ujerumani. Mwanzo nilikuwa nadhani ni mabaki yale ni ya mjusi mmoja, kumbe na mijusi

sita,lakini nazungumza kwa uzalendo na uchungu wa kuhakikisha haya mapato ni lazima yawasaidie Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama mimi sitatumia lakini kuna watu wanahitaji mapato hayo kwaajili ya elimu, barabara, afya na kadhalika. Ujerumani wamepeleka lile jusi na Watanzania kutoka Lindi wallibeba kichwani jusi moja lilikuwa na uzito wa tani 250 kutoka Dendeguru mpaka kufika Kilwa tu kwenye Bandari, basi ujue wametembea kilomita 150, wameteskaje watu kama hawa, wengine wamepoteza maisha yao ukichukulia kipindi hicho kilikuwa ni kipindi cha wanyama wakali; je, wale wananchi wa kule wameangaliwaje, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Tunaambiwa kuwa wao kwa mwaka wanakusanya *Euro* milioni 278, ukifanya *calculation* za haraka ni sawasawa na bilioni 834, sisi kama Tanzania hatujapata chochote. Ukiwauliza wanasema zile pesa zimejenga *museum* kule kwao, zinatumika kuwalipa mishahara watu wanaomtunza, zinalipa hela za tafiti mbalimbali, zinawawezesha wanafunzi wanaokwenda pale kujifunza wanatumia nafasi ile. Nasema haiwezekani na wanasema wameingia mkataba na Umoja wa Mataifa kuwa haiwezekani huyo mjusi kumrudisha Tanzania, hakuna kisichowezekana katika ulimwengu huu wa Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabilioni yale 834 wanayoyavuna Wajerumani hata kule anapotoka mjusi yule hawapathamani. Sisi Tanzania ndio *owner* wa yule mjusi na Watanzania mfunguke na siyo kila wakati mnataka kubeza, mbona kama mngekuwa naye Tanzania msingeweza kumfanyia chochote, je, kama nao wangemwacha wangepaidika, wasingepaidika naye. Ina maana kuwepo kwa mjusi yule kwao ndiyo wamefaidika. Leo dunia unaisikia inavyozungumza wanaitegemea Afrika ife ili wachukue rasilimali zetu na walikwenda pale kuchimba madini. Hivyo Ulaya unayoiona, dunia ya kwanza unayoiona ilitajirika kwa kupitia Afrika. Wametegemea dhahabu, almasi, *copper, zinc,*

shaba kutoka Afrika lakini sisi wenye Afrika hatujitambui na wala hatujielewi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao, wanahitaji viwanda vyao vifanikiwe na ili vifanikiwe wanahitaji *raw material* kutoka Afrika. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais anasema tunahitaji viwanda kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya nchi yetu. Haya mazao yetu badala ya kupelekwa Ulaya yatafanya kazi hapa hapa tutawapelekea vitu ambavyo tumevi-*process* Tanzania. Tuangalie kipindi hiki tunachokizungumza cha *Corona* hatuwezi kuleta chochote kutoka nje lakini kama viwanda vyetu vingefanya kazi, nani angeagiza khanga kutoka India au China, tungekuwa na khanga zetu kutoka urafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mjusi tumeunda Kamati, naomba uridhie na uingize ndani ya *Hansard* na uitambue kama Wabunge wako wamejitolea rasmi kuhakikisha haya mapato yanakuja Tanzania. Nataka niwatambue Wabunge ambao wako tayari akiwemo Mheshimiwa Kigua, Mheshimiwa Reuben Gwagilo, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Juma Hamad, Mheshimiwa Maimuna Patani na wengine watakoajitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mapato yaje Tanzania na siyo mapato tumekwenda kufanyiwa *presentation* Wizarani neno la kukatisha tamaa la kwanza wanasema haiwezekani hata mfanyaje mkafanikiwa. Mimi nasema inawezekana na tutafanikiwa. Lugha ya kukatishana tamaa Tanzania tuiache. Katika maisha yangu sina uwoga, nikipambana na kitu changu nasema hiki kitu kitafanikiwa na nasema nitafanikiwa. Ndiyo maana nakwenda sambamba na nyayo nafuatilia miguu *step by step* ya Mheshimiwa Rais kwa ajili ya mafanikio. Mheshimiwa Rais hana woga, ametishiwa sana, ameambiwa sana kuwa haiwezekani lakini yamewezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hoja ya madini imewezekana na hii hoja nahakikisha kuwa itawezekana. Nachoomba ni ushirikiano wa Wizarata mbalimbali zinaguswa

na hoja hii. Kama waliona mapambano haya hayaweze kani hata kama mimi naondoka lakini bado kuna wanaharakati wako humu ndani ya Bunge ambao watakwenda sambamba na tutashinda vita hii na kuiletea mapato nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alinipigia simu Balozi akaniambia Mama Lulinda usirudi nyuma na mimi nimemwambia niko na wewe sirudi nyuma. Ananiambia panafanyika mafunzo mbalimbali ya watu duniani kwenda kusoma kwa nini mji ili mikubwa imetoka Tanzania, sisi wenyewe Tanzania tuko wapi? Hatupo! Tuna watoto wamesoma wanahitaji kwenda kufanya *exchange program* kwa nini wanawachukua watoto kutoka Marekani, watoto wa Tendeguru wako wapi? Kuna watoto wamemaliza shule tunataka Wajerumani wakawasomeshe watoto wale ili tukijenga *Museum* kule Tendeguru basi na wao wawaeleze hapa ndipo palitoka *fossil* za mji kutoka Tanzania. Hivyo *exchange program* ya elimu naomba iwepo katika mkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, watu wa *University of Dar es Salaam* wanakwenda kuchukua *fund* kwa ajili ya kufanya *research*...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia ni dakika moja Mheshimiwa Lulida muda umeisha malizia.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Niendeleo?

MWENYEKITI: Malizia maneno yako ya mwisho.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *research University of Dar es Salaam* wanachukua pesa, watu wa Makumbusho wanachukua pesa lakini wanachukua *fund* zile bila kuwa na

utaratibu. Nachoomba sasa hivi pawepo na utaratibu Wajerumani waje kukaa na Tanzania tuwe utaratibu maalum haya mapato yaweze kuisaidia nchi yetu. Kwa mwaka wanapata Euro milioni 278 sawasawa na bilioni 834 Tanzania tunapata nini? Tunaomba Wizara...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lulida amekuwa akiongelea sana habari ya mjesi huyu mpaka watu wengine na yeye mwenyewe wanamuita mjesi lakini hoja yake ni ya msingi sana. Siku za nyuma hoja kubwa ilikuwa ni kumrudisha Tanzania yule *Dinosaur*, baadhi ya watu wakatutishia wakasema hata kwenye Bunge hili hatoshi. Tukasema, eeh, basi bora akae huko huko. Hata hivyo, hoja yake ya kusema kwamba tunaweza tukapata mapato fulani ni ya msingi sana, tutafanya kazi pamoja kuona tunafika hatua gani katika jambo hilo. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea, Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake kwa sasa.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, mjadala umeenda vizuri na muda wetu haupo upande wetu kwa sasa. Mjadala wetu utaendelea kesho na siku inayofuata, wale ambao hamjaongea msikate tamaa ndiyo mwanzo kabisa, naamini wote kabisa tutapata nafasi kwa dakika hizi hizi kumi kumi mpaka siku ya Ijumaa. Ila kila siku asubuhi tuandikishane upya.

Kwa wale ambao wako tayari kesho haya, walioko tayari keshokutwa sawasawa.

Mjadala mkubwa kama tulivyoona leo ni namna gani tunaisaidia Serikali kuongeza wigo wa mapato, tukishakuwa na wigo mpana wa mapato naamini mengine yote yanawezekana, tutakabana kwenye bajeti. Kama mapato huna sijui utagawana nini sasa? Michango imekuwa mizuri sana na tuendelee hivyo kwa mjadala wa kesho.

Nina baadhi ya matangazo hapa, tangazo la kwanza linatoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Ummu Mwalimu ambaye anawaomba Wabunge wote wa majimbo peke yao toka Zanzibar wawe na kikao kesho saa 7.00 mchana, tarehe 09 Februari, 2021 mara baada ya kuahirisha Bunge katika Ukumbi wa Msekwa. Wabunge wote toka Majimbo ya Zanzibar mkutane pale Msekwa na Mheshimiwa Waziri Ummu Mwalimu muwe na kikao si kirefu.

Ndugu zetu wa *CRDB* Benki wanawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wenye changamoto za kibenki wanawaomba mfike tawi la *CRDB* Bunge kuanzia Jumatatu tarehe 08 Februari, 2021 hadi Ijumaa tarehe 12 Februari, 2021, wiki nzima hii. Kutakuwa na huduma ya kipekee kwa ajili ya kutatua changamoto hizo mlizonazo. Wabunge wote ambao mna changamoto zozote na *CRDB*. Ukishaona tangazo kama hili si mnaelewa, changamoto, ni kwamba mambo yameanza. Wale waliodhania ziko nyingi sana ndiyo changamoto hizo, muende mkaangalie huko. (*Kicheko*)

Kuna semina ambayo inawahusu Wabunge wote ambao ni Wanachama wa UWT ndani ya Bunge, semina hiyo maalum kwa ajili ya Wabunge Wanawake Wanachama wa UWT kutoka kwenye Majimbo, UWT ambao ni wateule wa Rais, UWT ambao ni Viti Maalum itafanyika tarehe 13 Februari, 2021 siku ya Jumamosi kuanzia saa 2.00 asubuhi katika ukumbi wa *NEC*, kule *White House*. Kwa hiyo, mnaombwa Wabunge wanawake siku hiyo muweze kuhudhuria mafunzo hayo maalum.

Basi Meza yangu imekamilisha kila kilichopangwa siku ya leo, kwa jinsi hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.50 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 9 Februari, 2021, Saa Tatu Asubuhi)